UNIVERSITY of RWANDA

SKULI YA ELIMU
NDAKI YA ELIMU

# UKUZAJI WA TAFAKURI BUNIFU KUPITIA UFUNDISHAJI WA FASIHI KWA WANAFUNZI WA KISWAHILI SHULE TEULE ZA SEKONDARI WILAYANI KICUKIRO

**NA**


**Emmanuel NIYIRORA**
**NAMBARI YA USAJILI: 219016001**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**JUNI, 2022**

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, Emmanuel Niyirora ninatibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu ya asili na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwwa ajili yaa kutunukiwa shahada yoyote, au kwa ajili ya shughuli za kitafiti.



Tarehe :13/06/ 2022

# ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kuwa tasnifu hii yenye anwani ya **" Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Ufundishaji wa Fasihi kwa Wanafunzi wa Kiswahili Shule Teule za Sekondari Wilayani Kicukiro** " imefanywa chini ya usimamizi wake na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu.



Dkt. W. K. Mlaga (PhD)
(Msimamizi)
Tarehe 13/06/ 2022

# SHUKRANI

Kwanza, shukrani za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha katika kazi zote, kunirehemu na kuniwezesha kutimiza kazi hii ya utafiti.

Pili, ninamshukuru msimamizi wangu Dkt. Wallace Kapele Mlaga kwa ushauri wake na kuongoza tasnifu hii. Ninamshukuru sana kwa usimamizi wake mzuri tangu katika utayarishaji wa pendekezo la utafiti na uandishi wa tasnifu kama ilivyo hivi sasa.

Tatu, ninamshuru sana mke wangu Akimana Floride kwa uvumilivu wake na kuwatunza watoto wangu wakati nilipokuwa nasoma masomo yangu.

Nne, nawashukuru wazazi wangu kwa kunizaa na kunitunza kuanzia shule za msingi hadi ninapofika katika Chuo Kikuu.

Tano, shukrani zangu za dhati ziwafikie walimu wote walionifundisha kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu. Katika Chuo Kikuu cha Rwanda ninawashukuru Prof. Niyomugabo Cyprien, Dkt. Wallace Mlaga, Bw. Ntawiyanga Sylvain, Dkt. Stephanie Kolbusa, Bw. Basigayabo Pascal na Bw. Bazirushaka Isaie. Walimu hawa walinifundisha vizuri na walinitakia ufanisi kwa kunifaa kila nilipohitaji msaada wao. Mwenyezi Mungu awatunukie tunu tele. Isitoshe, shukrani pia ziwaendee wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu.

## TABARUKU

Kwa Mwenyezi Mungu,

Kwa wazazi wangu,

Kwa mke wangu mpendwa,

Kwa watoto wangu,

Kwa ndugu na marafiki zangu,

Nawatabaruku kazi hii.

.

# Ikisiri

Tasnifu hii imetokana na utafiti uliokusudia kuchunguza Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Ufundishaji wa Fasihi kwa Wanafunzi wa Kiswahili, Shule Teule za Sekondari Wilayani Kicukiro. Utafiti ulikuwa na malengo mahususi mawili: kubainisha nafasi ya fasihi andishi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda, na pia kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Ili kukamilisha malengo haya mahususi, data za msingi na data za upili zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, uchanganuzi matini na usaili. Wango la utafiti huu lilikuwa walimu wa Kiswahili na wakuu wa masomo walioteuliwa katika shule za sekondari Wilayani Kicukiro. Sampuli ya utafiti ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Aidha, utafiti ulitumia mkabala wa kitaamuli. Uchanganuzi na ufasiri wa data uliegemezwa kwenye Nadharia ya Utambuzi. Licha ya matokeo ya utafiti kuonesha kuwa fasihi ina nafasi muhimu katika ufundishaji wa tafakuri bunifu, ilionekana kuwa baadhi ya walimu hawafanikiwi kujumuisha stadi ya tafakuri bunifu sio tu katika maandalio ya masomo, bali pia katika ufundishaji na tathmini. Hii inatokana na sababu zifuatazo: Walimu kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu na utekelezaji wa MUU, muda mfupi wa kuandaa kazi za ufundishaji na majukumu mengi ambayo walimu wanapaswa kutimiza. Ili kukabiliana na vikwazo hivyo, matokeo ya utafiti yamebainisha mwongozo unaopaswa kufuatwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Mwongozo huu unaweka mkazo katika utumizi wa: kazi za makundi, kazi za uigizaji, kazi za fikiri-jozi-changia na midahalo. Aidha, matokeo ya utafiti yamebainisha mikakati tofauti inayoweza kutumiwa na walimu wa fasihi ili kuimarisha stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Mikakati hiyo ni pamoja na utumiaji wa michezo ya maneno, maswali bunifu, kazi wazi, hadithi duara na matumizi ya maswali ya mafumbo. Mwisho, tasnifu hii imedhihirisha mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa kuegemea katika mwongozo wa utumizi wa fasihi katika kukuza tafakuri bunifu. Aidha, tasnifu hii inapendekeza kwamba wadau wote wa sekta ya elimu wanalazimika kuungana mkono ili kuimarisha ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu na stadi nyingine za karne ya ishirini na moja miongoni mwa wanafunzi.

## YALIYOMO


IKIRARI NA HAKIMILIKI .......... ii

ITHIBATI YA MSIMAMIZI .......... iii

SHUKRANI .......... iv

TABARUKU .......... v

Ikisiri .......... vi

YALIYOMO .......... vii

ORODHA YA VIELELEZO .......... xii

ORODHA YA VIFUPISHO .......... xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Utafiti .......... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 5

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.4.1 Lengo la Jumla .......... 5

1.4.2Malengo Mahususi .......... 6

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 6

1.7 Mawanda ya Utafiti .......... 7

1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui .......... 7

1.7.2 Mawanda ya Kijiografia .......... 7

1.7.3 Mawanda ya Kimuda .......... 8

1.8 Vikwazo vya Utafiti .......... 8

1.9 Mpangilio wa Ripoti ya Utafiti .......... 9

1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ... 9
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ... 10
2.1 Utangulizi ... 10
2.2 Dhana ya Tafakuri Bunifu ... 10
2.3 Tafakuri Bunifu na MUU ... 10
2.4 Tafakuri Bunifu na Lugha ... 11
2.5 Tafakuri Bunifu dhidi ya Tafakuri Tunduizi ... 13
2.6 Tafakuri Bunifu na Utatuzi wa Matatizo ... 14
2.7 Mwongozo wa Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi ... 15
2.7.1 Utumizi wa Taswira ... 16
2.7.2 Utumizi wa Drama Bunifu ... 17
2.7.3 Utumizi wa Sitiari na Analojia ... 18
2.7.4 Ushirikishaji wa Kina wa Wanafunzi katika Sanaa ... 19
2.8 Elementi za Tafakuri Bunifu katika Muktadha wa Elimu ... 20
2.8.1 Udadisi ... 20
2.8.2 Ufyonzaji ... 21
2.8.3 Tafakari ... 22
2.8.4 Msukumo ... 22
2.9 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu ... 23
2.10 Mapengo ya Utafiti ... 24
2.11 Kiunzi cha Dhana ya Nadharia ... 25
2.12 Muhtasari wa Sura ya Pili ... 27
SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ... 28
3.1 Utangulizi ... 28
3.2 Paradima ya Utafiti ... 28
3.3 Usanifu wa Utafiti ... 28

3.4 Eneo la Utafiti .......... 29
3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti .......... 29
3.5.1 Wango la Utafiti .......... 29
3.5.2 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti .......... 29
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa .......... 30
3.6.1 Data za Msingi .......... 30
3.6.2 Data za Upili .......... 31
3.7 Njia za Kukusanyia Data .......... 31
3.7.1 Ushuhudiaji .......... 31
3.7.2 Uchanganuzi wa Matini .......... 32
3.7.3 Usaili .......... 32
3.8 Vifaa vya Utafiti .......... 33
3.9 UUchanganuzi wa Data .......... 33
3.10 Itikeli za Utafiti .......... 33
3.11 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti .......... 34
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu .......... 35
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI .......... 36
4.1 Utangulizi .......... 36
4.2 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu .......... 36
4.2.1 Uelewa wa Walimu kuhusu Tafakuri Bunifu, MUU na Fasihi .......... 37
4.2.2 Namna ambavyo Walimu HufundishaTafakuri Bunifu kupitia Fasihi .......... 41
4.2.3 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Andalio la Somo .......... 45
4.2.4 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Ufundishaji .......... 52
4.2.4 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Tathmini .......... 60

4.3 Mwongozo wa Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu kupitia Fasihi ........ 65
4.3.2 Namna ya Ufundishaji wa Stadi za Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi ........ 66
4.3.3 Mwongozo wa Utumiaji wa Mbinu za Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi ........ 71
4.3.4 Namna ya Kukuza Tafakuri Bunifu Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari ........ 80
4.3.5 Mfano wa Namna ya Kufundisha Fasihi kwa Mwongozo Unaokuza Tafakuri Bunifu ........ 86
4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 93
SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 94
5.1 Utangulizi ........ 94
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 94
5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 94
5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........ 95
5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika ........ 96
5.4Hitimisho ........ 97
5.5 Mapendekezo ........ 98
5.5.1 Mapendekezo kwa Bodi ya Elimu ya Msingi Nchini Rwanda ........ 98
5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu Nchini Rwanda ........ 98
5.5.3 Mapendekezo kwa Walimu wa Fasihi ........ 99
5.5.4 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule ........ 99
5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........ 99
5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano ........ 100
MAREJELEO ........ 101
VIAMBATISHO ........ 107

Mpango Kazi ........................................................................................................................ 107
Mwongozo wa Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili ........................................................ 108
Mwongozo wa Mahojiano kwa Wakuu wa Masomo ............................................................ 109
Mwongozo wa Ushuhudiaji kwa Walimu wa Kiswahili (Darasani) ...................................... 110
Barua ya Wilaya .................................................................................................................. 112
Kibali cha Chuo cha kufanya Utafiti .................................................................................... 113

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelozo 1: Andalio la Somo (1) ........ 46
Kielelezo 2: Andalio la Somo (2) ........ 49
Kielelezo3: Takisonomia ya Bloom........ 61
Kielelezo 4: Mfano wa Tathmini 1 ........ 62
Kielelezo 5: Mfano wa Tathmini 2 ........ 63

# ORODHA YA VIFUPISHO

**Dkt**: Daktari wa Falsafa (PhD)
**G.S:** Groupe Scolaire
**Ihj**: Ishatajwa hapo juu
**Khj**: Keshatajwa hapo juu
**MUU**: Mtaala Unaoegemea katika Uwezo
**REB**: Rwanda Education Board
**TEHAMA**: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
**TY**: Tafsiri Yetu
**Prof**.: Profesa
**Whj**: Wameshatajwa hapo juu

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ya utangulizi inahusisha vipengele vifuatavyo: usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa ripoti ya utafiti.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Katika zama za sasa, mambo mengi yanaonekana kubadilika kutokana na maendeleo ya teknolojia, uchumi, na utandawazi. Mabadiliko haya yamesababisha ulimwengu kuanza kufikiria stadi za ziada za kukabiliana na mabadiliko. Kwa madhumuni ya kukabiliana na mabadiliko haya, kuanzia miaka ya 1980 serikali, waelimishaji na waajiri wametoa maoni yao kuhusu uwezo na stadi zinazohitajika kwa wahitimu wa elimu. Stadi hizi zilipewa jina la stadi za karne ya ishirini na moja (Peck, 2005).

Stadi za karne ya ishirini na moja hufafanuliwa kama uwezo wa mtu unaomwezesha kukabiliana na changamoto tofauti za kimaisha katika mazingira mbalimbali. Stadi hizi ni kama vile tafakuri bunifu, tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, ugunduzi, utafiti, ushirikiano, mawasiliano, utawala binafsi, uwezo wa kusoma na kuandika, TEHAMA, uzalishaji na ujuzi wa kijamii (Sharon, 2019).

Tafakuri bunifu inachukuliwa kama stadi muhimu miongoni mwa stadi nyingine za karne ya ishirini na moja. Stadi hii humwezesha mjifunzaji kuzalisha fikra za kimsingi, mpya, zinazofaa katika utatuzi wa matatizo yanayoikumba jamii ya watu (Young & Chapman, 2010). Hii ina maana kwamba kama mwanajamii, ni lazima kutafuta suluhisho kwa baadhi ya changamoto zinazomkabili kwanza na pengine kutatua matatizo ambayo

yanazuia mafanikio ya jamii yake. Hii ina maana kwamba tafakuri bunifu ni stadi inayohitajika sana katika elimu kwa sababu ina mchango mkubwa katika maandalizi ya wafanyakazi wenye uwezo wa kutatua matatizo yaliyopo. Vilevile, ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu una mchango katika mafanikio na maendeleo endelevu ya watu binafsi, kampuni, viwanda na mataifa (Ford & Gioia, 2000).

Kutokana na maelezo ya hapo juu, inaonekana kwamba stadi ya tafakuri bunifu ni stadi muhimu inayopaswa kukuzwa katika viwango vyote vya elimu ili kumwandaa mwanafunzi mwenye uwezo wa kutatua matatizo yaliyopo katika jamii yake.

Ili kufanikisha haya, baadhi ya nchi duniani zilianza kuimarisha stadi ya tafakuri bunifu na stadi nyingine za karne ya ishirini na moja. Hili linajitokeza kuanzia miaka ya 1980 kwa nchi kama vile Marekani, baadhi ya nchi za Asia, Ulaya na katika Bara la Afrika (Wongnaa & Boachie, 2018). Nchi hizi zilifanya hivi ili kusisitiza ubunifu na utendaji katika michakato ya ufundishaji na ujifunzaji miongoni mwa wanafunzi (Mbarushimana & Kuboja, 2016).

Kwa hiyo, ulianza kutumiwa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo ambao kuanzia sasa tutaurejelea kama MUU. Mtaala huu unafasiliwa na Barman & Konwar (2011) kama mtaala ambao unalenga kuwapa wanafunzi uwezo wa kutumia mchanganyiko wa maarifa, stadi, mwenendo mwema na maadili, na mwenendo mwema katika mafanikio ya kikazi kwenye eneo lao la taaluma. Barman & Konwar (Whj) wanasema kwamba MUU unasisitizia uwezo unaopatikana baada ya ufundishaji na ujifunzaji. Uwezo huu unamwezesha mwanafunzi kutekeleza alichojifunza darasani katika maisha ya kila siku yaani kupata uwezo wa kubuni hoja sahihi ili kutatua tatizo lililopo. MUU

ulianza kutumiwa zamani katika nchi mbalimbali zilizoendelea duniani ukilinganisha na Bara la Afrika. Kwa mfano, nchini Marekani ulianza kutekelezwa mwaka wa 1970, Uingereza mnamo mwaka wa 1990, Iran mwaka wa 1999 (Sotco na Mwandanji, 2015; Wongnaa & Baachie, 2018). Nchini Irani, MUU ulisisitiza uendelezaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia ufundishaji wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza (Kiany, Mahdavy & Ghafar, 2011).

Katika nchi za Bara la Afrika, MUU umeanza kutumiwa hivi karibuni ukilinganisha na nchi zilizoendelea. Kwa mfano nchini Nigeria ni katika mwaka wa 2011, Kenya, ni katika mwaka wa 2016, Tanzania ni katika mwaka wa 2005 na Rwanda ni katika mwaka wa 2015 (Likisa, 2018). MUU ulitazamwa kuwa suluhisho la tatizo lililotokana na mfumo wa elimu ambao uliathiri vibaya ubora wa wahitimu katika soko la ajira.

Kama walivyofanya nchini Irani, inaonekana wazi kwamba stadi ya tafakuri bunifu inaweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza na hata lugha nyingine. Hivyo basi, ni vizuri kuonesha jinsi stadi ya tafakuri bunifu inavyoweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ambayo huchukuliwa kama lugha ya kigeni inayofundishwa kwenye nchi ya Rwanda.

Fasihi kama sanaa ya lugha nayo inaweza kutumiwa katika mchakato wa ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa lugha. Jack (2013) & Brisen (2019) katika utafiti wao kuhusu ukuzaji wa tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi katika lugha ya Kiingereza nchini Uturuki, wamebainisha kuwa ufundishaji wa fasihi katika lugha ya Kiingereza una mchango mkubwa katika kukuza ubunifu miongoni mwa wanafunzi wa lugha. Karpovu (2017) naye alifanya utafiti kuhusu ufanisi wa ufundishaji wa

tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi katika lugha ya Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Midwestern Mjini Arizona. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba ufundishaji wa fasihi unaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa ukuzaji wa tafakuri bunifu hususani kukuza uwezo wa fikra wa wanafunzi.

Kwa jumla, tafiti za watalamu hawa zinaonesha wazi kwamba fasihi ina mchango mkubwa katika kuendeleza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, tafiti hizi zina mapengo tofauti yaliyohitajika kuzibwa na utafiti wetu. Kwanza, tafiti hizi zilifanywa katika nchi zilizoendelea na zilizoanza kutumia mtaala unaoegemea katika uwezo muda mrefu uliopita ukilinganisha na nchi za Bara la Afrika, ikiwemo Rwanda. Pili, hakuna utafiti hata mmoja uliozungumzia kuhusu Bara la Afrika. Tatu, tafiti hizi zilifanywa katika lugha ya Kiingereza. Na mwisho, tafiti hizi zilifanyiwa vyuoni. Hivyo, hakuna utafiti hata mmoja uliozungumzia shule za sekondari. Tuna mtazamo kwamba, ni bora wanafunzi wajengewe mazingira yanayowasaidia kukuza stadi yao ya tafakuri bunifu wakiwa katika viwango vya chini kuliko kuwasubiri hadi wafike vyuoni.

Hivyo basi, utafiti huu ulikusudia kuziba mapengo haya kwa kuonesha namna fasihi ya Kiswahili inavyoweza kushiriki katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda. Hii ni kwa sababu nchi hii ilianza kutekeleza MUU hivi karibuni. Tafakuri bunifu ilichaguliwa kwa sababu ndiyo stadi muhimu katika kuwezesha wanafunzi kutatua matatizo yanayowakabili katika maisha yao.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tafakuri bunifu ni miongoni mwa stadi za karne ya ishirini na moja zinazotajwa kuwa ni muhimu hususani kusaidia kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi wanaokidhi mahitaji ya soko la ajira (Urban, 2007; Birdi, 2012). Aidha, tafakuri bunifu inadaiwa kuwasaidia wanafunzi kumudu stadi za lugha (Little, 1994; Abler, 2013).

Licha ya hivyo, tafiti zinaonyesha kwamba kiwango cha tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kingali kidogo na hivyo kuathiri sana mafanikio ya sekta ya elimu (Chang, 2009; Jack, 2013; Brisen, 2019). Tatizo lililopo nchini Rwanda ni kuwa walimu hasa walimu wa fasihi hawakuzi stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Isitoshe, katika nchi ya Rwanda, hakuna utafiti wowote kuhusu namna ambavyo tafakuri bunifu huweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili. Walimu kutokuza stadi ya tafakuri bunifu na kutokuwepo kwa tafiti hizi kumezuia wadau wa sekta ya elimu na watafiti kupata taarifa zinazohitajika kuhusu tafakuri bunifu na ufundishaji wa fasihi. Hii ilituchochea kufanya utafiti wetu katika eneo hili sio tu ili kuona namna gani stadi ya tafakuri bunifu inavyofundishwa na walimu wa lugha ya Kiswahili, bali pia kutoa mwongozo mwafaka wa ufundishaji wa stadi hii. Hii itasaidia kufikia malengo muhimu ya nchi ya Rwanda ya kuanzisha MUU katika ngazi zote za elimu ikiwemo ngazi ya sekondari.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo la jumla moja na malengo mahususi mawili.

#### 1.4.1 Lengo la Jumla

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kutathmini nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu katika shule teule za sekondari Wilayani Kicukiro (tamka kichukiro) nchini Rwanda.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

i) Kubainisha nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

ii) Kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Fasihi andishi ya Kiswahili ina nafasi gani katika ukuzaji wa tafakuri bunifu kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda?

ii) Ni mwongozo gani unaoweza kutumiwa katika ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Ufundishaji wa fasihi una manufaa tele katika ujifunzaji. Little (1994) anasema kuwa ufundishaji wa fasihi hushiriki vikubwa katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika maeneo mbalimbali ya kitaaluma, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Kwa upande wa taaluma, utafiti wetu utatumiwa kama rejeleo na wahadhiri, waelimishaji na wanafunzi wanaojishughulisha na taaluma za fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu utasaidia wahadhiri na walimu katika kuandaa maandalio ya somo na kuimarisha tafiti zaidi kwenye uwanja wa fasihi andishi ya Kiswahili.

Waelimishaji wa fasihi ya Kiswahili hasahasa nchini Rwanda watanufaika kutokana na utafiti huu. Kupitia data zilizochanganuliwa na matokeo ya utafiti, walimu watapata habari za kutosha kuhusu changamoto zinazoathiri kazi yao na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kwa upande wa sekta ya elimu, utafiti huu utakuwa muhimu kwa kuwa utaeleza mbinu zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili ili kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

Utafiti huu pia ulikusanya data kuhusu MUU. Kwa hiyo, utakuwa bora kwa Wizara ya Elimu ya Rwanda, Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda na kwa wapangaji wa elimu nchini Rwanda kwa sababu utawasaidia kupata taarifa kuhusu utekelezaji na matunda ya MUU baada ya miaka kadhaa tangu uanze kutumiwa katika elimu nchini Rwanda.

Mwisho, watafiti watakaotaka kufanya utafiti kuhusu mchango wa MUU na ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu wataitumia kazi hii ya utafiti kama rejeleo.

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti wetu ulikuwa na mawanda mbalimbali kama yanavyoonyeshwa hapa chini:

### 1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui

Kuna mambo mengi sana ambayo yanaweza kuathiri ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kutokana na wingi wa mambo hayo, utafiti huu ulisisitizia uboreshaji wa ufundishaji wa fasihi ili kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Fasihi ilisisitiziwa kwa kuwa ndiyo nyenzo muhimu inayoweza kufanikisha ufundishaji wa tafakuri bunifu.

### 1.7.2 Mawanda ya Kijiografia

Kwa upande wa jiografia, utafiti huu haukwenda mbali na shule zinazofundisha Kiswahili katika Wilaya ya Kicukiro Mjini Kigali. Eneo hili

lilichaguliwa kwa kuwa lilimwezesha mtafiti kupata taarifa kuhusu ukuzaji wa tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi.

### 1.7.3 Mawanda ya Kimuda

Kuhusu mawanda ya kimuda, utafiti ulijikita kwenye kipindi kati ya 2019-2021. Lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Rwanda. Utafiti ulijikita kwenye kipindi kati ya 2019- 2021 kwa sababu miaka mitano ilipita wakati nchi ya Rwanda ilipoanza kukutumia MUU na ni wakati mwafaka wa kufanya tathmini ya mtaala huu.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti ulioibua tasnifu hii ulikabiliwa na vikwazo mbalimbali kama ifuatavyo: mosi, kupata baadhi ya nyaraka zinazohitajika kutoka taasisi mbalimbali ilikuwa changamoto kwa mtafiti. Ili kukabiliana na changamoto hii, mtafiti aliomba idhini ambayo ilimwezesha kupata nyaraka zote zilizohitajika. Pili, baadhi ya watoa taarifa muhimu kama vile walimu na wakuu wa masomo walijaribu kutoa taarifa zisizo za kweli ili shule zao zionekane vizuri. Ili kukabiliana na hali kama hiyo, watoa taarifa wengi waliulizwa ili kupata taarifa kwa ujumla. Mwisho, Kutokana na kwamba shule zinazofundisha fasihi ya Kiswahili ni chache nchini Rwanda, haikuwa rahisi kwa mtafiti kupata taarifa wakati wa ukusanyaji data. Ili kukabiliana na changamoto hii, mtafiti aliziorodhesha shule zote zinazofundisha fasihi ya Kiswahili wilayani Kicukiro kabla ya kuanza ukusanyaji data za kitaamuli.

### 1.9 Mpangilio wa Ripoti ya Utafiti

Tasnifu ina sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa jumla. Sura ya pili ni mapitio ya maandiko. Sura ya tatu inahusu methodolojia ya utafiti. Sura ya nne inahusu uwasilishaji wa data, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti, na sura ya tano ni muhtasari wa matokeo ya utafi, hitimisho pamoja na mapendekezo.

### 1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii ya kwanza ya tasnifu hii inahusu utangulizi wa jumla. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbalimbali ambazo ni utangulizi, usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na mpangilio wa utafiti. Kwa jumla, sura hii inaeleza taarifa zote tangulizi kuhusu utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mapitio ya maandiko.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko. Mapitio ya maandiko ni jambo muhimu katika kazi yoyote ya utafiti. Maandiko hayo yamegawanyika katika makundi yafuatayo: dhana ya tafakuri bunifu, tafakuri bunifu na lugha, tafakuri bunifu na MUU, tafakuri bunifu na stadi za karne ya ishirini na moja, tafakuri bunifu na utatuzi wa matatizo, mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi, mbinu za ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu na nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa tafakuri bunifu. Vipengele vingine katika sura hii ni mapengo ya utafiti na kiunzi cha nadharia.

## 2.2 Dhana ya Tafakuri Bunifu

Tafakuri bunifu inafasiliwa na wataalamu tofauti. Wataalam hao ni kama vile, Ford & Gioia (2000), Kaufman (2010) na Kim (2011). Fasili za watafiti hawa zinafasili tafakuri bunifu kama ujuzi na uwezo wa uvumbuzi na utatuzi wa matatizo kwa kutumia mbinu mpya. Aidha, Sotco & Mwandanji (2015) wanaifasili tafakuri bunifu kama uwezo wa kuzalisha fikra za kimsingi, mpya, na zinazofaa katika utatuzi wa matatizo yanayoikumba jamii ya watu.

Katika utafiti uliofanyika, tafakuri bunifu ilichukuliwa kama uwezo wa hali ya juu wa mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kupata uamuzi kwa matatizo ya kimaisha kwa namna mpya. Kwa maneno mengine, stadi ya tafakuri bunifu inamsaidia mwanafunzi kuunda hoja mpya zinazomsaidia kutatua matatizo yanayomkabili na yanayoikabili jamii yake.

## 2.3 Tafakuri Bunifu na MUU

Tafakuri bunifu ni stadi muhimu katika maisha ya binadamu. Stadi hii inamsaidia mtu kutatua matatizo ya kimaisha ya kila siku anayokutana nayo.

Jones (2012) anaeleza kwamba elimu inaweza kushiriki katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

Kwa maneno mengine, wanafunzi wanaweza kufundishwa masomo yanayowachochea kufikiri kwa kina ili wakuze ubunifu wao. Hii pia inahusiana na lengo kubwa la kuanzisha MUU ambalo ni ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

MUU ni mtaala unaomshirikisha mwanafunzi katika kazi zote za ufundishaji na ujifunzaji. Mtaala huu unapendekeza kwamba malengo ya ujifunzaji na ufundishaji ni kumpa mwanafunzi uwezo, maadili na stadi ambazo zitamwezesha kufaulu katika maisha kupitia ubunifu wake (Jones, 2012). MUU ulichaguliwa na nchi kadhaa duniani ili kuandaa wazalendo ambao wataanzisha miradi ambayo inalenga kuwaajiri wananchi wengi na kutatua tatizo la ukosefu wa ajira. Katika MUU, nguzo muhimu ni tafakuri ambayo hulenga kuimarisha stadi ya utatuzi wa matatizo, ubunifu, ugunduzi, utafiti, mawasiliano, ushirikiano na ujifunzaji wa muda mrefu.

Hivyo basi, stadi ya tafakuri bunifu inachukuliwa kama kiini cha utekelezaji wa stadi hizi kwa sababu kila stadi huhitaji ubunifu katika utekelezaji wake. Kutokana na haya, tunaweza kusema kwamba stadi ya tafakuri bunifu ni kiini cha utekelezaji wa MUU kwa sababu msingi wake unahusika na kukuza ubunifu wa mwanafunzi. Hivyo basi, ili MUU utekelezwe vilivyo, ni lazima stadi ya tafakuri bunifu itiliwe mkazo kwa sababu MUU unahusika kwa kiwango kikubwa na ubunifu wa mwanafunzi.

**2.4 Tafakuri Bunifu na Lugha**

Lugha na tafakuri bunifu ni mambo mawili yanayotegemeana. Tafakuri bunifu husaidia wanafunzi kumudu stadi za lugha (Abler, 2013). Ufundishaji wa lugha ni lazima usisitize uwezo na ujuzi wa lugha unaoendana na

matumizi yake. Hii inamaanisha kwamba kufundisha wanafunzi lugha si kuwafundisha wanafunzi kuhusu lugha bali ni kuwafundisha kuitumia lugha katika miktadha tofauti ya mawasiliano.

Lugha pia huonekana kama rasilimali ambayo hutoa fursa inayochangia katika kuchochea ukuaji wa kiakili wa wanafunzi kupitia uhimizaji wa kufahamu na kuelewa ulimwengu unaowazunguka (Frank, 2000). Kwa maneno mengine, lugha inawasaidia wanafunzi kukuza fikra zao kwa kuelewa nini kinatendeka katika jamii yao na namna gani wanavyoweza kukabiliana na matatizo yanayoizunguka.

Hivyo basi, ili wanafunzi waweze kuimudu lugha ilivyo ni lazima wasaidiwe kukuza ubunifu wao kupitia ufundishaji wa lugha lengwa. Hivyo basi, ufundishaji wa lugha yeyote unapaswa kutilia mkazo kwenye ukuzaji wa ubunifu wa wanafunzi kwa namna ya uundaji hoja wanazoweza kutumia kimawasiliano.

Tunapozungumza lugha moja tunakubali kwamba maneno yanawakilisha mawazo ya watu, maeneo na matukio tofauti. Lugha iliyoteuliwa ambayo wanajamii hujifunza inaunganishwa na utamaduni na hata mazingira yao. Lakini je, kuna uhusiano wowote kati ya lugha na jinsi tunavyofikiria jambo ili kutatua matatizo? Kwa muda mrefu wanasaikolojia wamechunguza ikiwa lugha inaweza kushiriki katika kuathiri namna tunavyofikiri, mawazo na imani ya binadamu. Brundrett (2017) anasema kwamba ujifunzaji lugha unaosisitiza ukuzaji wa stadi zake ambazo ni kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika hushiriki katika kukuza ubunifu wa mwanafunzi pia. Hivyo basi, ni lazima walimu wa lugha wawawezeshe wanafunzi kukuza stadi zao zinazochangia katika kuendeleza stadi zao za ubunifu wakati wa matumizi yake katika miktadha tofauti ya mawasiliano.

Maelezo ya watalamu hawa yanaonesha kwamba stadi ya tafakuri bunifu inaweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi kama sanaa inayotumia lugha kuonesha yaliyomo katika jamii.

Licha ya umuhimu wa tafiti hizi wa kutoa taarifa zinazohitajika atika uwanja wa ufundishaji lugha , kuna mapungufu kadhaa yanayojitokeza. Kwanza, mtu anaweza kujiuliza ni mbinu ipi ya ufundishaji inayoweza kutumiwa? Pili, utafiti wake ulihusu wanafunzi wa kiwango gani cha elimu? Ni katika mazingira yapi ya ufundishaji haya yaweza kutendeka? Hivyo basi, utafiti huu ulikuja kuziba mapengo haya kwa kuonesha jinsi ufundishaji wa fasihi katika Kiswahili unavyoweza kutumiwa ili kuimarisha stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda katika mazingira ya MUU.

**2.5 Tafakuri Bunifu dhidi ya Tafakuri Tunduizi**

Stadi za tafakuri bunifu na tafakuri tunduizi huhusiana na hutofautiana. Tafakuri tunduizi ni busara na fikra za kutafakari ambazo zinalenga kuamua nini cha kuamini au kufanya. Kwa upande mwingine, tafakuri bunifu huelezwa kama uwezo wa kulinganisha na kulinganua athari za kila uamuzi unaoweza kuchukuliwa. Tafakuri bunifu inahusu kwenda zaidi ya fikra za awali na kuzalisha fikra nyingine mpya. Tafakuri tunduizi kwa upande mwingine ni tathmini zaidi katika michakato ya kiasili na kutambua jambo fulani.

Tafakuri bunifu na tafakuri tunduizi ni stadi muhimu sana katika elimu. Heinig (2003) anaeleza kwamba tafakuri bunifu na tafakuri tunduizi ni muhimu sana katika kumtayarisha mhitimu wa elimu ambaye atakidhi mahitaji ya waajiri kwenye soko la ajira kwa sababu stadi hizi mbili zinawahimiza wanafunzi kushiriki katika ujifunzaji na kuwawezesha kufikiri

kwa kiwango cha juu katika ugunduzi na utatuzi wa tatizo. Tafakuri bunifu na tafakuri tunduizi huwawezesha wanafunzi kutumia mantiki na mawazo ili kutafakari jinsi ya kukabiliana na maswala na changamoto tofauti za kimaisha (Kelly, 2016).

Kwa maneno mengine, stadi hizi mbili zinatoa mchango katika mafanikio ya elimu ya karne ya ishirini na moja kwa sababu zinahusu namna bora ya kupata uamuzi wa kukabiliana na changamoto tofauti zilizomo katika jamii ambalo ndilo lengo la msingi la elimu.

Utekelezaji wa stadi ya tafakuri tunduizi hutegemea stadi ya tafakuri bunifu kwa kiwango kikubwa. Tafakuri tunduizi ni stadi ambayo haiwezi kuwepo bila stadi ya tafakuri bunifu kwa sababu stadi ya tafakuri tunduizi inayohusika na tathmini ya hoja zinazohusiana na utatuzi wa tatizo inakuwepo baada ya hoja hizo kubuniwa. Kwa maneno mengine, stadi ya tafakuri tunduizi inategemea kwa kiwango kikubwa stadi ya tafakuri bunifu; stadi ya tafakuri bunifu isipokuwepo; stadi ya tafakuri tunduizi haiwezi kuwapo. Kwa hiyo, stadi ya tafakuri bunifu ndiyo inatoa kazi kwa tafakuri tunduizi. Hivyo basi, ili kumwandaa mwanafunzi sahihi wa karne ya ishirini na moja, ni lazima stadi ya tafakuri bunifu iwe stadi ya msingi katika ufundishaji.

### 2.6 Tafakuri Bunifu na Utatuzi wa Matatizo

Tatizo hufafanuliwa kama hali ambayo inahitaji uchunguzi, kujifunza, kufikiri, kuchambua na kutatua. Utatuzi wa matatizo hufafanuliwa kama uwezo na ujuzi katika nyanja tofauti unaowezesha mtu kutatua matatizo anayokumbana nayo (Eskin, 2009). Kwa maneno mengine, utatuzi wa matatizo unahusiana na ugunduzi na uundaji wa hoja zifaazo kuhusu utatuzi wa tatizo husika.

Mertoğlu na Öztuna (2004) wanaeleza kwamba maarifa yanafaa kuandamana na ubunifu ili kutatua matatizo yanayokabili maisha ya binadamu. Tafakuri bunifu ni muhimu sana katika utatuzi wa matatizo ya mwanafunzi hasahasa katika enzi za sasa ambapo mhitimu wa elimu hulazimika kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Maelezo haya yanaonesha wazi kwamba utatuzi wa matatizo tofauti yaliyojitokeza kutokana na teknolojia, sayansi na utandawazi katika karne ya ishirini na moja unahitaji sana stadi ya tafakuri bunifu. Hata hivyo, hayaelezi jinsi stadi hii inavyoweza kukuzwa miongoni mwa wanafunzi.

Katika elimu ya karne ya ishirini na moja inayosisitiza utatuzi wa matatizo yanayoikabili jamii, ni vema stadi ya tafakuri bunifu iwe ya msingi kwa sababu inachangia katika ubunifu na ugunduzi wa hoja faafu zinazohitajika katika utatuzi wa matatizo hayo. Kwa hiyo, nimuhimu stadi ya tafakuri bunifu itiliwe mkazo ili kumwandaa mwanafunzi mwenye uwezo wa kutatua matatizo yake na ya jamii yake kwa ujumla. Hivyo basi, utafiti huu unatoa mwanga kwa namna stadi hii muhimu inavyoweza kukuzwa miongoni mwa mwanafunzi kwa kutoa mwongozo wa ufundishaji kwa walimu wa fasihi katika shule za sekondari.

## 2.7 Mwongozo wa Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi

Ni ukweli usiopingika kwamba walimu wana jukumu muhimu katika kuendeleza maarifa, stadi, uwezo na maadili yanayofaa kwa wanafunzi. Pia, wanafunzi wanalazimika kujifunza na kumudu mikakati ya kutambua matatizo, kufanya uamuzi unaofaa na kutatua matatizo yanayokabili jamii wanamoishi. Kwa kuwa mwalimu na wanafunzi huwa na majukumu mahususi katika mchakato wa kielimu, stadi za tafakuri bunifu huwa zinahitajika ili kuwawezesha walimu na wanafunzi kutimiza majukumu yao

(Nagamurali, 2013). Stadi za tafakuri bunifu hufundishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali.. Nagamurali (Khj) anaeleza mbinu za kufundishia stadi za tafakuri bunifu ambazo ni utumiaji wa taswira akilini, drama bunifu, mkakati wa Torance na Safter, sitiari, ulinganifu na ushindani. Mbinu hizi zilichaguliwa katika utafiti wetu kwa sababu tuliona zinaweza kufaa sana katika ukuzaji wa tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi. Mbinu hizi kwanza zinafafanuliwa jinsi zinavyoweza kutumiwa ili kukuza ubunifu miongoni mwa wanafunzi. Pili, zinaonekana kutoa mapendekezo ya kusaidia wanafunzi kuhamisha ubunifu wanaopata shuleni na kuutumia katika maisha halisi. Katika sehemu hii, tunazifafanua mbinu hizi moja baada ya nyingine huku tukizihusisha na sekta ya elimu hususani ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.7.1 Utumizi wa Taswira

Mbinu hii inahusu kuleta mawazo katika dunia halisi. Taswira inahusiana na mawazo ya kiakili. Taswira ni muhimu sana katika kujenga picha za vitu fulani akilini. Picha hizo huwa ni za vitu ambavyo haviwezi kuonekana papohapo. Nagamurali (Khj) anatoa mfano akisema ya kwamba mwalimu anapowaambia wanafunzi: "Chumba cha malazi;" wanafunzi wataanza kuunda picha za vyumba vyao vya malazi akilini ingawaje hawapo kwenye vyumba hivyo wakati huo., taswira huwafanya binadamu wajenge picha akilini ambazo hujaa hisia tofauti za upendo, usalama na hata maumivu. Mara nyingine, taswira huleta picha zinazoambatana na hisia zinazolingana na picha hizo. Mchanganyiko huu wa picha na hisia ndio ambao huifanya taswira iwe mbinu bora katika ufundishaji na ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

Ili kufanikisha ufanisi wa utumiaji wa taswira, mwalimu anapaswa kuwa na kazi iliyoandikwa au ya akili kuhusu picha anazotarajia kuunda akilini mwa

wanafunzi. Wakati ambapo mwalimu anafundisha wanafunzi na kuwaongoza kupitia maudhui ya kozi, mwalimu huweza kuomba wanafunzi kufunga macho yao na kufikiri kuhusu picha fulani kutegemeana na funzo aliloandaa. Baada ya muda fulani, mwalimu huwapa wanafunzi nafasi ya kutoa maelezo na mapendekezo kuhusu picha walizounda akilini. Kwa kufanya zoezi kama hili, wanafunzi watapanua uwezo wao wa kufikiri na kuzalisha mbinu mpya za kukabiliana na changamoto tofauti.

Utumiaji wa taswira kwa upande mwingine, huwawezesha wanafunzi kutabiri vitu ambavyo havijawahi kuwapo duniani. Hii hutokea wakati ambapo mwanafunzi huchora picha akilini inayomwezesha kuzalisha kazi mpya ya sanaa au ya kisayansi ambayo haijawahi kutungwa na mtu yeyote. Kazi hiyo huweza kuwa ni shairi, riwaya, tamthilia, sanamu na nyinginezo. Isitoshe, Bagley (1987) anadhihirisha kwamba taswira ni mbinu muhimu sana katika utatuzi wa matatizo.

Maelezo yanayotolewa hapo juu, yanaonesha kwamba taswira inaweza kutumiwa na walimu katika kusisitiza maudhui ya kozi zilizosomwa awali kwa kutumia mikakati ambayo itawawezesha wanafunzi kuunda picha akilini. Picha hizo huwakumbusha taswira za maudhui ya kozi na maarifa kwa ufasaha. Katika utafiti huu, tulichunguza namna ambavyo walimu hasa wa fasihi huweza kutumia mbinu ya taswira katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

### 2.7.2 Utumizi wa Drama Bunifu

Kwa mujibu wa Dahl (1961) kichwa hakiwezi kusikia chochote mpaka moyo usikie. Anaongeza kwamba kile ambacho moyo unakijua leo, kichwa kitakielewa kesho. Utambuzi wa uwezo wa juu wa mtu binafsi unawezekana kupitia mbinu zinazoshirikisha akili na shughuli za kimwili. Katika muktadha

huo, Magret (1960) anadhihirisha mbinu ya drama bunifu kama mbinu ya ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu inayotumiwa katika kuamsha moyo na kichwa cha mwanafunzi.

Kupitia mchezo wa drama bunifu, mtu hupata uzoefu wa miktadha mbalimbali kwa kuzingatia majukumu anayopewa katika mchezo wa kuigiza. Uzoefu huo, kwanza, hutoa njia ya kujenga hisia. Pili, hukuza uwezo wa kukumbuka na kuhifadhi yaliyosomwa. Tatu, huendeleza hamu ya binadamu kuhusu uzuri na maajabu ya ulimwengu unaomzunguka na kumwezesha binadamu kujihusisha mwenyewe na ulimwengu kwa kutumia mbinu za kipekee.

Zaidi ya hayo, kupitia drama bunifu, wanafunzi hunufaika kuchunguza miili na akili yao katika kazi za sanaa tendaji. Mazoezi ya drama bunifu huwa na thamani katika ukuzaji wa ubunifu wa wanafunzi. Kama ilivyoelezwa na Nagamurali (Khj), michezo ya drama bunifu hukuza ukolezi, hisia, ufahamu, utawala binafsi na uchochezi.

Hii inamaanisha kwamba kupitia drama bunifu, mwanafunzi hubadilika na kuwa mwenye akili ya hali ya juu na ambaye ana uwezo wa kukubali na kukabiliana na hali yoyote ile. Mchango wa drama bunifu katika ukuzaji wa ubunifu wa binadamu umetuchochea kufanya utafiti huu ili kupata taarifa za kutosha zinazohusiana na namna ambavyo drama bunifu hutumiwa na huweza kutumiwa katika uimarishaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia ufundishaji wa fasihi.

### 2.7.3 Utumizi wa Sitiari na Analojia

Utumiaji wa sitiari na analojia ni mbinu muhimu sana katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Faida kubwa ya mbinu hii ni kurahisisha ufundishaji kwa kuwa haihitaji uwezo wa kiuchumi wa hali ya juu. Matumizi ya mbinu

hii pia huchukuliwa kama utaratibu wa ukuzaji wa ubunifu kwa sababu sitiari na analojia huwawezesha wanafunzi kuzalisha fikra chungu nzima. Mbinu ya utumiaji wa sitiari na analojia husisitizia fikra, aina na uzito wa fikra zinazotolewa (Nagamurali, Khj). Katika ufikiriaji katika muktadha wa sitiari na analojia, fikra moja inaweza kutumiwa katika muktadha mwingine kwa kuzingatia usambamba na uwiano. Analojia pia huweza kushiriki katika ukuzaji wa stadi za utatuzi wa matatizo na ugunduzi wa kisayansi.

Katika kufanikisha utumiaji wa mbinu hii katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu, walimu wanahitajika kuwapa wanafunzi mazoezi yatakayowalazimisha kufuata mbinu zilizotumiwa katika utatuzi wa tatizo fulani na kuzirekebisha ili ziweze kutumiwa katika kutatua tatizo jingine wanalokabiliana nalo.

### 2.7.4 Ushirikishaji wa Kina wa Wanafunzi katika Sanaa

Ushirikishaji wa kina wa wanafunzi katika sanaa ni namna nyingine inayoweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi ili kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Sanaa huelezwa kama ufundi wa kuibua mawazo yanayokuwa katika fikra na kuyaonesha kwa njia mbalimbali kama vile uchoraji, uchongaji, ufinyanzi, fasihi na kadhalika. Kazi za sanaa zinakuza ubunifu wa wanafunzi hasahasa katika madarasa mengi ya utotoni (Robert, 2010).

Sanaa ina nafasi kubwa katika maendeleo ya ufundishaji wa ubunifu kwa kuwa sanaa hukuza maendeleo ya uwezo wa utambuzi wa watoto. Kuchunguza na kushirikisha watoto katika kazi za sanaa tofauti huwapa wanafunzi uwezo wa kujitegemea katika kuzalisha masuluhisho mapya ya kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo. Licha ya mtaalamu huyu kuonesha umuhimu wa sanaa katika ukuzaji wa ubunifu, bado haoneshi ni

kiwango kipi cha elimu ambacho mbinu hii inaweza kutumiwa. Aidha, mtaalamu huyu haoneshi ni mwongozo upi unaoweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili ili waweze kukuza stadi ya tafakuri bunifu.

Kwa hivyo sasa, utafiti huu ulikusudia kuonesha jinsi ushirikishaji wa kina wa wanafunzi katika sanaa unavyoweza kutumiwa kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi na mwongozo unaoweza kufuatwa na walimu wa Kiswahili katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia ushirikishaji wa kina wa wanafunzi katika sanaa.

## 2.8 Elementi za Tafakuri Bunifu katika Muktadha wa Elimu

Tafakuri bunifu huwa na elementi tofauti ambazo ni udadisi, ufyonzaji, tafakari na msukumo (Appleton, 2015). Katika sehemu hii tunazieleza elementi hizi moja baada ya nyingine. Elementi hizi zinaelezwa kwa kuzihusisha na sekta ya elimu hususani ufundishaji na ujifunzaji:

### 2.8.1 Udadisi

Elementi hii inahusu utashi wa hali ya juu unaommotisha mtu na kumraghibisha kutaka kujifunza na kujua kitu fulani. Hii ni mbinu ya msingi katika ukuzaji wa tafakuri bunifu. Katika uwanja wa elimu, inaaminika kwamba mtu amejaliwa tabia tofauti alizozitoa katika jamii ambazo zinaweza kutumiwa kama chanzo cha kuzalisha udadisi unaohitajika sana katika kujifunza na kujua mengi kuliko yale ambayo anajua.

Kumshirikisha mwanafunzi katika kila kazi za elimu husaidia katika kukuza udadisi miongoni mwa wanafunzi (Brundrett, Khj). MUU unasisitizia sana kumshirikisha mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji ili kukuza ubunifu wa wanafunzi. Kwa hiyo, waelimishaji wanalazimika kuwamotisha wanafunzi ili kukuza udadisi miongoni mwao.

Maelezo haya yanaonesha wazi kuwa mbinu ya udadisi ndiyo ambayo huzalisha hiari na utashi wa kutaka kujua mengi miongoni mwa wanafunzi. Tamaa hii ya kutaka kujua mengi hufanikisha ukuzaji wa ubunifu wa mwanadamu. Kwa hiyo, elementi hii itawasaidia wanafunzi kutamani kujifunza, kujua na kutekeleza mengi wanayoyahitaji katika kukabiliana na changamoto za kijamii. Swala hili ni miongoni mwa maswala ambayo utafiti wetu uliyashughulikia kwa sababu tulitaka kuonesha jinsi wanafunzi wanavyoweza kusaidia kukuza elementi za stadi ya tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi kama sanaa ya lugha inayoeleza yaliyomo katika jamii na jinsi ya kuyatatua.

### 2.8.2 Ufyonzaji

Ufyonzaji ni elementi ya tafakuri bunifu ambayo inahusu namna ambavyo mtu hufyonza maarifa, stadi na maadili kutoka katika anayoyaona au anayoyasikia.

Katika elimu, udadisi wa wanafunzi wa kutaka kujua, huwawezesha kufyonza maarifa, stadi na maadili. Appleton (Khj) anasema kwamba ufyonzaji hujaza fikra nyingi mpya na kuzihifadhi kichwani. Akiba hiyo ya fikra mpya, ndiyo hukuza namna ya kufikiri na kuibua ubunifu wa hali ya juu miongoni mwa wanafunzi tangu wakiwa na umri mdogo.

Ufyonzaji huweza kukuzwa na mambo mbalimbali. MUU unaweza kufanikisha ufundishaji wa tafakuri bunifu. Kwa mfano, walimu wa lugha wanaweza kutumia usomaji vitabu, muziki, sinema na drama katika kukuza elementi ya ufyonzaji. Vitabu, na drama hutushawishi kutafakari ili kung’amua ni yepi ya kufyonzwa au kutofyonzwa kutegemeana na raghba inayotumotisha (Kaila, 2005). Hivyo basi, utafiti huu ulionesha jinsi

ufyonzaji unavyoweza kukuzwa miongoni mwa wanafunzi kupitia ufundishaji wa fasihi katika mazingira ya utekelezaji wa MUU.

### 2.8.3 Tafakari

Tafakari hueleweka kama utaratibu wa kugundua mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji ambazo huwezesha kuhusisha uwezo wa awali na uwezo unaofikiwa baada ya ufundishaji na ujifunzaji. Ndiyo sababu Appleton (Khj) anasisitiza kwamba tafakari huhakikisha kuwa wanafunzi wamefikia uwezo uliokusudiwa.

Ikumbukwe kwamba, tafakari hukuzwa na kuhakikisha ya kwamba wanafunzi wote wanajifunza kwa ufanisi zaidi ili kukidhi mahitaji yao na kuwawezesha kufanikiwa katika soko la ajira. Bila shaka, kama tunataka kuwapa wanafunzi elementi ya tafakari, ni lazima tuwafundishe kwa kufuata pendekezo la MUU linalosisitizia uwezo, maarifa, stadi na mwenendo mwema. Utafiti wetu ulikusudia kuonesha pia jinsi stadi hii ya tafakuri bunifu inavyoweza kukuzwa katika darasa la fasihi kwa wanafunzi wa lugha nchini Rwanda.

### 2.8.4 Msukumo

Msukumo ni elementi ya mwisho ya tafakuri bunifu ambayo ni mchakato wa uchochezi wa kiakili ambao humraghbisha mtu kufanya au kufikiria na kutekeleza jambo ambalo hasahasa ni la ubunifu. Elementi hii ina athari kubwa juu ya uwezo wa kuzalisha fikra muhimu za kiubunifu ambazo huchangia katika uboreshaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

Msukumo ni muhimu sana katika elimu. Watu ambao wana msukumo huwa ni wadadisi na wenye nia ya kutaka kujua mengi. Huwa na hisia ya maajabu na furaha katika kujifunza. Wenye msukumo huonesha nia ya kufikiri kwa namna ya kipekee na hustarehe wakati wanapojishughulisha na ujifunzaji.

Appleton (Khj) anaeleza kwamba msukumo huwafanya wanafunzi wawe wafikiriaji bunifu wanaotafakari juu ya mawazo na vikwazo vinavyoikumba jamii.

Msukumo hukuzwa kwa kuwapa wanafunzi kazi zinazochochea uwezo wao wa kufikiri. Katika muktadha wa MUU kwa ufundishaji wa lugha, kazi ambazo zinaweza kukuza msukumo ni kama vile mijadala, midahalo, utungaji wa insha na uchambuzi wa kazi za fasihi mbalimbali. Hivyo basi, kwenye utafiti wetu tulikusudia kuonesha jinsi elementi ya msukumo inavyoweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi. Vilevile, tulikusudia kuunda mwongozo wa namna stadi hizi za tafakuri tunduizi zinavyoweza kuimarishwa kupitia ufundishaji wa fasihi kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda.

**2.9 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu**

Fasihi ni kazi ya sanaa imulikayo hisia, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia maneno yaani lugha (Wamitila, 2003). Fasihi huonekana kama rasilimali ambayo hutoa fursa za lugha kwa kutoa mafunzo muhimu ya lugha. Mafunzo hayo huchangia katika kuchochea ukuaji wa kiakili wa wanafunzi kupitia uhimizaji wa kufahamu na kuelewa ulimwengu unaowazunguka.

Ufundishaji wa fasihi na ukuzaji wa tafakuri bunifu ni jambo ambalo limeongelewa na watafiti tofauti kama vile Heinig (1992), Frank (2000), Srinivasan (2007) na Kharkhurin (2010).Watafiti hawa wote wanakubaliana kwamba ufundishaji wa fasihi una nafasi kubwa katika ukuzaji wa tafakuri bunifu.

Kupitia fasihi, wanafunzi hufahamishwa historia ya fasihi, mila, urithi, asili ya ushawishi na uhusiano kati ya mwandishi na muktadha. Kwa kutaka kujua mengi kuhusu historia ya jamii wanamoishi, wanakuza ubunifu wao. Zaidi ya

hayo, uhakiki wa kazi za kifasihi unawafanya wanafunzi wakuze uwezo wao wa kufikiri. Uwezo huu unawawezesha kuzalisha fikra mpya za kukabiliana na changamoto zilizomo maishani mwao.

Tafiti hizi ni muhimu sana kwa kuwa zinaonesha jinsi fasihi inavyochangia katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu. Licha ya uzuri wake, tafiti hizi zina mapungufu mbalimbali. Mosi, tafiti hizi hazioneshi ni katika kiwango gani cha elimu fasihi inaweza kutumiwa kukuza stadi ya tafakuri bunifu. Pili, tafiti hizi hazitoi mwongozo wowote unaoweza kutumiwa na mwalimu wa fasihi ili aweze kukuza ubunifu wa wanafunzi kwa kiwango kadhaa. Tatu, hakuna tafiti miongoni mwa hizi inayozungumzia mazingira ya Kiafrika. Mwisho, tafiti hizi ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza; hali inayoashiria kuwa, zinazungumzia fasihi ya Kiingereza. Haya ni mapengo yaliyopaswa kuzibwa na utafiti wetu. Hivyo basi, utafiti wetu ulijikita sio tu kuonesha jinsi fasihi ya Kiswahili inavyoweza kuchangia katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa lugha, bali pia kufanya jaribio la kuunda mwongozo unaoweza kutumiwa na walimu wa Kiswahili katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

## 2.10 Mapengo ya Utafiti

Maandiko mbalimbali yaliyopitiwa yanaonesha kwamba ufundishaji wa fasihi unaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa ukuzaji wa tafakuri bunifu. Tafiti hizi zilijikita kuzungumzia maswala tofauti kuhusu stadi ya tafakuri bunifu na fasihi (Kiany, Mahdavy & Ghafar, 2011; Jack, 2013; Sotco na Mwandanji, 2015; Karpovu, 2017; Wongnaa & Baachie, 2018; Likisa, 2018 na Brisen 2019). Licha ya kuonesha maswala tofauti kuhusu fasihi na tafakuri bunifu, tafiti hizi zilionesha baadhi ya mapengo yanayopaswa kuzibwa na utafiti wetu. Baadhi ya mapengo hayo ni yafuatayo: Mosi, tafiti za watalamu

hawa hazioneshi kiwango cha elimu ambapo fasihi inaweza kutumiwa katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu. Pili, tafiti hizi hazitoi mbinu mwafaka ya ufundishaji inayoweza kutumiwa kwa kiwango fulani katika mchakato huu. Tatu, kazi hizi hazitoi mwongozo uanaoweza kutumiwa na walimu hasa wa Kiswahili. Mwisho, ni kuwa tafiti hizi zilizungumzia nchi zilizoendelea na kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hivyo basi, utafiti huu ulikusudiwa kuziba mapengo hayakwa kuonesha jinsi ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili unavyoweza kutumiwa ili kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa lugha katika shule za sekondari katika mazingira ya utekelezaji wa MUU nchini Rwanda.

## 2.11 Kiunzi cha Dhana ya Nadharia

Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Utambuzi katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Nadharia hii ilianzishwa na mwanasaikolojia wa Uswisi Piaget (1983). Mtaalamu huyu alianzisha nadharia hii kwa lengo la kugundua namna ambavyo tafakuri bunifu hukua. Mtaalamu huyu anasema kwamba binadamu ana tabia na uwezo unaomwezesha kuitikia na kuiga matendo na maitikio mengine ya wanaomzunguka ili kukabiliana na mazingira anamoishi. Anaendelea kusema kwamba tofauti na wanyama na ndege, wanadamu wana uwezo wa kubadilisha mbinu za kukabiliana na kuunda mbinu nyingine mpya.

Mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kwamba ubunifu si nakala ya ukweli, lakini ni zao la mwingiliano wa mtu na mazingira anamoishi.Hii inamaanisha kwamba jambo linaloonyesha kuwa ubunifu si uwezo wa kutenda mambo na kutaatua matatizo kwa kuiga mbinu zilizotumiwa na wengine bali, ubunifu ni uwezo wa kuzalisha mbinu mpya ambazo hazikutumiwa na mtu yeyote yule

ili kutatua matatizo kadhaa. Mhimili huu ulitusaidia katika utafiti wetu kwa kuonesha jinsi fasihi inayohusika na binadamu na maisha yake inavyoweza kukuza ubunifu wa mwanafunzi kutokana na mwingiliano wake na jamii yake.

Mhimili wa pili unasema kwamba unapomfundisha mtoto kitu bila kumshirikisha katika ujifunzaji, unamnyima milele nafasi yake ya kugundua mwenyewe. Mhimili huu ulitusaidia siyi tu katika uungaji wa mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bali pia katika ubainishaji wa namna fasihi inavyokuza stadi ya tafakuri bunifu kutokana na jinsi mwalimu anavyowashirikisha wanafunzi katika mjadala na midahalo na kazi nyingine za kifasihi zinazowasaidia kubuni hoja faafu kutokana na kile wanachotaka kujibu. Hii pia inaendana na lengo la MUU ambalo ni kuwashirikisha wanafunzi na kuwakuzia uwezo wa utambuzi, ubunifu na ugunduzi. Mhimili huu bunifu kupitia fasihi.

Mhimili wa mwisho unasema kwamba, utatuzi wa matatizo unategemea utambuzi, ubunifu wa binadamu na ugunduzi wa kisayansi. Mhimili huu ulitusaidia kuonesha jinsi utatuzi wa tatizo unavyotegemea sana stadi ya tafakuri bunifu kwa kuwa ili tatizo litatuliwe, ni lazima kuundwe hoja fulani zinazohusiana na tatizo lililopo.

Kwa jumla, mihimili ya nadharia hii inaonesha kwamba stadi ya tafakuri bunifu inapaswa kuwa kiini katika elimu inayotolewa kwenye karne ya ishirini na moja.

## 2.12 Muhtasari wa Sura ya Pili

Katika sura ya pili tulizungumzia mapitio ya maandiko pamoja na kiunzi cha nadharia ya utafiti. Maandiko yaliyopitiwa kuhusu fasihi na stadi ya tafakuri bunifu yalitoa taarifa za kutosha kuhusu uhusiano uliopo kati ya ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi na ufundishaji wa fasihi. Licha ya hayo, tulionesha mapengo ya utafiti yaliyopaswa kuzibwa na utafiti huu. Vilevile, sura hii imefafanuanadharia ya utambuzi ambayo itaongoza utafiti huu.

# SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu methodolojia ya utafiti. Methodolojia ya utafiti inaelezwa na Kothari (2008) kama sharia na mwongozo ambao humuonesha mtafiti hatua za kufuatwa ili kukamilisha utafiti anaokusudia kufanya. Vipengele vinavyofafanuliwa katika sehemu hii ni paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, aina ya data zilizokusanywa, njia za kukusanyia data, vifaa vya utafiti, uchanganuzii wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.2 Paradima ya Utafiti

Neuman (2009) anasema kwamba paradima ya utafiti ni sehemu muhimu inayohusu vigezo, matatizo yanayoweza kukabili utafiti, mbinu na zana zitakazotumiwa na mtafiti ili kujibu maswali ya utafiti. Wakati wa kufanya utafiti, mtafiti alijenga uhusiano wa karibu na washiriki wa utafiti. Ili uhusiano huu ufikiwe, mtafiti aliheshimu na kuthamini kila jibu na hoja iliyotolewa na washiriki wa utafiti ambao ni walimu, viongozi wa shule na wanafunzi katika shule zilizochaguliwa. Kadhalika, mtafiti alitumia mbinu zinazofaa ili kukabiliana na changamoto ambazo zingejitokeza wakati wa kufanya utafiti. Mbinu hizi zilimwezesha mtafiti kutimiza malengo ya utafiti.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni kipengele muhimu katika kudhihirisha kielelezo kamili cha jinsi utafiti utakavyofanyika tangu mwanzo mpaka mwisho. Kothari (Khj) anadhihirisha kuwa usanifu wa utafiti ni kama ramani ambayo huonesha picha kamili ya jinsi utafiti ulivyofanyika kuanzia kwenye hatua ya ukusanyaji data hadi kwenye uchanganuzi wake. Utafiti wetu ulikuwa wa

kitaamuli. Hii inamaanisha kwamba data za kitaamuli zilizokusanywa kuhusu ukuzaji wa tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Kicukiro nchini Rwanda, zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia maelezo.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huchukuliwa kama mahali ambapo utafiti utafanyika kwa madhumuni ya kukusanya data za utafiti ambazo zinakusudiwa kujibu maswali ya utafiti (Kothari, Khj). Kwa hiyo, eneo la utafiti katika utafiti huu lilikuwa shule za sekondari wilayani Kicukiro nchini Rwanda zinazofundisha Kiswahili tangu kidato cha nne hadi kidato cha sita. Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu lina watafitiwa wenye taarifa zilizomsaidia mtafiti kujibu maswali ya utafiti.

### 3.5 Wango na Sampuli ya Utafiti

#### 3.5.1 Wango la Utafiti

Wango la utafiti ni jumla ya binadamu au vitu vyote vinavyohitajika kufanyiwa utafiti kadri ya mwelekeo wa utafiti husika (TUKI, 2004). Katika utafiti wetu, wango la utafiti lilikuwa viongozi wa shule na walimu wa Kiswahili katika kidato cha nne, kidato cha tano na kidato cha sita katika shule teule wilayani Kicukiro nchini Rwanda. Wango hili lilichaguliwa kwa kuwa lilikuwa na taarifa zote zilizowezesha mtafiti kujibu maswali ya utafiti.

#### 3.5.2 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti

Robson (2007) anaeleza sampuli kama wawakilishi wanaochaguliwa kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa ili wamsaidie mtafiti kupata data ambazo zitawakilisha kundi lote. Mtafiti hawezi kupata sampuli bila ya kufanyika tendo la usampulishaji. Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua wawakilishi

wa watafitiwa wote ambao wanalengwa katika utafiti uliokusudiwa (Cresswell, 2000).

Utafiti wetu ulitumia mbinu ya usampulishaji lengwa kupata sampuli ya utafiti. Usampulishaji lengwa hufasiliwa kuwa ni aina ya usampulishaji ambapo mtafiti huchagua sampuli yake akiwa na imani kwamba sampuli hiyo itamsaidia kupata data za utafiti anazozihitaji.

Sampuli ya utafiti huu ilikuwa walimu wa Kiswahili 6 na wakuu wa masomo 6 walioteuliwa kutoka shule za sekondari wilayani Kicukiro ambazo ni G.S. Gatenga, G.S. Kicukiro, GS Kimisange, G.S. Remera Protestant na G.S. Gahanga. Wilayani Kicukiro kuna shule nyingi za sekondari lakini shule tano tu ziliteuliwa kutokana na kwamba ndizo ambazo zina mchepuo wa lugha ambamo fasihi ya Kiswahili hufundishwa. Hivyo, shule zilizoteuliwa zilimwezesha mtafiti kupata data zote muhimu.

### 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti ambao uliibua tasnifu hii ulitumia data za msingi pamoja na data za upili.

#### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data za utafiti ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kabla. Furlong (1984) anaeleza kuwa data za msingi huitwa pia data ghafi kwa kuwa ni data ambazo hazijawahi kufanyiwa kazi yoyote. Kwenye utafiti huu, data za msingi tulizikusanya kupitia usaili na ushuhudiaji wa walimu madarasani wakiwa katika ufundishaji. Aidha, tulitumia pia uchanganuzi wa nyaraka mbalimbali za ufundishaji za walimu wanaofundisha fasihi andishi ya Kiswahili kwenye shule zilizoteuliwa.

### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni data ambazo tayari zilikwisha kusanywa na watafiti waliotangulia. Data za upili hukamilisha data za msingi na kuzipa uhalali. Kwa kawaida, data za upili hukusanywa kutoka katika tasnifu, makala, vitabu, magazeti pamoja na makala nyingine zinazopatikana kwenye tovuti na wavuti (Yin, 1994). Hivyo, data za upili katika utafiti huu zilikusanywa katika maktaba na ofisi za shule zilizochaguliwa, pamoja na kutoka katika tovuti.

## 3.7 Njia za Kukusanyia Data

Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data kuhusu namna ambavyo walimu hukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia ufundishaji wa fasihi. Vilevile, mtafiti alikusanya data kutoka matini na nyaraka ambazo zina uhusiano na mada ya utafiti huu. Hivyo basi, mbinu za ushuhudiaji, uchanganuzi wa matini na usaili zilitumiwa katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Ushuhudiaji ulitumiwa ili kuchunguza namna ambavyo walimu hufundisha tafakuri bunifu kupitia lugha. Mbinu ya uchanganuzi matini na usili zilitumiwa ili kuchunguza namna ambavyo walimu hujumuisha tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo na tathmini pamoja na kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi. Mbinu hizi zilikamilishana ili kumwezesha mtafiti kupata taarifa zilizomsaidia katika kutimiza malengo ya utafiti.

### 3.7.1 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji hufasiliwa kama mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti hushuhudia vitendo na matukio mbalimbali ili kupata taarifa zitakazomsaidia kutimiza malengo mahususi ya utafiti wake (Kombo na Tromp, 2006). Mbinu hii ilitumiwa katika utafiti huu kwa kuwa mtafiti alilazimika kwenda katika

shule zilizochaguliwa na kushuhudia walimu wakifundisha madarasani na kurekodi data ili kuchunguza namna ambavyo walimu hujumuisha stadi ya tafakuri bunifu wanapofundisha. Mbinu hii ilisaidia katika kukusanya data zilizotumiwa katika kujibu maswali ya utafiti.

### 3.7.2 Uchanganuzi wa Matini

Uchanganuzi wa matini ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo humlazimisha mtafiti kupitia matini mbalimbali (Ponera, 2019). Uchanganuzi wa matini hauwezi kufanywa hovyohovyo tu, bali huwa na mwongozo maalumu wa kufuatwa na unaodhihirisha nini kinachotakiwa kukusanywa na namna kitakavyokusanywa. Mbinu hii ya uchanganuzi wa matini inaelezwa na Kombo na Tromp (Whj) kama mbinu ya kukusanya data kupitia usomaji matini ili kupata taarifa muhimu zitakazotumika katika kutimiza malengo ya utafiti. Mtafiti alichunguza matini za walimu hasa wanavyoandaa masomo ili ahusishe na jinsi wanavyotekeleza kile wanachoandaa. Katika utafiti wetu, tuliamua kutumia njia ya uchanganuzi wa matini ili kupata taarifa tulizozitumia sio tu katika kuchunguza namna ambavyo walimu hujumuisha stadi ya tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo na tathmini bali pia katika kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi.

### 3.7.3 Usaili

Ponera (Khj) anasema usaili ni mbinu ambayo hutumiwa katika kukusanya data. Mbinu hii huhusisha mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa wake. Mazungumzo hayo huhusu taarifa ambazo mtafiti anazihitaji kwenye utafiti wake. Usaili ulitumiwa na mtafiti kuwahoji walimu wanaofundisha Kiswahili pamoja na wakuu wa masomo katika shule zilizoteuliwa ili kujibu maswali ya ufafiti. Usali ulitumiwa ili kukusanya taarifa kuhusu uelewa wa walimu na wakuu wa masomo kuhusu tafakuri bunifu, fasihi na utekelezaji wa MUU.

### 3.8 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni vitu pamoja na zana zote ambazo mtafiti huzitumia katika ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data. Katika utafiti wetu, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia vifaa tofauti ambavyo ni pamoja na kalamu, karatasi, madaftari, simu ya mkononi na kompyuta. Mosi, kalamu na karatasi ilitumiwa kwa kuandika taarifa tofauti wakati wa ushuhudiaji, usairi na uchanganuzi wa matini. Pili, simu ya mikononi ilitumiwa kwa kurekodi majibu ya wajiwa wakati wa usaili. Mwisho, kompyuta itumiwa ilitumiwa kwa kuandika, kuhifadhi na kutoa mjadala kuhusu matokeo ya utafiti.

### 3.9 UUchanganuzi wa Data

Unganuzi wa data ni kitendo cha kupanga vizuri, kuchagua, kulinganisha, kulinganua na kufasili data.  Ili kujibu maswali ya utafiti, utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo. Huu ni mkabala unaotumiwa na mtafiti ili kuchambua na kutolea maelezo ya kutosha kuhusu data za utafiti katika mwelekeo ambao unasaidia kutimiza malengo ya utafiti. Data za utafiti wetu zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaudhui, zikawasilishwa kwa kutumia njia ya maelezo na madondoo. Aidha, zilichambuliwa na kisha kufafanuliwa kwa kutumia maelezo ya kina yaliyojibu maswali ya utafiti.

### 3.10 Itikeli za Utafiti

Ponera (Khj) anasema kwamba itikeli za utafiti ni suala muhimu katika utafiti. Suala hili huweka wazi urazini wa mtafiti kuhusu thamani, haki na hadhi za washiriki wa utafiti. Ili kuhakikisha kuwa itikeli za utafiti zimefuatwa, mikakati ifuatayo ilizingatiwa: mosi, data za utafiti huu zilirekodiwa na kuhifadhiwa bila majina ili kutunza siri ya watafitiwa. Pili, mtafiti aliwaahidi watafitiwa kuwa taarifa watakazozitoa hazitatumiwa kwa

namna itakayowadhuru baadaye. Tatu, kabla ya kukusanya data, mtafiti aliwaelezea watafitiwa lengo kuu la utafiti wake. Nne, mtafiti aliwaomba ridhaa watafitiwa ili watafitiwe. Ridhaa hii iliombwa mapema. Wale waliokubali ndio waliotafitiwa. Tano, hakuna pesa zilizolipwa ili watafitiwa watoe taarifa. Isitoshe, kabla ya kukusanya data, mtafiti aliwaelezea wasailiwa namna watakavyofaidika na utafiti huu.

### 3.11 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa utafiti ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima mambo yanayotakiwa kutafitiwa tu (Guba na Lincoln, 1994). Kwa upande mwingine, uthabiti wa utafiti hufasiliwa kuwa ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kutoa matokeo yanayowiana pale utafiti utapofanyika mahali pengine, wakati tofauti na unapofanywa na mtu tofauti (Guba na Lincoln, Whj).

Hivyo basi, uhalali na uthabiti wa utafiti wetu ulijengwa kwa kutumia mbinu tofauti ambazo ni hizi zifuatazo: Mosi, mtafiti aliwaelezea watafitiwa malengo ya utafiti. Pili, mtafiti alitumia lugha rahisi inayoeleweka kwa kila mtafitiwa ili watafitiwa waweze kuelewa kinachotafitiwa. Jambo hili lilisaidia katika kuepuka changamoto zinazoweza kuibuka wakati wa kukusanya data. Tatu, njia mseto ilitumiwa katika ukusanyaji wa data. Dowson (2002) anasema kwamba njia mseto ni njia bora katika kujenga uhalali na uthabiti wa utafiti kwa sababu inaondoa uwezekano wa kujitokeza kwa hitilafu za kiutafiti ambazo zinaweza kusababishwa na mtafiti au watafitiwa. Kwa hiyo, katika utafiti huu, tulitumia njia ya mseto katika ukusanyaji data kama vile ushuhudiaji, uchanganuzi wa matini na usaili. Nne, ili kujenga uhalali na uthabiti katika utafiti huu, mtafiti alifuata methodolojia ya utafiti kama ilivyopangwa ili ajiepushe na kwenda nje ya jambo analofanyia utafiti. Halikadhalika, mtafiti aliepuka kuongozwa na hisia zake

kwa kutobadilisha taarifa zilizopatikana wakati wa ukusanyaji wa data. Mambo yaliyoelezwa hapo juu yaliwezesha utafiti huu kuwa na matokeo halali na thabiti.

**3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu**

Sura hii imefafanua mbinu na zana tofauti zilizotumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Katika kukamilisha mbinu za utafiti, vipengele vya paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, aina ya data zilizokusanywa, njia za kukusanyia data, vifaa vya utafiti, uchanganuzii wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na muhtasari wa sura ya tatu vilielezwa. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

# SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Utafiti wetu ulikusudia kutathmini nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu katika shule za sekondari wilayani Kicukiro nchini Rwanda. Aidha, utafiti ulilenga kutimiza malengo mahususi mawili ambayo ni kubainisha nafasi ya fasihi andishi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda, na pia kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda.

Sura hii inahusu mjadala na uwasilishaji wa data za utafiti. Hivyo basi, sura hii inahusisha sehemu zifuatazo: utangulizi, nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa tafakuri bunifu, na mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi, namna ya kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondarinchini Rwanda.

## 4.2 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Bunifu

Kwa mujibu wa Frank (2000), lugha huonekana kama rasilimali ambayo hutoa fursa inayochangia katika kuchochea ukuaji wa kiakili wa wanafunzi kupitia uhimizaji wa kufahamu na kuuelewa ulimwengu unaowazunguka. Hivyo basi, lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kubainisha nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu. Ili kutimiza lengo hili, tulijiegemeza kwenye mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Utambuzi iliyoasisiwa na Piaget (1983) ili kugundua namna ambavyo tafakuri bunifu hukua. Nadharia ya Utambuzi inadhihirisha kwamba stadi ya tafakuri bunifu inapaswa kuwa kiini katika elimu ya karne ya ishirini na moja. Hivyo basi, wakati wa ukusanyaji wa data, mosi, tulijikita kwenye kuchunguza uelewa

wa walimu kuhusu tafakuri bunifu, MUU na fasihi. Pili, tulitathmini mbinu zinazotumiwa na walimu katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Zaidi ya hayo, tulichunguza namna ambavyo walimu hujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo, ufundishaji na tathmini.

### 4.2.1 Uelewa wa Walimu kuhusu Tafakuri Bunifu, MUU na Fasihi

Utafiti huu uliokusudia kuchunguza ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia ufundishaji wa fasihi, ulikusanya taarifa tofauti kutoka kwa wahojiwa ambao ni walimu na wakuu wa masomo. Mosi, wahojiwa walitoa maoni yao kuhusu maana ya stadi za tafakuri bunifu kwa kujibu swali hili "Ni nini maana ya tafakuri bunifu?" wahojiwa walijibu yafuatayo:

> "Kwa upande wangu, mimi ninaichukua tafakuri bunifu kuwa ni uwezo alio nao mtu ambao humsaidia katika kutatua matatazo fulani. Uwezo huu ambao mtu anautumia kutatua matatizo ndio ambao ninauchukulia kama tafakuri bunifu (Mwalimu 1)."

Mwalimu huyu anaeleza kwamba tafakuri bunifu ni uwezo unaomwezesha mtu kutatua matatizo. Maelezo ya mwalimu huyu kuhusu maana ya tafakuri bunifu yana dosari kidogo. Mwalimu huyu ingawaje anahusisha tafakuri bunifu na uwezo wa kutatua matatizo, yeye haelezi ni uwezo wa aina gani. Hapa mtu anaweza akajiuliza ikiwa ni uwezo wa kiuchumi, wa kimwili, wa kisiasa au wa kufikiri. Tulipojiegemeza kwenye maelezo yaliyotolewa na Mwalimu 1, tuliona kwamba yeye haelewi vizuri maana ya tafakuri bunifu. Baada ya kuona kuwa mwalimu wa kwanza aliyeulizwa ana uelewa wa hali ya chini kuhusu maana ya tafakuri bunifu, tuliamua kumuuliza mwalimu wa pili ili kupata taarifa za kutosha kuhusu uelewa wa washiriki wa utafiti kuhusu maana ya tafakuri bunifu.

> "Tafakuri bunifu ni stadi inayomwezesha binadamu kuzalisha fikra mpya zinazomwezesha kufanikiwa katika hali tofauti. Fikra mpya hizi zinaweza zikatofautisha mbinu ya utendaji wako wa mambo na namna ambavyo wengine huyatenda (Mwalimu 2)."

Dondoo la hapo juu linaonesha kuwa mwalimu huyu anaichukulia tafakuri bunifu kama stadi ambayo humpa mtu uwezo wa kuzalisha fikra ambazo humsaidia kukabiliana na kila hali. Tulipomaliza kuona kuwa walimu walioshiriki kwenye utafiti wetu hawana uelewa wa kutosha kuhusu maana ya tafakuri bunifu, tulitaka kujua ikiwa wakuu wa masomo wanaelewa maana ya tafakuri bunifu. Mkuu wa masomo aliyeulizwa alisema yafuatayo:

> "Tafakuri bunifu ni namna ya kina ambayo ni muhimu sana katika maisha ya mtu ya kila siku. Kama mtu anaweza kufikiri sana, tunaweza kusema kwamba ana tafakuri bunifu ya hali yajuu (Mkuu wa Masomo 1)."

Dondoo hili linaonesha kwamba Mkuu wa Masomo 1 anafahamu kuwa tafakuri bunifu ni uwezo wa kufikiri kwa kina tu. Sisi, hatukubabiliani na maelezo haya kwa kuwa hakuwezikuhusisha uzalishaji wa fikra mpya, utatuzi wa matatizo na changamoto zinazokabili jamii katika maelezo aliyoyatoa.

Madondoo ya hapo juu ya walimu na mkuu wa masomo yanaonesha kwamba walimu na mkuu wa masomo hana uwezo wa kueleza maana ya tafakuri bunifu ilivyo. Maelezo waliyoyatoa ni kinyume na maelezo yaliyotolewa na

Emmit & Wilson(2005) wasemao kwamba tafakuri bunifu ni stadi ya inayomwezesha binadamu kutafakari na kupata uamuzi kwa namna inayotofautiana na namna nyingine ili kukabiliana na changamoto zinazokabili mafanikio ya wanajamii.

Hivyo basi, wakati wa ukusanyaji wa data, tuliona kwamba walimu na mkuu wa masomo wana uelewa wa hali ya chini kuhusu maana ya tafakuri bunifu. Kama mwalimu haelewi vizuri maana ya tafakuri bunifu itakuwa vigumu kwake kuijumuisha katika ufundishaji na ujifunzaji.

Pili, katika utafiti wetu tulitaka kujua maoni ya watu tofauti kuhusu maana ya MUU. MUU ni mtaala ambao unahusika kwa kiwango kikubwa na ubunifu wa mwanafunzi. Hii ni kwa sababu, stadi ya tafakuri bunifu ni kiini cha utekelezaji wa MUU. Wakati wa ukusanyaji data za mahojiano, tulipata maoni yafuatayo kuhusu MUU kutoka kwa walimu pamoja na wakuu wa masomo. Tuliuliza swali hili: “Ni nini maana ya MUU?” Majibu yaliyopatikana ni haya:

> “MUU ni mtaala unaopendekeza kwamba mwalimu analazimika kumpa mwanafunzi uwezo wa hali ya juu utakaomwezesha kufanikiwa katika maisha yake ya siku zijazo (Mwalimu 3).”

Dondoo la hapo juu linaonesha wazi kwamba MUU ni mtaala ambao hulenga kumpa mwanafunzi uwezo wa hali ya juu. Kutokana na maelezo yaliyotolewa na Mwalimu wa 3, tuliona kwamba si maelezo kamili ya MUU. Kwa kujiegemeza kwenye maelezo hayo, Mwalimu 3, haelewi maana ya MUU. Tulipomaliza kuona kuwa mwalimu alishindwa kueleza maana ya MUU ipasavyo, tulikikusanya taarifa kuhusu maana ya MUU kutoka kwa wakuu wa masomo.

> “MUU ni mtaala ambao ulikuja kuziba ufa katika sekta ya elimu. Ufa huu ulisababishwa na mtaala uliokuwapo hapo awali ambao ulisisitizia ufahamu wa mwanafunzi tu. Kwa hiyo, MUU ni mtaala ambao kabisa unalenga kumtayarisha mwanafunzi kukabiliana na kila hali katika maisha ya shule na ya nje ya shule kwa kuwa MUU humpa uwezo wa kutosha (Mkuu wa Masomo 2).”

Dondoo la hapo juu linaonesha kuwa Mkuu wa Masomo 2, anachukua MUU kama mtaala uliobadili mtaala uliokuwapo zamani. Yeye anaelewa kwamba MUU unalenga kumpa mwanafunzi uwezo wa kutosha. Ingawaje maelezo aliyoyatoa kuhusu maana ya MUU ni mazuri, hata hivyo nayo bado yana dosari kidogo kwa kuwa hakukumbuka kugusia stadi na maadili katika maelezo yake.

Maelezo yaliyotolewa na Mwalimu 3 na Mkuu wa Masomo 2 hayaelezi vizuri maana ya MUU. Maelezo yaliyotolewa hayachukuani na maelezo yaliyotolewa na Kellie (2019) anayesema kwamba MUU ni mtaala ambao malengo yake muhimu ni kumpa mwanafunzi uwezo, maadili na stadi ambazo zitamwezesha kufaulu katika maisha. Hivyo basi, uelewa wa hali ya chini kuhusu maana ya MUU ulidhihirika kama changamoto ambayo inaweza ikakabili utekelezaji wa MUU katika madarasa ya fasihi.

Tatu, wakati wa ukusanyaji data za mahojiano, walimu walitoa maoni yao kuhusu maana ya fasihi kwa kujiu swali hili: “Ni nini maana ya fasihi?” Baadhi ya walimu waliotoa maoni yao kuhusu maana ya fasihi, walitoa maelezo yafuatayo:

> "Fasihi ni kazi ya sanaa inayoonesha mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia mbinu mbalimbali. Pia, fasihi ni utumiaji wa sanaa ili kuwasilisha ujumbe unaokuwa katika moyo wa binadamu (Mwalimu 4)."

Maelezo ya Mwalimu 4 yanaonesha kuwa mwalimu huyu anaelewa kuwa fasihi ni sanaa ya kuwasilisha mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia mbinu tofauti. Sisi hatukubalini na maelezo ya Mwalimu 4 kwa sababu kama mtu anaeleza fasihi bila kugusia lugha huwa anapotosha maana ya fasihi. Kwa hiyo, kwa kujiegemeza kwenye maelezo yaliyotolewa, inaonekana wazi kuwa Mwalimu 4 ana uelewa wa hali ya chini kuhusu maana ya fasihi. Tunasema haya kwa sababu maelezo yaliyotolewa hayachukuani na maelezo yaliyotolewa na Wamitila (2003) kuhusu maana ya fasihi. Mtafiti huyu anaeleza fasihi kama kazi za kisanaa au zinazotumia lugha kisanii na ambazo zinawasilisha swala maalum kwa kutumia mbinu inayoathiri maisha ya watu. Utafiti wetu unaunga mkono maelezo ya Wamitila (Khj) kwa kueleza fasihi kama kazi ya sanaa inayolenga kuwasilisha hisi, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha.

Katika sehemu hii, tuliona kwamba uelewa wa walimu na wakuu wa masomo hawana uelewa wa kutosha kuhusu maana ya tafakuri bunifu, MUU na fasihi. Sehemu anayofuata inahusu namna ambavyo walimu hufundisha stadi ya tafakuri bunifu katika fasihi.

### 4.2.2 Namna ambavyo Walimu HufundishaTafakuri Bunifu kupitia Fasihi

Katika sehemu hii, tulikusanya data ili kutathmini mbinu zinazotumiwa na walimu katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Katika ushuhudiaji, tulipata taarifa zifuatazo:

Baadhi ya walimu walioshuhudiwa, walionekana kwamba hawafanikiwi kufundisha stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi. Kwa mfano, kuna mwalimu tuliyemshuhudia ambaye alikuwa akifundisha somo la "Tanzu za Fasihi" Mwalimu huyu alifuata hatua zifuatazo:

Mosi, alipomaliza kuwasalimu wanafunzi, aliwauliza maswali yafuatayo: i) Jana tulijifunza nini? Ii) Ni nani ambaye anaweza kueleza tuliyosoma kuhusu maana ya fasihi?

Pili, mwalimu aliwajulisha somo ambalo walikuwa wanaenda kujifunza. Aliandika somo ubaoni "Tanzu za Fasihi."

Tatu, aliwaomba wanafunzi kukaa kwenye makundi ya wanafunzi watano watano na kuwapatia vitabu vya Kiswahili. Kisha aliwaomba kusoma vitabu kwenye ukurasa ambao unazungumzia tanzu za fasihi simulizi ili kujibu maswali yafuatayo: i) Taja na ueleze tanzu kuu mbili za fasihi. ii) Linganisha na ulinganue tanzu kuu mbili za fasihi. iii) Eleza vitanzu vidogo vinavyopatikana katika kila tanzu kuu ya fasihi.

Baada ya muda mfupi, mwalimu aliomba kila kundi kuja kuwasilisha yale waliyoyafanya. Baadaye, aliwaomba wanafunzi kutunga hadithi fupi kuhusu mapenzi ya watu wawili.

Kwa kweli, taarifa za hapo juu zilizopatikana wakati wa ushuhudiaji, zinaonesha kuwa kuna dosari katika ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi. Kwa mara ya kwanza, mwalimu alipoanzisha somo, alitumia namna ambayo haishirikishi kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa ubunifu wa wanafunzi. Jambo hili ni tofauti na mhimili wa Nadharia ya Utambuzi idhihirishayo kwamba ukimfundisha mwanafunzi bila kumshirikisha katika ujifunzaji, unamnyima milele uwezo wa kufikiri. Badala ya kuandika somo

ubaoni, mwalimu angewauliza wanafunzi maswali ambayo yanawachochea kutumia akili ili kugundua somo ambalo wanaenda kujifunza.

Dosari nyingine ni kwamba, mwalimu wa hapo juu, alipowaweka wanafunzi katika makundi, hakukumbuka kuchunguza ikiwa kila mwanafunzi anashiriki katika kazi walizopewa. Ilionekana kwamba katika baadhi ya makundi, mwanafunzi mmoja au wawili ndio ambao walionekana kama wenye mchango mkubwa katika kundi, pengine, maswali mwalimu aliyowauliza wanafunzi ni ya hali ya chini, kwa hiyo si maswali mazuri katika ukuzaji wa tafakuri bunifu. Kwa mujibu wa mhimili wa Nadharia ya Utambuzi, ubunifu si nakala ya kweli, lakini ni zao la mwingiliano wa mtu na mazingira anamoishi. Hivyo basi, mwalimu huyu angewauliza wanafunzi maswali ambayo yangewachochea kuhusisha somo la fasihi na maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, angewauliza: i) Chambua kifungu "Kwa nini chura ana ngozi mbaya" ueleze ni utanzu gani wa fasihi. ii) Tunga sentensi kumi za Kiswahili sanifu kuhusu heshima na adabu kwa kutumia nahau kumi tofauti. iii) Jadili umuhimu wa mafumbo na vitendawili katika maendeleo andelevu ya nchi.

Baada ya kushuhudia walimu wakifundisha madarasani, tuliwauliza walimu swali hili:

**"**Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unakuzaje stadi ya tafakuri bunifu unapofundisha fasihi?"

Yafuatayo ni baadhi ya majibu yaliyotolewa:

> "Ninakuza stadi ya tafakuri bunifu kwa wanafunzi kupitia kazi za fasihi ninazowapatia wanafunzi wangu. Kwa mfano, ninapofundisha utanzu wa fasihi andishi kama hadithi fupi,

> ninaweza kuwapatia kazi ya kutunga hadithi fupi inayoeleza kuhusu mapenzi kati ya watu wawili na kushughulikia mada tofauti za fasihi, kazi za makundi, michezo na kazi zinazohitaji kufanya utafiti. Wakati huo mwanafunzi atachukua muda wa kufikiri sana na atakuwa anakuza stadi yake ya tafakuri bunifu kupitia kazi hii ya kifasihi (Mwalimu 5)."

Dondoo hili linaonesha kuwa mwalimu huyu alisema kwamba anakuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kwa kuwapa wanafunzi kazi za kutunga hadithi kuhusu mapenzi na kushughulikia mada tofauti za fasihi. Mwalimu huyu anaamini kwamba kupitia kazi za kutunga hadithi kuhusu mapenzi na kushughulikia mada tofauti za fasihi mwanafunzi atakuwa anakuza stadi za tafakuri bunifu. Kwa kweli mwalimu huyu haelezi wazi mwongozo wanaolazimika kuufuata wanafunzi katika kazi za kutunga hadithi kuhusu mapenzi na kushughulikia mada tofauti za fasihi. Kushindwa kwa Mwalimu 5 kueleza mwongozo wa kufuatiliwa na wanafunzi katika kazi wanazopewa, kunakuwa chanzo cha kutofanikiwa katika ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi. Heinigy (Khj) anasema kwamba tafakuri bunifu hulenga kutatua tatizo fulani kwa kutumia mbinu mpya. Baada ya kuona kuwa kuna dosari katika mbinu zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi, tulitaka kujua ikiwa walimu wanafanikiwa kujumuisha stadi ya tafakuri bunifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa hiyo, tulifanya uchunguzaji wa namna ambavyo walimu hujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo, ufundishaji na tathmini.

#### 4.2.3 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Andalio la Somo

Tafakuri bunifu ni sehemu muhimu sana katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa stadi za tafakuri bunifu humpa mwanafunzi motisha ya kufurahia yale anayofundishwa (Mustafa, 2019). Hivyo basi, walimu hawana budi kujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika maandalizi yao ya masomo. Kwa sababu hiyo, katika utafiti wetu tulitaka kujua ikiwa walimu hufanikiwa kujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika andalio la somo. Ili kupata taarifa za kutosha, utafiti huu ulitumia ushuhudiaji pamoja na upitiaji nyaraka. Yafuatayo ni baadhi ya maandalio yaliyopitiwa:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mada | **LUGHA KATIKA SANAA** | | |
| Uwezo uhitajiwao katika somo | Mwanafunzi aweze kuelewa fasihi katika Kiswahili kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano | | |
| Somo lenyewe | **AINA ZA FASIHI: TANZU ZA FASIHI SIMULIZI** | | |
| Malengo ya kujifunza | Kwa kutumia vifungu mbalimbali, kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:<br>-Kuorodhesha tanzu za fasihi simulizi<br>-Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi<br>-Kuhusisha mila na desturi mbalimbali katika kuaga na kumbulishana salamu | | |
| Mahali mbapo somo litafundishiwa | | Somo litafundishiwa darasani | |
| Vifaa au zana kwa wanafunzi wote | | Kitabu cha mwalimu, kitabu cha mwanafunzi na kamusi. | |
| Vitabu vya rejelea | REB (2018). Kitabu cha Kiswahili IV. Kitabu cha Mwanafunzi & Mwalimu. Kigali. | | |
| Muda na hatua | **Mbinu za kufundisia na kujifunzia** | | Tafakuri tunduizi na maswala mtambuka vielezwe +maelezo mafupi |
| | Kwa kutumia vifungu vya habari tofauti, mwalimu atawawezesha wanafunzi kuonesha kwa usahihi matumizi sahihi ya sauti za Kiswahili, kutumia msamiati husika kwa matamshi na tahajia bora kwa usahihi na kuhusisha mila na desturi mbalimbali katika kuaga na kumbulishana salamu | | |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| Utangulizi Dakika. 10 | Kuuliza maswali ya kukumbusha somo la awali | Kujibu maswali maswali ya kukumbusha somo la awali | Mawasiliano katika lugha rasmi. |
| Somo lenyewe<br><br>Dakika: 50 | Kutoa tathmini tanguluzi<br><br>Kuwakaza wanafunzi kwenye makundi na kuwapatia wanavunzi tathmini endelezi.<br><br>Kuchunguza ikiwa kazi ianafanywa na kutoa msaada kama unahitajika.<br><br>Kuomba wanafunzi kwasilisha na kuwasaidia kusahihisha yaliyowasilishwa na kuyafanyia ufupisho | Kujibu maswali ya tathmini tangulizi<br><br>Kukaa kwenye makundi na kujibu maswali ya tathmini endelezi<br><br>Kufanya kazi na kuomba msaada kwa mwalimu kama unahitajika.<br><br>Kuwasilisha, kuungana mkono na mwalimu katika kusahihisha yaliyowasilishwa, kuyafanyia ufupisho na kuuandika madaftarini | Ubunifu na utatuzi wa matatizo.<br><br>Ujifunzaji wa muda mrefu |
| Hitimisho Dakika: 20 | Kuoa tathmini jumuishi | Kujibu maswali tathmini jumuishi | |
| Tathmini ya mwalimu | Lilifundishwa. | | |

**Kielelozo 1: Andalio la Somo (1)**

Andalio la somo hapo juu, linaonesha kuwa mwalimu aliyeandaa somo hili alitumia "*ubunifu na utatuzi wa matatizo*" kumaanisha tafakuri bunifu. Pengine alipoonesha uwezo wa ujumla ambao somo hukusudia kukuza miongoni mwa wanafunzi hakuweka maelezo yanayoonesha namna ambavyo uwezo huo utakuzwa kupitia somo aliloandaa. Vilevile, katika maswala mtambuka, andalio la somo la hapo juu halihusishi vema maswala mtambuka. Ikumbukwe kwamba, kama uwezo wa jumla maswala mtambuka

hayahusishwi ipasavyo katika andalio la somo, ni vigumu kwa mwalimu kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa hakika, andalio hili halielezi kinagaubaga namna ambavyo mwalimu huyu atakuza stadi za tafakuri bunifu wakati wa ufundishaji. Aidha, andalio la somo la hapo juu halielezi namna ambavyo mwalimu atawashirikisha wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Jambo hili haliendani na mhimili wa Nadharia ya Utambuzi unaosisitiza kwamba utumiaji wa mbinu shirikishi katika elimu ni mbinu bora ya kukuza ugunduzi na ubunifu wa mwanafunzi. Vilevile, tukirejelea sehemu ya malengo ya kujifunza, inadhihirika kuwa, ingawaje malengo yamekaa vizuri, bado yalihitaji yangefanyiwa marekebisho ili kulenga ukuzaji wa ubunifu miongoni mwa wanafunzi, badala ya kuandika:

Kwa kutumia vifungu mbalimbali, kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze:

-Kuorodhesha tanzu za fasihi simulizi

-Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi

-Kuhusisha mila na desturi mbalimbali katika kuaga na kutuma salamu

Angesema kwa mfano:

Kwa kutumia tanzu tofauti za fasihi simulizi, kwenye mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi darasani atakuwa na uwezo wa:

-Kueleza mchango wa kila utanzu wa fasihi simulizi katika maendeleo endelevu ya jamii anamoishi

-Kutunga kazi tofauti za fasihi simulizi zinazochangia katika utatuzi wa matatizo


-Kuhusisha mila na desturi za jamii katika utungaji wa kazi za fasihi zimulizi.

Maelezo ya hapo juu yanadhihirisha kuwa mwalimu aliyeandaa somo hilo hana uelewa na uwezo wa kutosha kuhusu andalio la somo linaloweza kuwasaidia walimu kufundisha stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi. Maelezo haya yanaungwa mkono na matokeo ya utafiti uliofanywa na Komba na Mwandanji (2015: 43) yanaonesha kuwa walimu wanashindwa kutekeleza MUU kutokana na ukosefu wa ujuzi kuhusu MUU kama inavyoonyeshwa na dondoo la hapa chini:

> Idadi kubwa ya walimu (86%) hawana maarifa ya kutosha kuhusu mtaala. Zaidi ya hayo, utafiti uliripoti kuwa idadi kubwa ya maandalio ya somo (78%) yaliyopitiwa hayakutimiza sifa za andalio la somo linalopendekezwa na MUU (Tafsiri Yetu).

Maelezo haya yanaonesha bayana kuwa idadi kubwa ya walimu haifanikiwi kuandaa somo ambalo linakidhi mahitaji ya MUU. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa walimu hawafanikiwi ipasavyo kujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo.

Baada ya kuchunguza andalio la somo la 1, tuliona kwamba ni lazima tuchunguze andalio la somo jingine ili tupate taarifa za kutosha kuhusu ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika andalio la somo.



| | | | |
|---|---|---|---|
| Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao | — | | |
| Mada | Lugha katika fasihi | | |
| Uwezo uhitajiwao katika somo | Kuweza kueleza dhana ya fasihi simulizi | | |
| Somo lenyewe | Umuhimu wa fasihi simulizi | | |
| Malengo ya kujifunza | - Kuweza kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi<br>- Kutambua umuhimu wa fasihi simulizi | | |
| Mahali ambapo somo litapofundishiwa | Darasani | | |
| Vifaa au zana kwa wanafunzi wote | Vitabu vya kiswahili, matini ya kiswahili | | |
| Vitabu vy rejea | Kiswahili, kidato cha 4 | | |
| Muda na hatua | Mbinu za kufundishia na kujifunzia: Kupitia majadiliano na mazoezi miongoni mwa wanafunzi x mwalimu | | Tafakuri tunduizi na maswala mtambuka vielezewe+maelezo mafupi |
| | Wajibu wa mwalimu | Wajibu wa mwanafunzi | |
| Utangulizi Dakika 10 | Kuuliza maswali kuhusu tanzu za f. simulizi | Kujibu maswali kuhusu tanzu za fasihi simulizi | |
| Somo lenyewe Dakika 60 | Kuomba wanafunzi kuunda makundi na kujaribu kutafuta mambo kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi<br>Kueleza mambo tofauti kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi | Kuunda makundi ya wanafunzi wawili wawili na kutafuta umuhimu wa fasihi simulizi. | Elimu itiyo na ubaguzi<br>Majori watakayounda hayatakuwa na ubaguzi wowote |
| Hitimisho Dakika 10 | Kuandika kazi ya nyumbani | Kuweka kazi ya nyumbani daftarini. | |
| Tathmini ya mwalimu | | | |

**Kielelezo 2: Andalio la Somo (2)**

Kama ilivyofanywa kwenye kielelezo (1), aliyeandaa somo hili alidhihirisha maswala mtambuka akasahau kuonesha uwezo wa jumla ambao utakuzwa kupitia somo. Kwa kweli kama uwezo wa ujumla haudhihiriki katika andalio la somo, ni vigumu sana kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Andalio hili la somo "*Umuhimu wa Fasihi Simulizi*" linaonesha kwamba mwalimu huyu hakujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika andalio lake la somo. Tulipochunguza vizuri, mosi, tuligundua kuwa mwalimu anatumia mtindo huu kwa kuwa unahitaji muda mfupi. Kwa kutaka kutunza muda, mwalimu huyu alisahau kuweka uwezo wa jumla kwenye andalio la somo

lake. Pili, inadhihirika kuwa mwalimu huyu hana uelewa kuhusu andalio la somo. Andalio la somo kama hili linaweza likapotosha ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

Maelezo yanayotolewa hapo juu kutokana na maandalio ya masomo yaliyopitiwa hayaendi mbali na matokeo ya utafiti uliofanywa na Sitenei (2020) ili kuchunguza mambo yanayoathiri utekelezaji wa MUU nchini Kenya. Matokeo ya utafiti yalionesha kwamba utekelezaji wa MUU unaathiriwa na mambo mengi yakiwemo uwezo wa hali ya chini wa walimu. Matokeo yalionesha kwamba idadi kubwa ya walimu (81.6%) walihudhuria warsha ya wiki moja kuhusu MUU, wakati ambapo walimu (18.4%) walihudhuria warsha ya wiki mbili. Matokeo haya yanaonesha kuwa walimu wengi hawajapata mafunzo ya kutosha juu ya MUU.

Pia, matokeo ya utafiti tuliofanya yanalingana na matokeo ya utafiti wa Momanyi na Rop (2019: 14) kuhusu utekelezaji wa MUU katika shule za serikali katika eneo la Nandi nchini Kenya. Matokeo hayo yalionesha kuwa idadi kubwa ya walimu hawana uwezo wa kuandaa somo ipasavyo. Walisema yafuatayo:

> Idadi kubwa ya wahojiwa (90%) walisema kwamba hawana uwezo wa kuandaa somo ipasavyo, walisema kwamba wana changamoto katika kudhihirisha majukumu ya mwalimu na mwanafunzi ambayo yatawawezesha wanafunzi kupata uwezo unaotarajiwa (TafsiriYetu).

Dondoo hili linasisitiza kwamba kuna changamoto ya uandaaji wa maandalio ya masomo yanayojumuisha stadi za tafakuri bunifu. Tatizo hili linajitokeza pia katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Hivyo, kama

mwalimu hawezi kuandaa somo ipasavyo, itakuwa vigumu kwake kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Isitoshe, Sarika (2020: 3) naye alifanya utafiti kuhusu mambo yanayoathiri walimu wanapoandaa masomo ya kufundisha. Alisema yafuatayo:

> Idadi kubwa ya walimu hufanya makosa katika maandalio ya masomo kwa sababu hawana muda wa kutosha. Tofauti na zamani ambapo walimu walikuwa na jukumu la kutimiza mtaala na kutathmini tu, leo hali ilikuwa ngumu sana. Leo, walimu wana majukumu mengi sana darasani. Hivyo basi, ni vigumu sana kwa walimu kushughulikia majukumu hayo. Jambo hili huwanyima muda wa kutosha wa kutayarisha masomo (Tafsiri Yetu).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa walimu hawana muda wa kutosha wa kutimiza majukumu yao yote. Maelezo haya yana ukweli kwa kuwa walimu shuleni wanakuwa na majukumu mengi ya kutimiza. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kufundisha wanafunzi, kusimamia nidhamu ya wanafunzi, kusimamia usafi shuleni, kusahihisha, kuadaa kazi za ufundishaji, kushauri wanafunzi, kushirikiana na wazazi katika malezi na makuzi ya wanafunzi, tukitaja kwa uchache. Hivyo basi, kutokana na majukumu mengi, walimu hawafanikiwi katika kujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo.

Wakati wa ukusanyaji data, tulibaini kwamba maandalio ya masomo yaliyoandaliwa na walimu yalikuwa hayaoneshi bayana namna ambavyo walimu watakuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kupitia fasihi. Baada ya kugundua kwamba walimu hawafanikiwi katika ujumuishaji

wa stadi za tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo, tulitaka kujua ikiwa walimu wana uwezo wa kuzijumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji hata kama hawawezi kuzijumuisha katika maandalio yao ya masomo.

### 4.2.4 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Ufundishaji

Kwa mujibu wa Torre (2009), ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu huwakilishwa na kuwahusisha wanafunzi, kuwahamasisha, kuwasisimua na kuwamotisha. Mtafiti huyu anaendelea kueleza kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za tafakuri bunifu huhusu ujuzi uliojengwa na ushiriki kamili wa somo kutoka katika andalio mpaka katika ufundishaji wake. Ujuzi huu huwapa wanafunzi hamu ya ndani na nafasi ya kujieleza bila uoga kwa kuwaweka wanafunzi katika mchakato wa kielimu. Hii inamaanisha kwamba wakati wa ufundishaji wa somo linalolenga kukuza stadi za tafakuri bunifu, mwalimu hana budi kuwashirikisha wanafunzi katika somo kwa kutumia mbinu zinazoweza kuwachochea kutumia fikra zao.

Hii inawasaidia kugundua mbinu mpya za kukabiliana na changamoto kadhaa zinazojitokeza katika jamii wanamoishi. Kwa hivyo, wakati wa ukusanyaji data, hasa wakati wa usaili na ushuhudiaji kila mwalimu aliyeulizwa ikiwa anajumuisha stadi za tafakuri bunifu, alijibu kwamba anajaribu kuzijumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wake. Hata wakuu wa masomo nao walijibu kwamba walimu wao wanajumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wao. Walitoa jibu hili kwa kuwa wanajua kwamba ujumuishaji wa tafakuri bunifu na stadi nyingine za karne ya ishirini na moja ni mambo ya lazima ili kutekeleza MUU. Kwa mujibu wa IBE (2017), katika mchakato wa kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji, jukumu la mwalimu sio kutoa mafunzo tu. Jukumu la mwalimu ni kutumika kama mwelekezaji,

mrahisishaji na mwezeshaji wa stadi ambazo ni mawasiliano na ushirikiano, tafakuri tunduizi na utatuzi wa matatizo, tafakuri bunifu, uraia, ufanisi wa kibinafsi na TEHAMA. Kwa kuwa ni sharti kujumuisha uwezo wa kiujumla katika ufundishaji kama unavyopendekeza MUU, wahojiwa wote walijibu kuwa stadi za tafakuri bunifu zinahusishwa katika ufundishaji.

Kabla ya kushuhudia kila mwalimu akifundisha, tulifanya usaili na kila mwalimu aliyeshuhudiwa ili kukusanya taarifa kuhusu ujumuishaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Tuliuliza swali hili "Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unaijumuisha stadi ya tafakuri bunifu unapofundisha fasihi?" Yafuatayo ni baadhi ya majibu yaliyotolewa na walimu:

> "Ndiyo, mimi wakati ninapokuwa ninafundisha fasihi ninajaribu ipasavyo kujumuisha tafakuri bunifu. Ninaijumuisha tafakuri lakini nakumbwa na tatizo la utumiaji wa lugha kwa wanafunzi" (Mwalimu 4)."

Jibu hili linaonesha kwamba mwalimu huyu anajumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji ingawaje anakumbwa na changamoto inayotokana na wanafunzi ambao wana ujuzi wa hali ya chini kuhusu lugha ya Kiswahili. Baada ya kupata taarifa kutoka kwa mwalimu huyu, tulijaribu kumuuliza mwalimu mwingine ili tuchunguze na hatimaye tupate taarifa za kutosha. Mwalimu mwingine alitoa jibu la hapo chini.

> "Ninajaribu kuijumuisha stadi ya tafakuri bunifu kwa sababu kama tunavyojua fasihi ni kama maisha ya kila siku na tafakuri bunifu kama stadi muhimu haiwezi kukosekana katika ufundishaji wowote. Ndiyo sababu wakati wa ufundishaji wa fasihi siwezi

> kusahau kusisitizia tafakuri bunifu (Mwalimu 6)."

Jibu la mwalimu huyu linaonesha kwamba yeye anafahamu umuhimu wa kujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wa somo lolote. Yeye anasema kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya maisha ya kila siku na stadi za tafakuri bunifu. Maelezo haya hayatoshi kwa kuwa Mwalimu 6 haelezi uhusiano huo uliopo kati ya tafakuri bunifu na maisha ya kila siku. Baada ya kupata taarifa kutoka kwa walimu, tulijaribu kukusanya data kutoka kwa wakuu wa masomo ili kupata taarifa za kutosha kuhusu ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji. Tuliulisa swali hili "Je, walimu wa Kiswahili wanaijumuisha stadi ya tafakuri bunifu wanapofundisha?"

Wakuu wa masomo nao walitoa majibu yafuatayo:

> "Kwa uhakika waalimu wanajumuisha stadi za tafakuri bunifu katika shughuli zao za kufundisha kwa sababu walimu huwapa wanafunzi nafasi ya kuchunguza uwezo wao wa kujaribu kufanya vitu peke yao kwa mfano wanaweza kusoma shairi na kwa kujiegemeza kwenye yale waliyoyasoma, wakaweza wenyewe kutunga shairi wao wenyewe (Mkuu wa Masomo 4)."

Mkuu wa masomo anasema kuwa walimu wake wanajumuisha stadi ya tafakuri bunifu katika ufundishaji wao. Baada ya kuambiwa kwamba stadi za tafakuri bunifu zinahusishwa katika ufundishaji, tulitaka kujua namna ambavyo stadi hizo huhusishwa katika ufundishaji. Ili kupata taarifa mwafaka, walimu walioshiriki katika utafiti wetu walilazimika kujibu swali

lifuatalo: “Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unaijumuishaje stadi ya tafakuri bunifu unapofundisha fasihi?” Hapo chini ni baadhi ya taarifa zilizopatikana:

> “Ninajumuisha stadi ya tafakuri bunifu kupitia kazi za fasihi ninazowapatia wanafunzi wangu. Kwa mfano ninapofundisha utanzu wa fasihi andishi kama hadithi fupi, ninaweza kuwapatia kazi ya kutunga hadithi fupi inayoeleza kuhusu mapenzi kati ya watu wawili. Wakati huo mwanafunzi atachukua muda wa kufikiri sana na atakuwa anakuza stadi yake ya tafakuri bunifu kupitia kazi hii ya kifasihi (Mwalimu 6).”

Dondoo hili linaonesha kwamba mwalimu huyu huzijumuisha stadi za tafakuri bunifu kwa kutumia kazi za kutunga hadithi fupi kuhusu mapenzi. Anaongeza kuwa kupitia kazi za utungaji wa kazi za fasihi, wanafunzi hukuza ubunifu wao. Dondoo hili ingawaje linatoa taarifa muhimu, lina dosari kidogo kwa sababu mwalimu huyu hahusishi kazi za utungaji anazowapa wanafunzi na maisha pamoja na utatuzi wa changamoto zinazoikabili jamii ambamo wanafunzi huishi. Baada ya kupata taarifa hizi kutoka kwa mwalimu wa kwanza, mwalimu wa pili alitoa taarifa zifuatazo:

> “Katika fasihi kuna tanzu tofauti ambazo nafundisha kama mwalimu.Tanzu hizo ni kama vile nahau, methali, hadithi, majigambo, ushairi, vitendawili, mizio na nyinginezo. Tanzu hizi zote humsaidia mwanafunzi kupanua uwezo wake wa kufikiri (Mwalimu2.”

Dondoo hili linaonesha kuwa mwalimu huyu anapofundisha fasihi, anazijumuisha stadi za tafakuri bunifu kwa kuhusisha fasihi na maisha ya kila

siku ya wanafunzi ili kukuza uwezo wa kufikiri. Ingawaje mwalimu huyu hakueleza namna ambavyo anahusisha fasihi na maisha ya kila siku, sisi tunakubaliana naye kwa kuwa fasihi inayohusika na binadamu na maisha yake inaweza kutumiwa ili kukuza ubunifu wa mwanafunzi kutokana na mwingiliano wake na jamii yake kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya nadharia ya utafiti wetu. Mwalimu wa tatu naye alitoa taarifa zifuatazo:

> "Ninapofundisha fasihi, ninajaribu kuwaweka wanafunzi katika makundi na kuwapatia mada tofauti za kazi ya kifasihi ambazo wanaweza kushughulikia. Katika kushughulikia mada hizo, watakuwa wanakuza uwezo wao wa tafakuri bunifu kama mojawapo ya stadi muhimu sana katika maisha ya kila siku (Mwalimu 6)."

Mwalimu huyu yeye alidhihirisha wazi kwamba anajumuisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wa fasihi kwa kuwapa kazi za makundi kuhusu mada tofauti. Anasema kwamba wanafunzi wanapokuwa wanashughulikia mada tofauti katika fasihi, huwa wanakuza ubunifu wao. Kwa kweli, mwalimu huyu hakudhihirisha namna ambavyo kazi hizi hutolewa, namna ambavyo zinakuza ubunifu na mwongozo anaoufuata ili kazi hizo za makundi zizae matunda katika utekelezaji wa malengo ya kufundisha na kujifunza yakiwemo ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Hivyo basi, tulikusanya data kutoka kwa mwalimu mwingine ili tuone ikiwa tunaweza kupata taarifa kinyume na zilizotangulia.

Mwalimu wa mwisho alisema:

> “Kuwapa wanafunzi kazi za kifasihi kama shairi la beti mbili na kuwaomba kuisoma na kuifanyia uchambuzi. Katika kufanya kazi hii watakuwa wanakuza uwezo wao wa kufikiri na kubuni kazi zinazowajengea uwezo wao katika maisha ya kila siku (Mwalimu 4).”

Mwalimu huyu alisema kwamba anahusisha stadi za tafakuri bunifu kwa kuwapa wanafunzi kazi za kifasihi na kuwaomba wazifanyie uchambuzi. Mwalimu huyu anaamini kuwa uchambuzi wa kazi za fasihi hukuza ubunifu wa wanafunzi. Maelezo haya hayatoshi kwa sababu si kila uchambuzi wa fasihi unaweza ukashiriki katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu. Mwalimu huyu angeeleza aina ya uchambuzi anaotaka kumaanisha na namna ambavyo unaweza ukashiriki katika ukuzaji wa ubunifu.

Madondoo ya hapo juu yanaonesha mbinu zilizotolewa na walimu kama mbinu wanazozitumia katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu. Mbinu zilizotolewa ni kama vile: utungaji wa kazi za fasihi, kuzungumzia maisha ya kila siku, kazi za makundi na uchambuzi wa mashairi.

Baada ya kupata majibu tofauti kuhusu ikiwa walimu wanajumisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wao, tulijaribu kuingia madarasani na kuwashuhudia wakifundisha ili kuchunguza ikiwa waliyoyasema wakati wa usaili wanayatimiza katika ufundishaji. Wakati wa ushuhudiaji, taarifa zilizopatikana ni kinyume sana na taarifa zilizotolewa na walimu pamoja na wakuu wa masomo kuhusu ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji.

Kwa kweli, wakati wa ukusanyaji data, tulishuhudia walimu sita wakitekeleza andalio la somo la fasihi madarasani. Ushuhudiaji ulifanyika

katika shule tofauti. Wakati wa ushuhudiaji, ilionekana wazi kuwa kati ya walimu sita walioshuhudiwa, ni walimu wawili tu ndio walijaribu kuhusisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wao kwa kutumia mbinu ya maswali wazi, drama bunifu na michezo tofauti ambayo iliwachochea wanafunzi kukuza ubunifu wao.

Kwa upande mwingine, ilionekana kwamba walimu wanne hawana uwezo wowote kuhusu ujumuishaji wa tafakuri bunifu wanapofundisha somo la fasihi. Matokeo haya yanatuonesha kwamba ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji kwenye shule za sekondari nchini Rwanda ungali kwenye kiwango cha chini. Ilionekana pia kwamba kutohusisha stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji hutokana na kwamba walimu wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu tafakuri bunifu na stadi nyingine muhimu zinazopendekezwa na MUU. Zaidi ya hayo, wakati wa ushuhudiaji tuliona kuwa ingawaje walimu wengi walihudhuria mafunzo tofauti kuhusu utekelezaji wa MUU, bado idadi kubwa ya walimu hawakuonesha mabadiliko. Tuliona kwamba kuna walimu ambao mpaka sasa wangali wanafundisha kwa kutumia mbinu za ufundishaji zinazolenga kukuza maarifa na ufahamu tu miongoni mwa wanafunzi. Tuliyoyapata katika ushuhudiaji yanaungwa mkono na matokeo ya utafiti uliofanywa na Muraraneza & Mtshali (2018: 36) kuhusu utekelezaji wa MUU nchini Rwanda. Matokeo ya utafiti wao yanaonesha kwamba utekelezaji wa MUU nchini Rwanda unaathiriwa na changamoto kadhaa zikiwemo walimu ambao walishindwa kubadilika. Wanasema:

> Nchini Rwanda changamoto inayokabili utekelezaji wa MUU ni kwamba walimu wote walifundishwa kuhusu utekelezaji wa MUU lakini wengine

> walishindwa kubadilika na kuanza kutumia mbinu mpya ya kufundisha kwani wamezoea sana mbinu za zamani na wengine wanajihisi vizuri zaidi wanapotumia vifaa vya ufundishaji walivyokuwa wanatumia awali, badala ya kutumia mbinu mpya zinazopendekezwa na MUU (Muraraneza & Mtshali, Whj).

Maelezo ya watafiti wa hapo juu yana ukweli kwa kuwa Mtaala Unaoegemea katika Maarifa ulitumiwa nchini Rwanda kwa muda mrefu. Kutokana na hayo, MUU ulipoanza kutekelezwa nchini Rwanda, baadhi ya walimu hawakubadilisha mbinu walizokuwa wakitumia katika ufundishaji. Hivyo basi, walimu walioshindwa kubadilika, hawakufanikiwa kutekeleza mahitaji ya MUU.

Ingawaje Nadharia ya Utambuzi inasema kwamba tofauti na wanyama na ndege, wanadamu wana uwezo wa kubadilisha mbinu za kukabiliana na kuunda mbinu nyingine mpya, maelezo ya Muraraneza & Mtshali (Whj) yanaonesha kuwa walimu waliozoea kufundisha ili kukuza maarifa na ufahamu wa wanafunzi kwa muda mrefu, ni vigumu sana kwao kubadilisha mbinu wanazotumia na kuanza kufundisha kwa kutumia mbinu mpya ili kukuza maarifa, ufahamu, stadi na maadili. Hii ni changamoto kubwa ambayo huhitaji wadau wa elimu kuungana mkono ili kukabiliana nayo.

Changamoto hii ilituchochea kutaka kujua namna ambavyo walimu hujumuisha stadi za tafakuri bunifu katika tathmini.


### 4.2.4 Ujumuishaji wa Tafakuri Bunifu katika Tathmini

Tathmini ni mchakato unaotumika ili kupima ufundishaji na ujifunzaji kwa kukusanya na kutafsili vigezo binafsi vya mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza na kutoa uamuzi kuhusu mafanikio ya mwanafunzi kuhusu upimaji wa viwango vilivyotolewa. Tathmini ni sehemu muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji. Katika mtaala wa upimaji wa ujuzi, tathmini inapaswa iwe imelenga katika ujuzi ambao mwanafunzi atapewa, mazingira mchanganyiko au magumu yanayohusiana na maisha yake ya kila siku, na pia kuambiwa atumie aliyojifunza katika kupambana au kujitatulia matatizo hayo (REB, 2015). Malengo ya ujifunzaji na ufundishaji hufikiwa kiurahisi wakati ambapo ufundishaji na tathmini hujikita kwenye mapendekezo ya mtaala wa kielimu.

Kama tathmini imeandaliwa kutokana na malengo yaliyopendekezwa na mtaala, walimu na wanafunzi hunufaika (Airasian, 1994). Namna wanafunzi wanavyotathminiwa ni muhimu sana kwa kuwa wanafunzi wana uwezekano mkubwa wa kujifunza wakati ambapo tathmini wanazopewa zinatathmini kile walichofundisha. Jambo hili hueleza wazi kuwa namna walimu wanavyotathmini wanadhihirisha namna walivyofundisha. Kama mwalimu anataka kukuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi, ni lazima ajikite kwenye stadi hizo siyo katika ufundishaji tu, bali na katika maandalio ya tathmini.

Hivyo basi, ili kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi, walimu wanalazimika kuandaa maswali ambayo yatawachochea kufikiri kwa kina. Ili kufanikisha mkabala wa tathmini, walimu huandaa tathmini kwa kufuata viwango vya ujuzi kutoka katika maswali rahisi kwenda katika maswali magumu.

Katika mwelekeo huu, Bloom (1956) anaeleza viwango vya ujuzi na uwezo vinavyotathminiwa katika kielelezo cha hapo chini kijulikanacho kama Takisonomia ya Bloom (Bloom's Taxonomy) .




**Kielelezo 3: Takisonomia ya Bloom (Bloom, 1956)**

Ball na Washburn (2001) wanasema kwamba ili kukuza uwezo wa kufikiri wa wanafunzi, walimu wanalazimika kujikita kwenye kuuliza maswali ambayo yanatathmini viwango vya ujuzi vya hali ya juu ambavyo ni kuchunguza, kutathmini na kubuni.

Katika kukusanya taarifa kuhusu ujumuishaji wa tafakuri bunifu katika tathmini, katika utafiti huu tulikusanya taarifa kuhusu usomaji makini wa tathmini zinazoandaliwa kwa kudadisi ikiwa kwenye sehemu ya fasihi walimu wanawauliza wanafunzi maswali ambayo yanaweza kukuza ubunifu wao. Zifuatazo ni baadhi ya tathmini zilizochunguzwa:

**SEHEMU YA TATU: FASIHI (Alama 35)** |

1) a)Fasili maana ya Fasihi ya Kiswahili. (alama 2)
   b) Orodhesha vipengele vya fasihi simulizi. (alama 4)
2) Jaza methali hizi kama inavyostahili ili iwepo maana kamili. (alama 7)
   a. Mtoto umleavyo…
   b. Asiyefunzwa na mamaye…
   c. Mtoto wa nyoka…
   d. Hakuna masika yasiyo…
   e. Haba nah aba …
   f. Simba mwenda pole …
   g. Fadhila ya punda…
3) **Linganisha methali kutoka A na maana mwafaka kutoka B. (alama 5)**


| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1.Ada ya mja hunena muungwana ni vitendo | a) Usisubiri misaada kutoka kwa wengine. |
| 2. Ahadi ni deni | b) Uvivu humfanya mtu kutokuwa na maendeleo maishani. |
| 3.Ajizi ni ufunguo wa umaskini | c) Ni muhimu kutumia busara tuliyopewa. |
| 4.Mtegemea cha nduguye hufa maskini. | d) Ni muhimu tutimize tuliyoyasema |
| 5.Akili ni mali | e)Vitendo ndivyo vinavyothibitisha utu wa mtu. |

4) a) Eleza maana ya fasihi simukizi.(alama 2)
   b) Fasihi simulizi ina umuhimu gani katika? (alama 4)
5) Tofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi.(alama 4)
6) a) Orodhesha aina za hadithi angalau tatu (alama 3)
   b) Ni aina gani ya hadithi inayosimulia kuhusu watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii? (alama 4)

**Kielelezo 4: Mfano wa Tathmini 1(Data za msingi, 2022)**

Kielelezo 4 kinaonesha mfano wa tathmini ya mwisho wa muhula wa pili mwaka wa 2018 kwa wanafunzi wa kidato cha nne, mchepuo wa LKK katika shule mojawapo ya shule zilizochaguliwa. Kama inavyoonekana, mtahini alijikita sana kwenye viwango vya chini vya ujuzi na uwezo. Jambo hili

hudhihirishwa na vitenzi alivyotumia katika tathmini yake kama vile: *eleza* (kukumbuka), *orodhesha* (kukumbuka), *jaza methali* (kukumbuka), *linganisha* (kufahamu), fafanua (kukumbuka) na *ni aina gani* (kukumbuka). Kwa hiyo, stadi za tafakuri bunifu hasa kwenye sehemu ya fasihi. Baada ya kuchanganua andalio la somo la kidato cha nne na kuona kuwa halijumuishi stadi ya tafakuri bunifu vilivyo, tuliamua kuchunguza andalio la somo la kidato caha tano mchepuo wa LKK ili kuchunguza ikiwa linatofautiana na la awali. Kielelezo cha hapo chini kinaonesha tuliyoyapata.



**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)**

11) Unafahamu nini kuhusu dhana ya fasihi? **(Alama 5)**
12) Kuna tofauti gani kati ya Fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa Kiswahili? **(Alama 5)**
13) **Kamilisha methali zifuatazo** **(Alama 10)**
a) .............sharti ainame.
b) ...............hufa maskini.
c) Hayawi hayawi.............
d) Usiwatukane wakunga.................
e) Asiyekuwepo .............

14) **Eleza maana ya nahau zifuatazo:** **(Alama 5)**

a) Kula chumvi nyingi
b) Kumwaga unga
c) Kuwa na ulimi wa upanga
d) Kumpa mtu nyama ya ulimi
e) Kuona/kupata cha mtemakuni

**Kielelezo 5: Mfano wa Tathmini 2(Data za msingi, 2022)**

Kielelezo nambari 5, kinaonesha mfano wa tathmini ya mwisho wa mwaka, kwa mwaka wa 2019 kwa wanafunzi wa kidato cha tano, mchepuo wa LKK

katika mojawapo ya shule miongoni mwa zilizochaguliwa. Kama ilivyoonekana katika Kielelezo nambari 4, mtahini huyu katika kielelezo nambari 5 alijikita sana kwenye viwango vya chini vya ujuzi na uwezo. Jambo hili linadhihirishwa na vitenzi alivyotumia katika tathmini ambavyo ni: *unafahamu nini* (kukumbuka), *kuna tofauti gani* (kukumbuka), *kamilisha* (kukumbuka), *eleza* (kukumbuka), *fafanua* (kukumbuka). Baada ya kuchunguza vitenzi vilivyotumiwa, ni dhahiri kuwa tathmini hii haijumuishi kamwe ukuzaji wa tafakuri bunifu.

Baada ya kuchunguza tathmini kadhaa zilizoandaliwa na walimu mbalimbali katika shule tofauti, iligunduliwa kuwa walimu wengi hawana uelewa kuhusu namna ya ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika tathmini. Hali hii husababishwa na kwamba wakati wa kuandaa tathmini, walimu wanaathiriwa na mtaala uliotangulia MUU ambao ni Mtaala Unaoegemea katika Uwezo. Ukweli huu hauendi mbali na matokeo ya utafiti wa Momanyi na Rop (2019: 14) kuhusu changamoto zinazokabili utekelezaji wa MUU nchini Kenya. Utafiti unaonesha kwamba idadi kubwa ya walimu huathiriwa na mihimili ya Mtaala Unaoegemea katika Maarifa. Wanasema:

> Asilimia 100 ya waliohojiwa walisema kuwa walimu wana changamoto katika utekelezaji wa MUU. Walionesha kuwa walimu bado wanatumia mbinu za ufundishaji zinazoegemea kwa mwalimu ambazo huenda kinyume na mbinu zinazokuza ugunduzi na ambazo zinawawezesha wanafunzi kutumia mahitajiyao na vipaji ili kupata ujuzi na uwezo kupitia kujifunza binafsi (Tafsiri Yetu).

Tunakubaliana na maelezo ya watafiti hawa kwa kuwa MUU sasa hivi ni takribani miaka saba tangu uanze kutekelezwa katika elimu nchini Rwanda. Kwa kweli walimu wengi hasa wale waliokuwa wanafundisha kabla ya mwaka 2015, wangali na athari za Mtaala Unaoegemea katika Maarifa. Athari hizo hudhihirika wanapoandaa tahmini inayokidhi mapendekezo ya MUU. Hii ni kwa kuwa walimu ambao walizoea kutumia Mtaala Unaoegemea katika Maarifa walishindwa kubadilika na kuanza kutumia mbinu za ufundishaji mpya zinazopendekezwa na MUU.

Isitoshe washiriki wa utafiti walionesha kwamba wanashindwa kufundisha ipasavyo stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa sababu wanakabiliwa na changamoto kadhaaa. Changamoto zilizodhihirishwa ni pamoja na kutohusisha mambo wanayojifunza kwenye somo la fasihi na maisha ya kila siku, kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tafakuri bunifu, kushindwa kuandaa vema andalio la somo linalojumuisha stadi ya tafakuri bunifu, kushindwa kujumuisha tafakuri bunifu wakati wa ufundishaji, na pia kushindwa kuitathimini vema stadi ya tafakuri bunifu. Ili kukabiliana na changamoto hizi, tuliamua kuunda mwongozo wa ufundishaji ambao unaweza kufuatiliwa na walimu kuimarisha ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi.

### 4.3 Mwongozo wa Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu kupitia Fasihi

Sehemu hii imechagizwa na lengo mahususi la pili la utafiti wetu lililokusudia kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo hili, mosi, tulijiegemeza kwenye mhimili wa pili wa Nadharia ya Utambuzi ya Piaget (1983) usemao kwamba unapomfundisha mtoto kitu bila kumshirikisha katika ujifunzaji, unamnyima milele nafasi yake ya

kugundua mwenyewe. Pili, tuliongozwa na mhimili wa tatu wa Nadharia ya Utambuzi ya Piaget (1983) unaosema kwamba utatuzi wa matatizo, unategemeana na utambuzi, ubunifu wa binadamu na ugunduzi wa kisayansi. Kwa kujiegemeza kwenye mihimili ya Nadharia ya Utambuzi, kwanza, tulipendekeza mbinu za kufundishia stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Pili, tulionesha mwongozo wa ufundishaji wa stadi ya tafakuri kupitia fasihi. Tatu, tulijadili mikakati ya ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi, na mwisho, tulionesha mfano wa ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

### 4.3.2 Namna ya Ufundishaji wa Stadi za Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi

Ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu ni jambo linalohitajika hasa katika elimu inayotolewa kwenye karne ya ishirini na moja. Kuna mbinu kadhaa ambazo ni bora sana katika ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu. Mbinu hizo ni pamoja na utumiaji wa taswira, drama bunifu, sitiari na analojia (Nagamurali, 2013).

Mbinu hizi kwanza zilionekana kama mbinu ambazo zinaweza kufaa katika kukabiliana na changamoto zilizodhihirishwa na walengwa wa utafiti. Hapo chini, tunaeleza namna ambavyo mwalimu wa fasihi anavyoweza kutumia kila mbinu ili kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

#### 4.3.2.1 Ufundishaji Unaotumia Taswira

Data zilizopatikana wakati wa ukusanyaji wa data kupitia uchanganuzi wa matini, taswira ilielezwa na Nagamurali (2013) kama mbinu ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu ambayo humsaidia mwalimu kuweka picha za vitu visivyoonekana akilini mwa wanafunzi. Picha hizi ambazo wanafunzi hujenga akilini zinawasaidia kupanua uwezo wao wa kufikiri.

Kwa mfano, wakati wa ufundishaji wa riwaya ya Adili na Nduguze, mosi, mwalimu anaweza kuomba kila mwanafunzi kufumba macho na kufikiri kuhusu picha ya “mji wa mawe” ambao unasimuliwa katika riwaya ya Adili na Nduguze. Baada ya dakika tatu, mwalimu anaweza kuomba kila mwanafunzi kuandika kwenye daftari la mazoezi maelezo mafupi kuhusu picha ya “mji wa mawe” aliyounda akilini mwake. Pili, wanafunzi wanaweza kuwekwa kwenye makundi ya wanafunzi watano watano na kufanya zoezi la kulinganisha na kulinganua maelezo ya picha ya kila mwanafunzi aliye kundini. Wakati wa kufanya zoezi hili, mwalimu ana wajibu wa kukagua ili kuhakikisha kila mwanafunzi anashiriki ipasavyo na kutoa msaada pale panapohitajika. Baada ya dakika takribani ishirini, kila kundi linaweza kupewa nafasi ya kuwasilisha waliyoyafanya kwenye makundi yao. Tatu, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi ruhusa ya kuuliza maswali katika kila kundi linalowasilisha. Baada ya kufanya muhtasari na kupata suluhisho kuhusu somo, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi kazi ya nyumbani ifuatayo:

“Kwa kujiegemeza kwenye picha ya “mji wa mawe” uliyounda akilini mwako, linganisha na ulinganue picha hiyo na picha ya mji mwingine unaojua katika nchi ya Rwanda.”

Hivyo basi, mwalimu anapofuata mbinu hii ya utumiaji wa taswira katika ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi, atafanikiwa kwa sababu taswira ni mbinu ambayo inashirikisha wanafunzi kwa kiasi kikubwa na kuwapa uwezo wa kutatua matatizo yanayokabili maisha yao. Jambo hili linaunga mkono mhimili wa Nadharia ya Utambuzi usemao kwamba utatuzi wa matatizo unategemea na utambuzi, ubunifu wa binadamu na ugunduzi wa kisayansi.

#### 4.3.2.2Ufundishaji Unaotumia Drama Bunifu

Mbinu ya drama bunifu ni mbinu ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu ambayo hulenga kuamsha moyo na kichwa cha mwanafunzi (Magret, Khj). Mbinu hii inapotumiwa katika darasa la fasihi inafanikisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa inakuwa kama mchezo ambao huwamotisha wanafunzi na kuwakuzia uwezo wa ubunifu na ugunduzi.

Kwa mfano, mwalimu anapofundisha fasihi, anaweza akawagawanya wanafunzi katika makundi ya wanafunzi sitasita. Baada ya kuwaweka wanafunzi kwenye makundi, mwalimu anaweza kuomba wanafunzi kutunga mchezo wa kuigiza ambao unaweza kushiriki katika utatuzi wa tatizo fulani linaloikabili jamii. Hapa, wanafunzi wanaweza wakatunga mchezo wa kuigiza kuhusu mapenzi, uchumi, utandawazi, utamaduni nakadhalika.

Baada ya kutunga mchezo wa kuigiza, mwalimu anaweza kuwaomba kila kundi kuja mbele na kuigiza mchezo ambao wametunga mbele ya wenzao darasani. Baada ya maigizo ya kila kundi, kwa kujiegemeza kwenye mchezo ulioigizwa, mwalimu anaweza kubahatika kutoa tathmini ambayo inaweza kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Yafuatayo ni baadhi ya maswali ambayo anaweza kuuliza kuhusu kila mchezo unaoigizwa: A) Mchezo ulioigizwa ulihusu nini? B) Jadili tabia za mhusika aliyekupendeza na mhusika ambaye hakukupendeza katika mchezo ulioigizwa. C) Dhihirisha tatizo lililomo katika jamii unamoishi ambalo linaweza kutatuliwa kwa kutumia mchezo ulioigizwa. D) Tathmini umuhimu wa mchezo ulioigizwa katika maendeleo endelevu ya wanajamii. E) Tunga methali tano zinazohusiana na mchezo ambao uliigizwa.

Maelezo ya hapo juu yanaonesha kuwa kwa kufuata mbinu ya ufundishaji kwa kutumia drama bunifu, mosi, kila mwanafunzi anaweza kushiriki katika

ufundishaji na ujifunzaji. Pili, ubunifu wa mwanafunzi unapanuka. Tatu, kupitia drama bunifu, wanafunzi wanapendezwa na mazingira ya darasa. Na mwisho, mbinu hii huweza kuwasaidia walimu kuandaa tathmini ambazo zinatathmini stadi ya tafakuri bunifu.

#### 4.3.2.3Ufundishaji Unaotumia Sitiari na Analojia

Sitiari na analojia ni mbinu za ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu zinazosisitia uboreshaji wa mbinu iliyotumiwa katika utatuzi wa tatizo fulani ili kutatua tatizo jingine (Nagamurali, Khj). Mbinu hii imedhihirishwa kama mbinu bora ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa kuwa inasisitiza fikra, aina ya fikra na uzito wa fikra inayotolewa. Mbinu hii ni rahisi kutumiwa kutokana na kuwa haihitaji uwezo wa kiuchumi wa hali ya juu.

Katika darasa la fasihi, mwalimu anapofundisha riwaya ya *Adili na Nduguze*, anaweza kuwaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watanowatano. Kisha, anaweza kuwaomba wanafunzi kuchunguza kwa makini mbinu iliyotumiwa na Mfalme Rai wa Ughaibu kutatua migogoro iliyokuwapo kati ya Adili na nduguze ambao walitoka uhayawani wakawa watu.

Aidha, mwalimu anaweza akatumia baadhi ya maswali yafuatayo: A) Mfalme Rai wa Ughaibu alitumia mbinu bora kutatua migogoro kati ya Adili na nduguze, Jadili. B) Ungekuwa Mfalme Rai wa Ughaibu ungetumia mbinu gani kati ya Adili na nduguze? C) Tathmini namna ambavyo mbinu zilizotumiwa na Mfalme Rai zisivyoweza kutumiwa katika kutatua matatizo yanayojitokeza katika jamii unamoishi. D) Rekebisha mbinu zilizotumiwa na Mfalme Rai ili ziweze kufaa katika utatuzi wa migogoro inayodhihirika katika jamii yako.

Wakati wa kujibu maswali haya, mwanafunzi atalazimika kufikiri kwa kina ili kutathmini na kuboresha mbinu iliyotumiwa na Rai ili iweze kufaa katika utatuzi wa matatizo yanayoikabili jamii anamoishi mwanafunzi. Katika kufikiri kwa kina, mwanafunzi atakuza uwezo wake wa ugunduzi na ubunifu. Maelezo haya yanaungwa mkono na Nagamurali (Khj) asemaye kwamba sitiari na analojia hushiriki katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu, utatuzi wa matatizo na ugunduzi wa kisayansi. Aidha, jambo hili linaendana na mhimili wa Nadharia ya Utambuzi iliyoongoza utafiti wetu inayosema kwamba utatuzi wa tatizo unategemea sana stadi ya tafakuri bunifu kwa kiwango kikubwa kwa kuwa ili tatizo litatuliwe, ni lazima kuundwe hoja fulani zinazohusiana na tatizo lililopo.

#### 4.3.2.3 Ufundishaji Unaotumia Ushirikishaji wa Kina wa Wanafunzi katika Sanaa

Sanaa ni ufundi wa kuibua mawazo yanayokuwa katika fikra na kuyaonesha kupitia uchoraji, uchongaji, ufinyanzi, fasihi nakadhalika. Robert (2010) anaeleza kwamba ushirikishaji wa kina wa wanafunzi katika sanaa ni mbinu bora ya ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu hasa kwa vijana. Anaongeza kwamba sanaa inakuwa bora sana katika ufundishaji wa tafakuri bunifu kwa kukuza maendeleo ya uwezo wa utambuzi wa watoto. Hapo chini, tumeeleza namna ambavyo mbinu hii inavyoweza kutumiwa katika kuimarisha stadi ya tafakuri bunifu katika madarasa ya fasihi.

Kwa mfano, mwalimu anayefundisha fasihi (riwaya ya *Adili na Nduguze*) anaweza kuwaweka wanafunzi katika majozi. Mwanafunzi mmoja katika kila jozi akaombwa kuchora picha ya Adili na ya ndugu zake Adili. Baada ya muda mfupi, mwalimu anaweza kuomba wanafunzi kuweka maelezo kwenye picha walizozichora kutokana na tabia za mtu waliyemchora pichani.

Mwanafunzi ataandika tabia hii kwa kujiegemeza kwenye tabia zilizoelezwa katika riwaya. Baadaye, mwalimu anaweza kuomba kila jozi kuunganisha kazi, picha zenye maelezo walizozichora na kuelezeana sababu zilizomsukuma kila mtu kuchora alivyochora na kutoa maelezo aliyotoa. Baadaye, mwalimu anaweza kuomba kila jozi kubandika picha zenye maelezo walizozichora ukutani. Zaidi ya hayo, mwalimu anaweza kuwaruhusu wanafunzi kutembea darasani wakitazama picha zenye maelezo zilizobandikwa kwenye ukuta kwa jozi tofauti. Baadaye, mwalimu anaweza akawauliza wanafunzi maswali yafutayo: A) Je, kati ya Adili na nduguze ni nani ana tabia ya kuigwa na kila mtu? Eleza jibu lako. B) Kutokana na picha zenye maelezo ambazo umeziona ukutani, tabia kama za ndugu za Adili zina athari gani katika jamii? C) Tunga shairi huku ukisifu tabia za Adili. D) Kwa kujiegemeza kwenye tabia za ndugu zake Adili, tunga wimbo huku ukiyakashifu matendo mabaya waliyomtendea Adili.

Hivyo basi, kwa kushirikisha wanafunzi katika kazi za sanaa kwa kufuata mwongozo huu, kutawapa wanafunzi uwezo wa kujitegemea katika kuibua masuluhisho mapya ya kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo. Baada ya kujadili namna ambavyo walimu wanaweza wakatumia mbinu tofauti katika ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu, tulitaka kuunda mwongozo wa kufuatiliwa na walimu ili kufanikisha ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

### 4.3.3 Mwongozo wa Utumiaji wa Mbinu za Ufundishaji wa Tafakuri Bunifu Kupitia Fasihi

Katika sehemu hii, tulijaribu kuunda mwongozo ambao unaweza kutumiwa na walimu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Mwongozo huu ulijikita kwenye namna bora ya utumiaji wa mbinu za

ufundishaji ambazo zinasisitiza kumshirikisha mwanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kumpa uwezo wa kutatua matatizo anayokabiliana nayo. Hivyo basi, katika sehemu hii tumeonesha mwongozo wa kufuatiliwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa kutumia kazi za makundi, uigizaji, fikiri-jozi-changia na midahalo.

#### 4.3.3.1 Kazi za Makundi

Baada ya kufanya ushuhudiaji na kugundua kwamba ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi hukabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uwezo wa hali ya chini wa walimu kuhusu ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji na ujifunzaji, tuliunda namna ya kufundisha stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa kutumia kazi za makundi. Kazi za makundi ni namna ya kujifunza pamoja katika kundi dogo la watu wanne au watano ambao hushirikiana ili kufanya kazi walizopewa darasani. Pengine, kazi za makundi ni shughuli za kujifunza ambazo zinahusisha kikundi kidogo cha wanafunzi wanaofanya kazi pamoja. Makundi yote yanaweza kupewa kazi moja, au sehemu tofauti za kazi kubwa.

Wakati wa kufundisha fasihi kwa mfano, mwalimu anaweza akawagawanya wanafunzi kwenye makundi ya watu watanowatano, baadaye, kila kundi linaweza likapewa kazi ya kufanya. Mwalimu analazimika kuwapa wanafunzi mwongozo watakaofuata wakati wa kufanya kazi katika makundi. Baada ya kutoa mwongozo, mwalimu anapaswa kuchunguza ikiwa kila mwanafunzi anashiriki ipasavyo katika kufanya kazi makundini. Baada ya muda uliowekwa, mwalimu anaweza kuomba kila kundi kuja mbele na kuwasilisha waliyoyafanya kundini. Wakati wa uwasilishaji, mwalimu

anashauriwa kuwaruhusu wanafunzi kuliuliza maswali kundi linalowasilisha ili wapate uelewa wa kutosha kuhusu somo analofundisha.

Mwisho, mwalimu anaweza kushirikiana na wanafunzi katika kufanya muhtasari na kupata suluhisho kuhusu somo alilokusudia kufundisha.

Bila shaka, mwongozo huu wa utumiaji wa kazi za makundi ni mbinu bora ya ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi kwa kuwa unaweza kuwapa wanafunzi nafasi kubwa ya kushiriki katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Hili huendana na mhimili wa Nadharia ya Utambuzi ambao husisitiza ushirikishaji wa mwanafunzi katika elimu kama mbinu bora ya ukuzaji wa uwezo wake wa kugundua mambo tofauti. Pia, kazi za makundi hutazamwa kama mbinu ya kufundisha stadi za tafakuri bunifu kupitia lugha kutokana na kwamba huwamotisha wanafunzi na kuwapa fursa ya kuonesha kile wanachokijua. Maelezo tuliyayotoa hapo juu hayaendi mbali na matokeo ya utafiti uliofanywa na Brown (2001: 23) kuhusu mikakati ya ufundishaji wa lugha kama asemavyo:

> Wakati wanafunzi wanapokuwa katika makundi, wanahisi usalama katika ujifunzaji. Hawawezi kukosolewa au kudhalilishwa kwa urahisi. Wanafunzi waliozuiwa kushiriki nao wanapata nafasi ya kushiriki katika mchakato wa kujifunza na kufundisha. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wanafanya kazi pamoja ili kufikia malengo fulani. Kwa kufanya kazi katika makundi, motisha miongoni mwa wanafunzi, na kiwango cha kujiamini huongezeka (Tafsiri Yetu).

Dondoo hili linadhihirisha kwamba kazi za makundi ni mbinu bora inayoweza kutumiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia lugha kwa kuwa, mosi, huwashirikisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Pili, huwamotisha wanafunzi na kuwakuzia hamu ya kutaka kujua mengi zaidi ya waliyofundishwa. Mwisho, huwakuzia wanafunzi kiwango cha kujiamini. Hivyo basi, walimu wa fasihi wanashauriwa kutumia kazi za makundi ili kufanikisha ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi.

**4.3.3.2 Uigizaji**

Katika harakati za kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu, tulipendekeza uigizaji kama mbinu bora inayoweza kutumiwa na walimu wa fasihi ili kukuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Lengo kuu la ujifunzaji na ufundishaji ni kumweka mwanafunzi katikati ya mchakato wa elimu ili kumpa uwezo utakaomwezesha kushindana na kufaulu kwenye soko la ajira. Uigizaji ni mfano wa kuvutia wa mkakati wa kujifunza na kufundisha ambao humweka mwanafunzi katikati ya mchakato wa elimu na kumsaidia kukabiliana na changamoto tofauti. Kwa mujibu wa Osuafor (2015) Uigizaji ni njia ya mafundisho ambayo husaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao kisayansi, ubunifu na uwezo wa kukabiliana na changamoto za karne ya 21. Uigizaji unaweza kujumuisha michezo ya kuigiza, tamthilia, filamu, vichekesho, futuhi au komedi, utambaji hadithi, michezo, ngonjera, vibonzo jongefu na maandamano ya kesi halisi za maisha kuhusiana na mada tofauti.

Wakati wa uigizaji, mosi, wanafunzi wanaweza kuwekwa katika makundi mbalimbali. Pili, kila kundi linapewa seti ya maandishi yenye hatua za kufuatiliwa ili kufanya kitu fulani. Tatu, kila mwanafunzi katika kundi

anapewa kadi moja iliyo na hatua moja baadhi ya hatua kadhaa za kufanya kitu. Hapa, kila mwanafunzi analazimika kutafuta mshiriki wake kutokana na hatua inayoandikwa kwenye kadi yake. Nne, wanafunzi husoma kwa sauti maneno yaliyoandikwa kwenye kadi waliyopewa ili wapate washiriki wao. Baada ya kuweka kadi pamoja kwa kuzifuatanisha ipasavyo, wanafunzi wanaweza kuzalisha kazi ya fasihi kamili. Tano, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi kwenda mbele kuwasilisha waliyoyafanya katika uigizaji. Mwisho, mwalimu anaweza kutathmini ufahamu na uelewa wa wanafunzi juu ya somo alilotarajia kufundisha na kuwasaidia wanafunzi katika kufikia hitimisho.

Kwa kufuata taratibu hizi, wanafunzi wanaweza wakakuza stadi za tafakuri bunifu kiurahisi. Kupitia utumiaji wa uigizaji katika ufundishaji na ujifunzaji, ubunifu wa wanafunzi hukuzwa kwa kuwafanya wavutiwe na mazingira ya darasani na kwa kuwasaidia kuhusisha wanayofundishwa na maisha ya kila siku. Yanayoelezwa hapo juu, yanaungwa mkono na Usman (2015: 101):

> Kutumia uigizaji darasani huwahimiza wanafunzi kutumia lugha lengwa katika hali halisi ya maisha. Mchezo huwafanya wapendezwe na mazingira ya darasani wafurahie kujifunza. Jambo hili linapotendeka, ujifunzaji hufanyika bila kizuizi (Tafsiri Yetu).

Dondoo hili linaonesha kwamba matumizi ya uigizaji katika ufundishaji huwapa wanafunzi nafasi ya kutumia ujuzi walioupata shuleni katika hali halisi za maisha. Maelezo haya hayatofautiani na maoni ya Nadharia ya Utambuzi yasemayo kwamba binadamu ana tabia na uwezo unaomwezesha kuitikia na kuiga matendo na maitikio mengine ya wanaomzunguka ili

kukabiliana na mazingira anamoishi. Hivyo basi, uigizaji humpa mwanafunzi uwezo wa kuiga matendo na kuitikia matendo ya wanajamii ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili wanajamii. Kwa hiyo, uigizaji ni mbinu muhimu inayoweza kutumiwa na walimu hasa wa fasihi kwa madhumuni ya kukuza ubunifu miongoni mwa wanafunzi.

#### 4.3.3.3 Fikiri-Jozi-Changia

Baada ya kushuhudia walimu wakifundisha na kuona namna ambavyo walimu kadhaa husumbuka wakati wa kufundisha stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi, tuliunda mwongozo wa fikiri-jozi-changia kama mbinu bora mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Mbinu hii ni mbinu inayoweza kutumiwa na walimu wa fasihi ambapo mwanafunzi kwanza, hufikiri kuhusu kazi aliyopewa. Kisha, mwanafunzi hujiunga na mwenzake ili kumuonesha anayofikiri juu ya kazi waliyopewa. Mwisho, kila jozi huchangia na jozi nyingine.

Kwa kutumia mbinu ya Fikiri-Jozi-Changia, mosi, wanafunzi wanapewa maagizo kuhusu nini cha kufanya kuhusu kazi ya fasihi. Pili, mwalimu husambaza karatasi zenye maandishi kwa kila mwanafunzi. Kila karatasi inalazimika kuwa na sehemu moja ya kazi ya fasihi ambayo imegawanywa katika sehemu mbili. Tatu, mwalimu anawaomba wanafunzi kufikiri kibinafsi na kujaribu kuelewa kazi waliyopewa. Kwenye hatua hii, mwalimu analazimika kumkagua kila mwanafunzi ili kuhakikisha anajishughulisha na mchakato wa kufikiri ipasavyo. Nne, wanafunzi hufanya hatua ya kuoanisha kazi zao katika jozi kwa kusogelea wenzao ambao wamepewa karatasi zenye sehemu ya kazi ya fasihi tofauti. Hapa, mwalimu anapaswa kuchunguza ikiwa kila mwanafunzi yuko kwenye jozi inayofaa na kuwasaidia wanafunzi panapohitajika. Baadaye, mwalimu huomba kila jozi kuchangia na jozi

waliyokaribiana nayo kuhusu kazi ya fasihi waliyopewa. Tano, wanafunzi wanarudi kwenye jozi zao za mwanzo na kujadili kile walichopata kutoka katika jozi waliyokaribiana nayo. Mwisho, wawakilishi wa kila jozi wanaripoti matokeo ya majadiliano. Wanafunzi wengine wanaweza kutoa maoni na kuuliza maswali panapohitajika. Hivyo basi, kwa kufikiri, kushiriki jozini, kuchangia na wengine yaliyofanya, kuuliza na kujibu maswali, mwanafunzi hukuza ugunduzi na ubunifu wa kuzalisha mbinu mpya za kutatua matatizo. Jambo hili haliendi mbali ya mhimili wa tatu wa Nadharia ya Utambuzi ambao unasema kwamba utatuzi wa matatizo, unategemeana na utambuzi, ubunifu wa binadamu na ugunduzi wa kisayansi. Maelezo haya huenda sambamba na maelezo ya Rowe (1972) anayesema:

> Through Think-Pair-Share, students get time to think critically, creating a learning environment that encourages high quality responses (uk. 15).
>
> Wanafunzi hupata muda wa kufikiri kwa umakini, kujenga mazingira ya kujifunza ambayo yanahimiza majibu ya hali ya juu (Uk.15).

Utafiti wetu unakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Rowe (Khj) kwa kuwa wakati ambapo mwanafunzi anachangia fikra na wenzake katika majozi, anapata nafasi ya kudhihirisha kile ambacho anakiweza. Kupitia mbinu ya Fikiri-Jozi-Changia, mwanafunzi anapata motisha ya kufanya iwezekanavyo ili atoe jibu ambalo litashiriki katika utatuzi wa matatizo.

Mbinu ya Fikiri-Jozi- Changia pia, inaweza kufanikisha ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi hasa kwenye shule za sekondari nchini Rwanda ambapo kuna idadi kubwa ya wanafunzi. Hoja hii inatetewa na

maoni ya Judy & Leigh (2017:01) waliofanya utafiti kuhusu zana bora za kufundishia stadi tofauti. Wanasema:

> "Fikiri-Jozi- Changia (FJC) ni mbinu bora ya kufundishia kwa kuwa inaweza kuzaa matunda na hasa kwenye madarasa makubwa na kwa masomo tofauti (Tafsiri Yetu)".

Dondoo hili linathibitisha kwamba walimu wa fasihi wakitumia mbinu ya Fikiri-Jozi- Changia, wanaweza kufanikiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Maelezo yanayotolewa katika dondoo hili yana ukweli. Kama darasa lina wanafunzi wengi, mwalimu hana budi kutumia mbinu shirikishi. Kwa hiyo, mbinu ya Fikiri-Jozi- Changia ndiyo mbinu bora ambayo inaweza kutumiwa kwenye madarasa makubwa kwa kuwa inamnufaisha kila mwanafunzi kushiriki.

#### 4.3.3.4 Midahalo

Mbinu nyingine ambayo inaweza ikatumiwa na walimu wa fasihi kwa ajili ya kuhamasisha stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi ni midahalo. Kwa mujibu wa Hall (2011) Mdahalo ni mkakati wa elimu ambao unakuza uwezo wa kufikiri na pia huongeza ujuzi, maadili na imani kupitia utoaji wa hoja tofauti kuhusu mada fulani. Kwa mujibu wa Vo na Morris (2006), matumizi ya mdahalo katika elimu yanaweza kuwa yameanzishwa na Sophists na Aristotle katika karne ya tano ili kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi, mwalimu anaweza akawapa wanafunzi mada ya kufanyia mdahalo kuhusu fasihi na umuhimu wake katika utatuzi wa matatizo yanayokabili maendeleo ya wanajamii. Baada ya kutoa na kueleza mada, wanafunzi wanajigawa katika

makundi ya watetezi, wapinzani na wasikilizaji washiriki. Hapa, mwanafunzi mmoja anaweza akachaguliwa kama mwenyekiti na mwingine kama katibu. Baadaye, kila kundi linalazimika kutoa hoja zao kuhusu mada ya mdahalo huku wasemaji wakijiegemeza kwenye utafiti walioufanya au kwenye maarifa ambayo wametoa pahali tofauti.

Kupitia utafiti unaofanywa na wanafunzi, utafutaji wa hoja za kutoa kutegemeana na upande wanaoshikilia, na uchanganuzi wa hoja zinazotolewa na wanafunzi kutoka kwenye kundi tofauti, huwashirikisha wanafunzi. Mhimili wa kwanza wa Nadhari ya Utambuzi unaonesha kwamba unapomshirikisha mwanafunzi, unampa milele nafasi ya kukuza ugunduzi na ubunifu wake. Hivyo basi, mwanafunzi akishirikishwa katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji, anakuza uwezo wake wa kufikiri. Maelezo yetu kuhusu umuhimu wa mdahalo katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi hayaendi mbali na matokeo ya utafiti uliofanywa na Vargo (2012: 32) kuhusu umuhimu wa midahalo katika ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo ya utafiti wa Vargo (Khj) yanaonesha yafuatayo:

> "Matokeo ya tafiti kadhaa zilizotangulia yamefichua kuwa kutumia mdahalo katika elimu kunawawezesha wanafunzi kuwajibika katika masomo yao wenyewe kwani kunawapa wanafunzi fursa ya kujiandaa na kuwasilisha kazi zao kwa wanafunzi wenzao wengine. Kwa hivyo, matumizi ya mdahalo kama mbinu ya ufundishaji yanaungwa mkono na nadharia ya ufundishaji ambayo inasema kwamba wanafunzi hujifunza vizuri

wanapojifunza pamoja kwa kushirikiana (Tafsiri Yetu)".

Dondoo hili linaonesha kwamba mdahalo ni mbinu bora ya kufundishia stadi tofauti kwa kuwa huwapa wanafunzi uwezo wa kuwasilisha kazi zao binafsi kwa kushirikiana na wenzao. Kwa hiyo, midahalo ni mbinu bora ambayo walimu wa fasihi wanaweza kutumia ili kukuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Baada ya kuonesha mwongozo wa kufuatiliwa na walimu ili kukuza tafakuri bunifu kupitia lugha, tuliona kwamba ili kuwakabidhi walimu wa fasihi msaada wa kutosha katika ufundishaji wao wa tafakuri bunifu kupitia fasihi, ni bora kudhihirisha mikakati ya kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari.

### 4.3.4 Namna ya Kukuza Tafakuri Bunifu Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari

Kwa kutambua kuwa mfumo wa elimu ni jambo muhimu katika maendeleo endelevu ya kila nchi, ni lazima elimu itiliwe nguvu ili kuhakikisha ukuaji wa haraka wa maendeleo (Hwande na Mpofu, 2017). Ili kuboresha elimu ni lazima wapangaji wa elimu waandae mfumo wa kielimu ulio bora katika kukabiliana na changamoto zinazoikumba jamii.

Katika dunia hii inayotawaliwa na utandawazi, sayansi na teknolojia ni lazima wasomi wawe na uwezo wa hali ya juu wa kukabiliana na maisha ya enzi za leo kwa kufundishwa stadi za karne ya ishirini na moja. Ingawaje stadi za karne ya ishirini na moja ni nyingi, katika ukusanyaji wa data za utafiti wetu tulisisitiza kuhusu stadi ya tafakuri bunifu. Stadi ya tafukuri bunifu ilisisitizwa katika utafiti wetu kutokana na kuwa mihimili ya Nadharia ya Utambuzi iliyoongoza utafiti huu inaonesha kwamba stadi ya tafakuri bunifu inapaswa kuwa kiini katika elimu ya karne ya ishirini na moja. Hivyo basi, baada ya kuunda mwongozo wa ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu

kupitia fasihi, tulijaribu kudhihirisha mikakati kadhaa inayoweza kutumiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Ingawaje mikakati ni mingi kutegemeana na watafiti, sehemu hii inajiegemeza kwenye mikakati iliyopendekezwa na Abdulslam, Zainab na Ayoola (2014).

#### 4.3.4.1 Utumiaji wa Michezo ya Maneno

Kwanza kabisa, ili kuimarisha stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi, watafiti hawa wanapendekeza kwamba walimu wanaweza kutumia michezo kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia. Wanasema kwamba mwalimu anaweza kutumia zoezi la kuwaamsha wanafunzi linaloingizwa katika mchezo bunifu ambao utawachochea wanafunzi kuunganisha vizuri mchezo huo na mada ya somo ambalo mwalimu anatarajia kufundisha.

Kwa mfano, mwalimu anaweza kumpatia mwanafunzi neno moja na kumuomba atafute neno jingine linalohusiana na neno alilopewa. Abdulslam na wenzake (Whj) wanachukua mfano wa neno "kandanda," wakasema kwamba kwanza, kwa kutumia neno hili mwanafunzi anaweza kupendekeza neno "bao," mwingine akasema "wavu wa bao,' na mwingine akapendekeza golikipa. Kwa kujibu hivyo, msamiati wote unaohusiana na mpira wa miguu utagundulika kupitia mchezo wa maneno ambao umeanzishwa na mwalimu. Maelezo ya watafiti hawa tunayaunga mkono kutokana na kwamba mchezo huu wa maneno unaweza kumchochea mwanafunzi kufikiri sana ili aweze kugundua msamiati unaokaribiana na ule aliopewa. Hili huendana na mhimili wa Nadharia ya utambuzi usemao kwamba ubunifu si nakala ya ukweli, bali ni zao la mwingiliano wa mtu na mazingira anamoishi. Bila shaka, kwa kutumia mchezo wa maneno, mwanafunzi ataweza kukuza ubunifu wake.

Mbinu hii pia inaweza ikatumiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi.

#### 4.3.4.2 Utumiaji wa Maswali Bunifu na Kazi Wazi

Mkakati wa pili wa ufundishaji wa tafakuri bunifu uliopendekezwa na Abdulslam na wenzake (Whj) ni matumizi ya maswali bunifu na kazi wazi. Watafiti hawa wanasema kwamba ili mwalimu akuze stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi ni lazima awaulize maswali yatakayowaruhusu wanafunzi kueleza na kuonesha namna yao ya kufikiri badala ya kutumia maswali ambayo yanampasa mwanafunzi kujibu kwa neno moja au mawili tu. Kwa kuwafanya wanafunzi waeleze, wathibitishe na washawishi wenzao kukubali namna walivyofikia jibu sahihi, huwaongezea wanafunzi ujuzi, stadi, mawasiliano, uwezo wa kufikiri na uwezo wa kujitathmini wao binafsi.

Kuhusiana na maswali bunifu, Abdulslam na wenzake (Whj) wanaeleza kwamba matumizi ya maswali bunifu huwaruhusu wanafunzi kutumia ujuzi na uelewa kutokana na waliyofundishwa na waliyoyajua. Hivyo basi, walimu ni lazima wawape wanafunzi maswali bunifu yanayowawezesha wanafunzi kutoa mchango wao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Maelezo ya hapo juu yanaonesha kwamba kazi wazi na maswali bunifu ni mkakati ambao huwapa wanafunzi fursa ya kufanya kazi pamoja na wenzao kwa mbinu ya ushirikiano ili kukabiliana na matatizo.

#### 4.3.4.3 Matumizi ya Hadithi Duara

Abdulslam na wenzake (Whj) wanasema kwamba mkakati wa tatu wa ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu ni matumizi ya hadithi duara. Mkakati huu unaweza kutumiwa na walimu kwa kuwapa wanafunzi karatasi zenye umbo la duara na kuwaomba kuchora vitu vingi tofauti kwa kadri wanavyoweza ili kuwasaidia kuweka maelezo ya kutosha kwa kila

wanachokichora kwenye karatasi yenye umbo la duara. Kwa mfano, duara linaweza kugeuzwa na kufanywa kama uso wa mtu kwa kuongeza midomo, macho, pua na masikio. Pengine, duara linaweza kufanywa kama jua au tandabui nakadhalika.

Katika zoezi hili, mwalimu anaweza kuwaruhusu wanafunzi katika majozi kulinganisha na kulinganua waliyoyachora kwenye karatasi. Kutokana na kuelezeana, kulinganisha na kulinganua mambo waliyoyachora pamoja na maelezo yaliyotolewa, wanafunzi watakuwa wanaendeleza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwao kwa kuwa zoezi hilo litawaruhusu wanafunzi kuzalisha mawazo, kupendekeza dhana, kutumia ubunifu na kufikia matokeo mapya ya kiubunifu.

Kama inavyodhihirishwa na matokeo ya utafiti uliofanywa na Broudy (1977), mwanafunzi anapopewa mazoezi yanayomlazimisha kutumia akili yake binafsi ili kuzalisha fikra mpya, mazoezi hayo humsaidia sana kuendeleza ubunifu wake.

Maelezo ya hapo juu yana ukweli kwa kuwa mwanafunzi anapojaribu kutafakari juu ya swali fulani alilopewa na kulitafutia jibu bila kuongozwa na mwalimu au mtu mwingine, mwanafunzi ananufaika katika ukuzaji wa tabia ya kujitegemea katika kukabiliana na changamoto yoyote anayokabiliana nayo katika maisha.

#### 4.3.4.4 Matumizi ya Maswali ya Mafumbo

Isitoshe, Abdulslam na wenzake (Whj) wanasema kwamba mkakati mwingine wa ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu ni matumizi ya maswali ya mafumbo. Kama wanavyoeleza watafiti hawa, walimu wanaweza kufundisha stadi za tafakuri bunifu kwa wanafunzi kwa kuwauliza maswali ambayo yatawachochea kutumia ubunifu. Kwa mfano, mwalimu anaweza

kuwauliza swali la fumbo kwa kuwaomba wanafunzi kupendekeza kitu kinachoweza kutokea kama jambo fulani limefanywa. Swali kama hili linaweza kuwahimiza wanafunzi kuendeleza mawazo ambayo ni ya kiasili na yenye kusudi ambayo yanaboresha na kuongezea thamani kitu ambacho kinaweza kuishia sio kuwanufaisha wanafunzi pekee yao, bali kuwa na faida kubwa kwa kundi kubwa la wanajamii wengine. Walimu pia wanaweza kutumia mbinu ya kufundishia ambayo inawawezesha wanafunzi kujiuliza maswali wao wenyewe. Baadhi ya maswali hayo ni kama: "Hali hii inaweza kuendelezwa vipi*?"*

Mwalimu pia, anaweza kuleta sanduku ambalo lina vitu vinavyovutia ambavyo wanafunzi hawavijui. Vitu hivyo vinaweza kuwa ni picha, michoro au vitu vingine. Mwalimu anaweza kuleta vitu hivyo bila kueleza kitu chochote kuhusiana na vitu hivyo. Baada ya hapo anaweza kuwaruhusu wanafunzi kufungua sanduku na kuwaacha waangalie vilivyomo sandukuni.

Kwanza kabisa, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali kuhusu muonekano wa vitu vile, kisha akawaomba kujaribu kugundua kitu kinachohusiana na picha, michoro au vitu vingine walivyokuta sandukuni. Baadaye, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali yatakayowalazimisha kujaribu kuzalisha kitu kipya kutokana na vitu walivyoona sandukuni. Ili kufanikisha jambo hili, kila mwanafunzi atakayetambua kitu, alazimishwe kutoa maelezo.

Hapo mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi kutafakari juu ya maelezo yaliyotolewa na mwenzao. Wanaweza kuyaunga mkono au kutoyatetea kwa njia ya mdahalo ambao huzalisha hoja nyingi muhimu. Baada ya kupata hoja tofauti, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi kupendekeza kitu kingine kifananacho na vile vya sandukuni au kitu kinachoweza kutumiwa kama kitu

walichotoa sandukuni. Zaidi ya hayo, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi kupendekeza jinsi kitu kile kinavyoweza kuboreshwa na pahali pengine kinapoweza kutumiwa. Hapa ikumbukwe kwamba wajibu wa mwalimu si hazina ya maarifa, bali mwalimu hapa, ana wajibu wa kusaidia wanafunzi kama mfasili, mwelekezaji na mrahisishaji. Kwa kufanya haya, bila shaka stadi za tafakuri bunifu zinaweza kuimarika kiurahisi. Utumiaji wa mbinu hii unaonekana kama mkakati bora wa kufundisha stadi za tafakuri bunifu. Mkakati huu pia unapotumiwa na walimu wa fasihi, unaweza kuzaa matunda katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Ijapokuwa mkakati huu umeelezwa na Abdlslam na wenzake (Whj) kama mkakati bora wa ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu, mkakati huu unahitaji nyenzo, vifaa vya kujifunzia na kufundishia ambavyo baadhi ya shule haziwezi kuvipata. Hii ni changamoto kubwa ambayo yaweza kuwazuia walimu kutumia mkakati huu.

Maelezo haya hayatofautiani sana na maelezo yaliyotolewa na Muraraneza & Mtshali (2018: 55) waliofanya utafiti kuhusu utekelezaji wa MUU nchini Rwanda. Matokeo ya utafiti wa watafiti wa hapo juu yanadhihirisha kuwa uhaba wa vifaa vya kufundishia ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa MUU nchini Rwanda. Wanasema:

> "Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kuhusu MUU katika shule ni kizuizi kingine ambacho huzuia utekelezaji wa mbinu mpya za ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya vifaa vilivyopo bado nakala za kielektroniki ambazo si rahisi kuzitumia (Tafsiri Yetu)."

Dondoo la hapo juu linaonesha kuwa uhaba wa vifaa vya kufundishia ni channgamoto kubwa ambayo inaweza kuathiri ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Kwa kweli, katika utekelezaji wa MUU, mwalimu anahitaji

vifaa tofauti ili kutimiza malengo ya ujifunzaji na ufundishaji. Ingawaje vifaa tofauti vinahitajika katika mafanikio ya sekta ya elimu, shule nyingi nchini Rwanda hazina uwezo wa kiuchumi wa kupata vifaa hivyo. Changamoto hii pia, inaukabili ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

Baada yakudhihirisha mikakati ya kukuza tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari, sehemu inayofuata ni mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa mwongozo unaokuza tafakuri bunifu.

### 4.3.5 Mfano wa Namna ya Kufundisha Fasihi kwa Mwongozo Unaokuza Tafakuri Bunifu

Sehemu hii inazungumzia mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa mwongozo unaokuza tafakuri bunifu. Katika sehemu hii, tulichukua mfano wa ufundishaji wa riwaya ya Adili na Nduguze. Katika shule za sekondari nchini Rwanda, kuna kazi za fasihi tofauti ambazo hufundishwa ili kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Wakati wa ukusanyaji data, hasa wakati wa uchanganuzi wa matini, tulijikita kwenye kuchunguza mchango wa riwaya ya Adili na Nduguze katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu. Tuliamua kutumia riwaya hii kwa kuwa ndiyo ambayo ilionekana kuwa inatumiwa katika takribani shule zote zilizochaguliwa katika utafiti wetu.

Wakati wa uchanganuzi matini, tuliona kuwa kuna faida nyingi katika kufundisha riwaya ya Adili na Nduguze kwenye shule za sekondari nchini Rwanda kwa sababu inachangia sana katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

Kwanza kabisa, riwaya ya Adili na Nduguze huchangia katika ukuzaji wa udadisi miongoni mwa wanafunzi. Kama inavyoelezwa na Appleton (2015), udadisi ni elementi ya ukuzaji wa tafakuri bunifu ambayo inahusu utashi wa hali ya juu wa kutaka kujua mengi zaidi. Kwenye riwaya ya Adili na

Nduguze, Robert (2010) amewaumba wahusika kwa namna ambayo huweza kuzalisha udadisi miongoni mwa wasomaji kupitia kutamani kujua sababu iliyomsababisha msanii kuwapamba wahusika wake namna alivyowapamba. Kwa mfano, ukitazama namna ambavyo msanii anampamba mhusika ambaye ni Rai mfalme wa Ughaibu, utakuwa na hamu ya kutaka kujua mengi kuhusu alichokikusudia Robert (Khj).. Yafuatayo ni maelezo yanayoonesha sifa maalum ambazo mfalme Rai amepewa na msanii:

> Rai mfalme wa Ughaibu, alikuwa mfalme wa namna ya peke yake duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za watu wengine wa zamani zake. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama ngozi ya pundamilia. Katika theluthi ya kwanza alikuwa msuluhifu akapendwa na watu kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji wa wanyama, na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Sulemani akatiiwa na majini. Kutawala suluhu na mapenzi ya wanadamu, utunzaji wa wanyama na utii juu ya viumbe wasiioonekana kama majini hutaka uwezo mkubwa sana (Robert, 2010: 1).

Udadisi wa kutaka kujua mengi kuhusu sababu iliyomsababisha msanii kutoa sifa hizi huweza kuwasaidia wanafunzi kupanuka kiakili na kugundua kwamba katika jamii za Kiafrika, wafalme na malkia huchukuliwa kama watu ambao si wa kawaida na wenye nguvu za ajabu. Robert (Khj) alitumia sifa hizi ili kuonesha kwamba wafalme hawakuwa viongozi wa kisiasa tu, bali walikuwa viongozi wa ajabu wa kimafumbo na kidini. Pia, walikuwa na ishara za kiungu, za afya na ustawi wa wanajamii (Mbiti, 1999). Bila shaka ufundishaji wa sehemu hii huchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa elementi ya udadisi wa kutaka kujua mengi na hata kwa wahusika wengine waliotumiwa katika kazi hii ya fasihi. Kwa hiyo riwaya ya Adili na Nduguze

huweza kusaidia sana katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Rwanda.

Vilevile, riwaya ya Adili na Nduguze ni muhimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi kutokana na kwamba riwaya hii huweza kukuza ufyonzaji miongoni mwa wanafunzi. Ufyonzaji ni elementi ya ukuzaji wa tafakuri bunifu inayohusu uigaji wa maarifa, stadi na maadili. Riwaya ya Adili na Nduguze inawasaidia walimu kuwapa wanafunzi uwezo wa kumudu mbinu zilizotumiwa na Robert (Khj) katika utungaji wake na kuzifyonza ili kutunga kazi mpya za kifasihi andishi. Frank (2000) anadai kwamba fasihi andishi ni kichocheo bora cha ukuzaji wa uwezo wa uandishi wa kiubunifu; kwa hiyo anahimiza waelimishaji kuwa daraja la kuboresha ufundishaji wa fasihi andishi ili kuwawezesha wanafunzi kuwa watunzi wa siku zijazo wenye stadi bora za utungaji. Bila shaka kwa kuhakiki namna ambavyo Robert (Khj) alioanisha fani na mudhui katika riwaya ya Adili na Nduguze, wanafunzi wanakuziwa ubunifu wao kwa kuweza kufyonza na kuboresha zaidi yaliyofanywa na mtunzi kwa ajili ya kutunga kazi zao mpya za fasihi andishi katika lugha ya Kiswahili.

Ni vema kutosahau ukweli kwamba ufundishaji wa kazi ya fasihi kupitia riwaya ya Adili na Nduguze huchangia katika ukuzaji wa elementi ya tafakari kwa wanafunzi. Kama inavyoelezwa na Appleton (2015), uakisi ni elementi ya ukuzaji wa tafakuri bunifu inayokusudia kudadisi maarifa binafsi ya kitaaluma na kuwawezesha wanafunzi kupiga hatua ili kutatua matatizo yanayoikabili jamii wanamoishi. Appleton (Khj) anaongeza kwamba uakisi unahimiza uzalishaji wa mbinu mpya za kukabiliana na changamoto zinazoathiri maendeleo endelevu ya jamii husika. Tukichukua mfano wa riwaya ya Adili na Nduguze, wanafunzi wakiichambua, wanaweza kufahamu

changamoto zilizokuwa zinaikabili jamii ya kufikirika ya Ughaibu. Changamoto ya kwanza ilikuwa ukosefu wa uongozi bora.

Ili kukabiliana na changamoto hii, Robert (Khj) alimuumba mhusika mfalme Rai ili kuonesha mfano bora wa kiongozi anayehitajika kwa kuhimiza kuwa tabia ya uadilifu katika uongozi ni mhimili wa maendeleo. Zifuatazo ni baadhi ya sifa za kiongozi bora zilizotolewa na msanii kuhusu mfalme Rai:

> Rai mfalme wa Ughaibu, alikuwa mfalme wa namna ya peke yake duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za watu wengine wa zamani zake. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama ngozi ya pundamilia. Katika theluthi ya kwanza alikuwa msuluhifu akapendwa na watu kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji wa wanyama, na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Sulemani akatiiwa na majini. Kutawala suluhu na mapenzi ya wanadamu, utunzaji wa wanyama na utii juu ya viumbe wasiioonekana kama majini hutaka uwezo mkubwa sana. Alikuwa kiongozi muadilifu na mfalme mwema sana. Hakusita kufanya kazi ndogo wala kubwa kwa mikono yake mwenyewe. Kazi nyingi za ufalme alizitenda yeye mwenyewe. Zile ambazo hakuwahi kuzitenda yeye mwenyewe alipenda kuziona kwa macho yake zilivyofanywa. Kwa bidii zake kubwa aliweza kushiriki

> katika mambo mengi ya maisha akasaidia maendeleo makubwa ya nchi yake. Hakulazimisha mtu yeyote kutenda tendo fulani, lakini alishawishi kila moyo wa mtu kuiga alivyotenda kwa hiyari yake mwenyewe. Alikuwa na mvuto mkubwa juu ya mioyo ya watu. Alitumia mvuto huu juu ya watu mpaka nchi yake ilikuwa haina mvivu, goigoi wala mwoga. Ilikuwa si desturi ya Rai kusema maneno na kuacha watu wengine watende matendo, lakini alitenda matendo akaacha watu wengine waseme maneno. Tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno. Haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana upesi, lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka. Rai alifahamu haya lakini watu wake hawakufahamu. Hawa walipaswa kuamshwa katika usingizi wao kwa matendo, sio kwa maneno. Maisha ya Rai yalipita katika matendo mbalimbali (Robert, 2010: 1).

Dondoo hili linaeleza kuwa Rai alikuwa mfalme mwenye utu na tabia njema. Anaonekeana kama suluhisho ya changamoto ya ukosefu wa uongozi bora inayokumba baadhi ya jamii duniani hasa barani Afrika.

Changamoto nyingine aliyokusudia kuitatua msanii iliyokuwepo katika jamii alimokuwa akiishi ni ukosefu wa utu katika jamii. Changamoto hii inadhihirishwa wakati wanafunzi wanapojifunza namna ambavyo ndugu zake Adili walivyotaka kumuoa mke wa Adili kama inavyoelezwa na dondoo hili:

> Usiku Adili alipokuwa amelala na jahazi inakwenda mbio kwa pepo za omo, ndugu zake walikuwa macho. Mawazo mabaya hurusha usingizi. Kuzinduka kwake Adili alijiona amechukuliwa hangahanga. Kufumbua macho aliona ndugu zake wamemfunga kifati. Mmoja alimshika kichwani na mwingine miguuni. Koo yake ilisongwa sana. Aliwauliza kwa pumzi nyembamba aliyoweza kuvuta neno walilotaka kumtendea. Alijibiwa,"Huss!, Fedhuli we! Wauliza neno ulijualo. Koma saa! Tumesalitika na mapenzi ya mwanamke aliye chomboni. Tumekushauri kumwoa shirika. Umekataa. Huna budi kufa." Alitoswa baharini kama kitu kilichokuwa hakifai (Robert, 2010:42).

Dondoo la hapo juu linaonesha kwamba Hasidi na Mwivu waliruhusu hisia zao zitawale uamuzi wao. Kwa kufanya hivi, walipoteza utu wao (Madoshi, 2015). Isitoshe, kwa kukabiliana na tatizo hili la ukosefu wa utu katika jamii, msanii alitumia tena mbinu ya kumuumba mhusika mfalme Rai wa Ughaibu ambaye alitumia jitihada ili kuwafanya ndugu zake Adili waepukane na maovu warejeshe utu miongoni mwao. Sehemu hii inapofundishwa shuleni, huwawezesha wanafunzi kukuza tafakari inayowawezesha kuzalisha mbinu mpya za kugundua na kutatua matatizo yanayoikabili jamii yao. Juhudi za Mfalme Rai zilizorejesha utu kwa ndugu zake Adili na kuwafanya wawe watu tena zilifanikiwa kama dondoo lifuatalo linavyoonesha:

> "Mara ile Huria alirudi kwa Adili akatangaza kuwa hoja ya Rai ilifaulu. Mfalme wa majini alikubali ndugu zake kuwa watu tena. Aliyakabili manyani akasema tokeni katika uhayawani mrudi katika utu. Walikuwa watu tena wakajiangusha miguuni mwa ndugu yao kuomba radhi. (Robert, 2010: 47)."

Kwa kujifunza haya, mwanafunzi anasaidiwa kuwa na uwezo wa kugundua matatizo yaliyomo katika jamii na kuweza kuzalisha mbinu mpya ya kukabiliana nayo mithili ya Adili na Rai mfalme wa Ughaibu. Hivyo basi, riwaya ya Adili na Nduguze ni riwaya muhimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu.

Vilevile, riwaya ya Adili na Nduguze huwasaidia walimu kuhimiza elementi ya tafakuri bunifu ambayo ni msukumo. Appleton (Khj) anasema kwamba msukumo ni elementi ya ukuzaji wa tafakuri bunifu inayohusiana na kumshawishi mtu na kumlazimisha mtu kufikiria na kutekeleza jambo ka kiubunifu. Kwa kweli, mwalimu anapofundisha namna ya kuihakiki riwaya ya Adili na Nduguze kwa kutumia mbinu zinazopendekezwa na MUU, wanafunzi watasaidiwa sana kukuza ubunifu wao kutokana na kwamba msanii Robert (Khj) alitunga riwaya hii kwa kutumia lugha fiche ambayo inawalazimisha wanafunzi kufikiri kwa kina ili kugundua alichotarajia kumaanisha. Katika pilikapilika za kugundua alichokusudia kumaanisha msanii, wanafunzi watajiraghbisha kufikiria na kutekeleza mambo mapya hasahasa wakilenga kuiga ili kuboresha zaidi waliyojifunza kupitia riwaya ya Adili na Nduguze.

## 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura ya nne inahusu mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura hii, mosi, ilijadili nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa tafakuri bunifu. Katika sehemu hii, tuliona kuwa baadhi ya walimu wa fasihi katika shule za sekondari nchini Rwanda hawafanikiwi kufundisha tafakuri bunifu kupitia fasihi. Pili, katika sura ya nne, tuliunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi.

# SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika sehemu tano ambazo ni utangulizi, muhtasari wa matokeo ya utafiti, ufaafu wa nadharia ya utafiti iliyotumika, hitimisho na mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Tasnifu hii ilikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni kubainisha nafasi ya fasihi andishi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda, na pia kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza katika tasnifu hii lilikuwa kubainisha nafasi ya fasihi andishi ya Kiswahili katika ukuzaji wa tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Matokeo ya utafiti kuhusu lengo hili yanaonesha kuwa walimu wa fasihi hawana uwezo wa kutosha wa kutumia fasihi kama nyenzo ya kukuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari. Jambo hili linadhihirishwa na matokeo ya utafiti.

Mosi, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa idadi kubwa ya walimu haina uwezo wa kuzijumuisha stadi za tafakuri bunifu katika andalio la somo kutokana na ukosefu wa uelewa kuhusu utekelezaji wa MUU pamoja na

majukumu mengi yanayowasababisha walimu kutopata muda wa kutosha wa kuandaaa masomo ipasavyo.

Pili, matokeo ya utafiti yanatuonesha kwamba ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji wa fasihi kwa shule za sekondari nchini Rwanda ungali kwenye kiwango cha chini. Kutohusishwa kwa stadi za tafakuri bunifu katika ufundishaji kulihusishwa na walimu wengi ambao hawana uelewa wa kutosha kuhusu tafakuri bunifu na stadi nyingine muhimu zinazopendekezwa na MUU. Ilionekana pia kuwa,ingawa walimu walihudhuria mafunzo tofauti kuhusu utekelezaji wa MUU, kungali idadi kubwa ya walimu walioshindwa kubadilika.

Mwisho, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa walimu wa shule za sekondari wanashindwa kuzijumuisha stadi za tafakuri bunifu katika tathmini kwa sababu wakati wa kuandaa tathmini, walimu wanaathiriwa na mtaala wa kielimu ulioutangulia huu wa MUU.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo la pili la utafiti wetu lilikuwa ni kuunda mwongozo wa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Ili kutimiza lengo la pili la utafiti wetu, mosi, tulijiegemeza kwenye mihimili tofauti ya Nadharia ya Utambuzi, tukaunda mwongozo wa ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi. Tuliunda mwongozo bora wa mbinu unaoweza kutumiwa na walimu wa fasihi ili kukuza stadi za tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Mwongozo tuliounda ni ule ambao unakuza ubunifu wa mwanafunzi kwa kumshirikisha katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kumpa uwezo wa kukabiliana na changamoto kadhaa zinazoweza kukabili jamii anamoishi. Mwongozo huo ni wa kutumia kazi za makundi, uigizaji, mbinu ya fikiri-jozi

na changia na midahalo. Pili, tulijadili mbinu nyingine zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kutegemeana na mwongozo tuliotoa. Mbinu hizo ni kama vile Utumiaji wa michezo ya maneno, utumiaji wa maswali bunifu na kazi wazi, matumizi ya hadithi duara na matumizi ya maswali ya mafumbo. Zaidi ya hayo, tulijadili mfano wa namna ya kufundisha fasihi kwa mwongozo unaokuza tafakuri tunduizi. Katika sehemu hii, tulichukua mfano wa ufundishaji wa riwaya ya Adili na Nduguze. Utafiti unaonesha namna ambavyo riwaya ya Adili na Nduguze huweza kushiriki katika ukuzaji wa elementi za tafakuri bunifu.

## 5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika

Katika utafiti wetu, nadharia ambayo tuliamua kutumia ni Nadhari ya Utambuzi iliyoasisiwa na Piaget (1983). Nadhari ya Utambuzi imetumika kwa kiasi kikubwa katika utimizaji wa malengo ya utafiti wetu. Ili kudhihirisha namna ambavyo stadi za tafakuri bunifu hukua, mosi, Nadharia ya Utambuzi inasisitizia kumshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji kama mbinu bora ya kukuza uwezo wa kufikiri na kugundua. Pili, Nadhari ya Utambuzi inaonesha kuwa ubunifu si nakala, lakini ni zao la mwingiliano wa mtu na mazingira anamoishi. Zaidi ya hayo, Nadharia ya Utambuzi inaeleza kwamba utatuzi wa matatizo, unategemeana na utambuzi, ubunifu wa binadamu na ugunduzi wa kisayansi. Isitoshe, nadharia hii inaeleza kwamba stadi ya tafakuri bunifu ni lazima isisitiziwe katika elimu ya karne ya ishirini na moja.

Nadharia ya Utambuzi ilitufaa sana katika kupata matokeo ya utafiti. Kwa upande na nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa tafakuri bunifu, Nadharia ya Utambuzi imetusaidia kugundua kwamba walimu wanashindwa kujumuisha stadi ya tafakuri bunifu katika maandalio ya masomo, ufundishaji na katika

tathmini. Jambo hili lilihusishwa na uelewa na uwezo wa hali ya chini wa walimu wa fasihi kuhusu ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kama unavyopendekeza MUU. Aidha, tuligundua kuwa ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi haufanikiwi kutokana na changamoto kadhaa zikiwemo ukosefu wa uelewa wa walimu kuhusu utekelezaji wa MUU, muda mfupi, majukumu chungu nzima wanayopewa walimu, lakini pia kuwapo kwa walimu walioshindwa kubadilika ili kuendana na MUU.

Kwa upande wa mwongozo wa ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi, Nadharia ya Utambuzi imetusaidia kuunda mwongozo ambao unafaa kufuatiliwa na walimu wa fasihi ili kuimarisha tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi. Zaidi ya hayo, Nadharia ya Utambuzi ilituwezesha kuonesha mikakati inayoweza kufanikisha ufundishaji wa tafakuri bunifu kupitia fasihi.

Mikakati hii inasisitizia kuwashirikisha wanafunzi katika ufundishaji ili kuwakuzia uwezo wa kuzalisha mbinu mpya za kukabiliana na changamoto zinazokabili jamii wanamoishi. Mwisho, Nadharia ya Utambuzi ilituongoza katika kudhihirisha mfano wa ufundishaji wa fasihi unaoshiriki katika ukuzaji wa stadi ya tafakuri bunifu.

## 5.4Hitimisho

Utafiti huu umefanikiwa kukamilisha lengo lake kuu baada ya kukamilika kwa malengo mahususi yote mawili. Katika utafiti wetu, ilionekana kuwa fasihi ina nafasi kubwa katika ukuzaji wa stadi za tafakuri bunifu. Utafiti wetu ulikuja kama suluhisho kwa changamoto kadhaa zinazokabili ufundishaji wa tafakuri bunifu ambazo ni pamoja na: walimu kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu na utekelezaji wa MUU, muda mfupi wa kuandaa kazi za ufundishaji na

majukumu mengi ambayo walimu wanapaswa kutimiza. Utafiti wetu unakabilana na changamoto hizi kwa kubainisha mwongozo unaopaswa kufuatwa na walimu katika ufundishaji wa stadi za tafakuri bunifu kupitia fasihi.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya utambuzi ambayo ilinusaidia kuchunguza namana ambavyo walimu hujumuisha stadi ya tafakuri bunifu katika ufundishaji, maandalio ya masomo na tathimini. Vilevile, dadharia ya utambuzi ilitufaa kuunga mwongozo wa ufundishaji kupitia fasihi.

## 5.5 Mapendekezo

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Bodi ya Elimu ya Msingi Nchini Rwanda

Wakati wa kufanya utafiti huu iligunduliwa kuwa kuna baadhi ya walimu ambao hawana uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kisasa ya ufundishaji. Ilidhihirika kuwa jambo hili husababisha na ukosefu wa mafunzo ya kutosha ambayo hupewa walimu.

Kwa hivyo, Bodi ya Elimu ya Msingi Nchini Rwanda wanashauriwa kutoa mafunzo na kozi ambazo zinalenga kuwawezesha walimu kukuza uwezo na ujuzi wao kuhusu ujumuishaji wa stadi za tafakuri bunifu na stadi nyingine zinazopendekezwa na MUU katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaj.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu Nchini Rwanda

Ili walimu wapewe masomo ya kutosha kuhusu ufundishaji wa tafakuri bunifu na utekelezaji wa MUU, kunahitajika vifaa tofauti pamoja na miundo mbinu inayohitaji uwezo wa kiuchumi ambao baadhi ya shule za sekondari nchini Rwanda haziwezi kupata.

Hivyo basi, Wizala ya Elimu nchini Rwanda inashauriwa kuongeza mchango wake katika mafunzo ya walimu kwa kuzipa shule uwezo wa kupata vifaa na miundo mbinu inayohitajika ili kuwapa walimu uwezo wa kujumuisha tafakuri bunifu kwenye ufundishaji maandalio ya masomo.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Walimu wa Fasihi

Walimu wana mchango mukbwa katika mafanikio ya sekta ya elimu. Ili stadi ya tafakuri bunifu iimarishwe kwa wanafunzi, walimu wanatakiwa kuwa na uwezo wa kutosha pamoja na uelewa unaofaa kuhusu mbinu bora za ufundishaji wa tafakuri bunifu pamoja na utekelezaji wa MUU.

Kwa kuwa walimu ndio nyenzo muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, wanatakiwa kufanya kila liwezekanalo ili wakuze uwezo wao na ujuzi wao kupitia ujifunzaji wa muda mrefu, usomaji nyaraka, kuhudhuria warsha tofauti na kufanya utafiti. Kwa hiyo, walimu wanalazimika kushiriki kama wafasili, warahisishaji na waelekezaji katika uhamasishaji wa stadi za karne ya ishirini na moja miongoni mwa wanafunzi.

### 5.5.4 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule

Vilevile, wakurugenzi na wakuu wa masomo shuleni wanalazimika kuwasaidia walimu ili waweze kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Tunapendekeza kuwa wakurugenzi na wakuu wa masomo waungane mkono na walimu pamoja na wadau wengine wote wa sekta ya elimu katika kutafuta vifaa na mbinu za kufundishia ili kukuza stadi za karne ya ishirini na moja.

### 5.5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Watafiti wengine wanatakiwa kufanya tafiti kuhusu mada zifuatazo: Mosi, watafiti wanatakiwa kufanya utafiti kuhusu ufundishaji wa stadi za karne ya

ishirini na moja kama vile tafakiri kupitia fasihi ili kudadisi namna ambavyo fasihi inaweza kufanikisha ufundishaji wa stadi hizo. Tunatoa pendekezo hili kwa kuwa stadi ya tafakuri tunduizi ni stadi yenye uhusianao na tafakuri bunifu ambayo ni lazima ifanyiwe utafiti

Pili, watafiti wengine wanapendekezwa kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa MUU kupitia fasihi huku wakidhihirisha uhusiano uliopo kati ya MUU na fasihi. Kwa kuwa ni zaidi ya miaka mitano tangu MUU uanze kutekelezwa nchini Rwanda, ni lazima kufanya tafiti kadhaa kuhusu MUU ili kutoa taarifa za kutosha kuhusu utekelezaji wa MUU.

Aidha, watafiti wanatolewa wito wa kuchunguza umuhimu wa stadi za tafakuri bunifu katika maendeleo endelevu ya wanajamii na changamoto zinazokabili ufundishaji wa stadi za karne ya ishirini na moja kupitia fasihi.Kwa kuwa ufundishaji wa enzi za sasa unakabiliwa na changamoto kadhaa, ni lazima watafiti wachunguze ikiwa stadi za karne ya ishirini na moja zinaweza kushiriki katika kukabiliana na changamoto hizo.

### 5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura ya tano ilihusu hitimisho la jumla la utafiti. Sura hii ilionesha muhtasari wa matokeo ya utafiti. Sura hii pia ilijadili ufaafu wa nadharia iliyoongoza utafiti huu, isitoshe, sura hii ilitoa mapendekezo kwa wadau wa elimu na watafiti wengine ili kuboresha ufundishaji wa stadi ya tafakuri bunifu kupitia fasihi.

## MAREJELEO


Abdulsalam, H., Zainab, A. & Ayool., A, A. (2014*)*. Strategies for Improving the Imaginative and Creative Competence of Students in secondary Schools. *British Journal of Education European Centre for Research Training and Development*, 2(3), 1-21.

Abler, W.L. (2013). *Isolating, Identifying and Defining the Uniquely Human Component of Mind*. *Cog Crit UMN*

Airasian, P. W. (1994). *Classroom Assessment*. New York: McGraw-Hill.

Appleton, S. (2015). *3 Elements of Creativity Writing*. Fantasy: Sci-Fi Mystery

Bagley, M. T. (1987). *Using imagery in creative problem solving*. New York: Trillium Press.

Ball, A., L., & Washburn, G.S. (2001). Teaching Students to Think: Practical Applications of Bloom's Taxonomy. *Agricultural Education Magazine,74*(3), 16.

Barman, A., & Konwar, J. (2011). Competency Based Curriculum in Higher Education: A Necessity Grounded by Globalization, *Revista Romaneasca Educatie, Multidimessionala*, *Year* 3( 6),7-15.

Birdi, K., Leach, D. & Magadley, W. (2012). Evaluating the Impact of TRIZ Creativity Training: an Organizational Field Study. *R&D Management*, 42(4), 315-326. doi: 10.1111/j.1467-9310.2012.00686.x

Birsen, B. (2019). Development of Creative Thinking Skills of Students through Journal Writing. *International Journal of Progressive Education,15(5).*

Bloom, B. (1956). *Taxonomy of Educational Objectives: The Classification of Educational Goals. Handbook 1: Cognitive Domain.* New York: David McKay.

Broudy, H., S. (1977). *Schooling and the Acquisition of Knowledge*. New Jersey: Erlbaum Associates Publishers.

Brown, H. D (2001). *Teaching by Principles. An Interactive Approach to Language Pedagogy*. New York: Longman.

Brundrett, M. (2017). *Bringing Creativity back into Primary Education*. Education 13(3), 105-107.

Chang, C., T. (2009). Developing Creative Thinking through Literature Reading. *Feng ChiaJournal of Humanities and Social Sciences*, *19*(3), 287-317

Creswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches.* Los Angeles: SAGE Publications.

Dahl, R. (1961). *James and the giant peach*. New York: Puffin Books.

Dowson, C. (2002). *Practical Research Methods*: A User-friendly Guide to Mastering Research Techniques and Projects. Oxford: How to Book Ltd.

Eskin, M. (2015). *Sorunlarımı Çözebilirim*. (I can Solve my Problems, in Turkish). Ankara: Turkish Psychological Association.

Fisher, R. (2004).What is Creativity? In Robert Fisher and Mary Williams (wahariri) Unlocking Creativity: *Teaching Across the Curriculum* 6–20. New York: Routledge.

Ford, C., & Gioia, D. (2000). Factors Influencing Creativity in the Domain of Managerial Decision Making. *Journal of Management*, *26*(4),705-32.

Frank, M. (2000). *If you are Trying to Teach Kids how to Write . . . You've Gotta Have this Book*! (Toleo la pili.). Nashville, TN: Incentive Publications.

Furlong, N. (2000), *Research Methods and Statistics*: *An Intregrated Approach*, New York: Hartcourt Colledge Publishers.

Guba, E.G., &Lincoln,Y.S.(1994).*CompetingParadigmsinQualitativeResearch.*In N.K.Denzin&. Zin & Y. S.Lincoln(Wahariri.),*Handbook of Qualitative* Research (pp.105-117).ThousandOaks,CA:Sage.

Hall, D. (2011). Innovative Teaching to Enhance Critical Thinking and Communication Skills in Healthcare Professionals. *Internet Journal of Allied Health Sciences and Practice*, 9 (3).

Heinig, R. B. (1992). *Creative Drama for the Classroom Teacher* (Toleo la nne.). Upper Saddle River, NJ: Prentice-Hall.

Hwande, E., & Mpofu, J. (2017). The Preparedness of Primary Schools to Implement the grade 3 New Curriculum in Zimbabwe: Case Study of Bulawayo etropolitan Primary Schools. *European Journal of Social Sciences Studies*, *5*(1), 9 – 19

IBE-UNESCO (2017). *External Report on Curriculum pilot Implementation*. Nairobi: UNESCO.

Jack, C. R. (2013). Creativity in Language Teaching. *Iranian Journal of Language Teaching Research* 1(*3*), 19-43.

James, S. (1960). *The Clock of God*. New York: The Macmillan Company.

Jones, R. (Ed.). (2012). *Discourse and Creativity*. Harlow: Pearson

Kaila, H. (2005). Democratizing Schools across the World to Stop Killing Creativity in Children*:* an Indian Perspective. *Counseling Psychology Quarterly*, 18, 1-6. doi:10.1080/09515.

Kaufman, J. C., & Baer, J. (2008). Gender Differences in Creative Thinking. *Journal of Creative Behavior*, 42 (2), 75-105. DOI: 10.1002/j.2162-6057.2008.

Kellie, S. (2019) *Competency-based Learning in Higher Education*. The University of Arizona Press:Arizona

Kharkhurin, A. V. (2010b). Sociocultural Differences in the Relationship between Bilingualism and Creative Potential. *Journal of Cross-Cultural Psychology*, 41, 776-783. http://dx.doi.org/10.1177/0022022110361777

Kiany, G.R., Mahdavy, B., & Ghafar S. R. (2011). Towards A Harmonized Foreign Language Education in Iran: National Policies and English Achievement. *Literacy Information and Computer Education Journal*, *2*(3), 462-469.

Kim, K. H. (2011). The Creativity Crisis: the Decrease in Creative Thinking Scores on the Torrance Tests of Creative Thinking. *Creativity Research Journal*,*23*(4), 285-295.

Komba, S., & Mwandanji M. (2015). Reflections on the Implementation of Competence Based Curriculum in Tanzanian Secondary Schools. *Journal of Education and Learning*, *4*(2), 45 -65.

Kombo, K.D. and Tromp, L.A.D. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *An Introduction.*Nairobi: Paulines Publishers.

Kothari, C.R. (2012). *Research Methodology- Methods and Techniques.* New

Delhi. Willey Eastern Limited.

Likisa, K.D. (2018). Challenges and Prospects of Competency-based Education: The Case of Adama Science and Technology University Alumni Students and Hawas TVET College, Adama, Ethiopia.*The Journal of Competency based Education*, *3*(2),1-7.

Madoshi, J. P. (2015).*Folk Narratives and the Reflection of (Utu) Humanness in Shaaban Robert's Adili na Nduguze*"*The Belogradchik Journal for*

*Local History, Cultural Heritage and Folk Studies*. Tanzania: University of Dodoma.

Mbarushimana, N., & Kuboja, J. M. (2016). A Paradigm Shift towards Competence-Based Curriculum: The Experience of Rwanda. *Saudi Journal of Business and Management Studies, 1*(1), 6–17.

Mbiti, J.S. (1999). *African Religions and Philosophy*. London: Heinemann.

Momanyi. J &. P.K. Rop (2019). Teacher Preparedness for the Implementation of Competency Based Curriculum in Kenya: A Survey of Early Grade Primary School Teachers' in Bomet East Sub-County. The Cradle of Knowledge: *African Journal of Educational and Social Science Research, 7(1)* AJESSR - ISSN 2304-2885-p, 2617-7315-

Muraraneza. C. G & Ntombifikile. M (2018) Implementation of Competency-based Curriculum in Pre-service Nursing education: Middle range theory: *International Journal of Arica Nursing Sciences* 8,53-58

Nagamurali E. (2013). Teaching Creative Thinking Skills. *International Journal of English Language & Translation Studies* 1(2), ISSN: 2308-5460 kutoka https://pdfslide.net/documents/teaching-creative-thinking-skills-full-paper.html

Neuman, W. L. (2009). *Social research methods: Qualitative and Quantitative Approaches* (Toleo la 7). Boston: Allyn & Bacon.

Osuafor, A. M. (2015).*Role - Play*: *An Effective Strategy for Teaching and Learning of Basic Science in Primary Schools*. Nnamdi Azikiwe: University Press.

Öztuna, V. (2004) Injection-Induced Contracture of the Quadriceps Femoris Muscle in Children. *Orthopedics*, 27, 65-66.

Peck, J. (2005).Struggling with the Creative class*" International Journal of Urban and Regional Research*,29,740–770

Piaget, J. & Garcia, R. (1983). *Psychogenèse et Histoire des Sciences.* Paris: Flammarion.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitamuli na Uandishi wa Tasnifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Robert, S. (2010). *Adili na Nduguze*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Robson, C. (2007), *How to do a Reserch Project*: *A Guide for Undergraduate Students*. Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Rowe, M. (1972). *Wait time and Rewards as Instructional Variables*: Their Influence on Language, Logic and Fate Control. Columbia University: New York.

Runco, M.A., & Jaeger, G. J. (2012). TheStandard Definition of Creativity, Creativity. *Research Journal, 24 (1),* 92-96.

Rwanda Education Board. (2015). *Competency-Based Curriculum-Summary of Curriculum Framework Pre-Primary to Upper Secondary.Kigali:Rwanda Education Board*. Imesomwa tarehe 15 Novemba 2021 kutoka kutoka http://reb.rw/fileadmin/competence_based_curriculum/syllabi/curriculum_framework_final_pri nted.Compressed.pdf

Sarika, K. (2020). NEP 2020 Challenges to Teachers' Education.*International Journal of Applied Research*, *6*(10), 420-424.

Sharon, K. (2019). Improving 21st-Century Teaching Skills: The Key to Effective 21st Century Learners. *Research in Comparative & International Education*,14 (1) 99–117.

Sitenei, C. (2020). *School Based Factors Influencing Implementation of CBC in Public Primary Schools In Kibera Sub-County, Nairobi City County, Kenya* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya: Haijachapishwa).

Sotco, K. & Mwandanji, M. (2015). Reflections on the Implementation of Competency based Curriculum in Tanzania Secondary Schools. *Journal of Education and Learning,4(2),*73-80.

Srinivasan, N. (2007). Cognitive Neuroscience of Creativity: EEG based approaches. *Science Direct, 42(1), 109-116. http://dx.doi.org/10.1016/j.ymeth.2006.12.008*

Torre, de la, S. (2009). La universidad que queremos. Estrategias Creativas en el Aula Universitaria [The University we want. Creative Strategies in the University classroom]. *Revista digital universitaria,* 10(12), 1067-1079

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Oxford University Press: Dar es saam.

Urban, K. (2007). *Assessing Creativity Thinking: A componential model*. In A. Tan, (Mhariri), Creativity: A handbook for teachers. Singapore: NJ: World Scientific Publishing.

Usman, K. (2015). Implementation of Group Work in the Classroom University. *Banda Aceh Lingua, 12*(1),97-106.

Vargo, S.P. (2012).Teaching by debate.*International Journal of Learning, Teaching and Educational Research*, 15(7), 110-126.

Vo, H. X., & Morris, R. L. (2006). Debate as a Tool in Teaching Economics: Rationale, Technique, and Some evidence. *Journal of Education for Business*, 81(6), 315-320.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Wizara ya Elimu. (2009). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari*. Taasisi ya Elimu Rwanda: Kigali

Wongnaa, C.A. and Boachie W. (2018). Perception and Adoption of Competency-based Training by Academicians in Ghana. *International Journal of STEM Education*, *5*(52), 1-13.

Yin, R. K., (1994), *Case Study Research: Design and Methods*, (Toleo la 2.) Thousand Oaks Calif:

Young, J. & Chapman, E. (2010): Generic Competency Frameworks: A Brief Historical Overview. *Education Research and Perspectives*, 37(1), 1-24.

# VIAMBATISHO

**Mpango Kazi**

| TATIZO | KAZI/ UKABILIAJI | WASHIRIKI | KIPINDI/MUDA |
|---|---|---|---|
| Upitiaji wa nyaraka kuhusu mada ya utafiti | Kupitia kihakiki kazi tofauti kuhusu mada ya utafiti | Mtafiti, msimamizi | Miezi minane (Februari-Septemba) |
| Uundaji wa mwongozo wa usaili na ushuhudiaji na uchanganuzi matini | Kuandaa maswali ya usali na mwongozo wa ushuhudiaji na uchanganuzi matini | Mtafiti na msimamizi | Mwezi mmoja(Octoba) |
| Kuomba ridhaa ya kufanya utafiti (Chuo na Wilaya) | Kuomba ruhusa ya kufanya utafiti kwa Chuo na kwa Wilaya ya Kicukiro nitakamofanyia utafiti | Mtafiti na msimamizi | Mwezi mmoja (Disemba) |
| Kufanya ushuhudiaji darasani | Kushiriki katika somo la Kiswahili kuangalia namna walimu wanavyofundisha fasihi ya Kiswahili. | Mtafiti, na Walimu washiriki wa Kiswahili | Mwezi mmoja (Januari) |
| Kufanya usaili | Kuhojiana na washiriki wa utafiti (Walimu wa Kiswahili). | Mtafiti, Walimu wa Kiswahili | Mwezi mmoja (Januari) |
| Kuchanganua matini | Kuchanganua kazi za | Mtafiti | Mwezi mmoja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | fasihi ya Kiswahili | | (Januari) |
| Uchambuzi wa matokeo ya utafiti | Kuchambua data zitakazotokana na ushuhudiaji na mahojiano na walengwa wa utafiti. | Mtafiti | Mwezi mmoja (Fabruari) |
| Uandishi wa Ripoti ya Utafiti | Kuandika Ripoti ya Utafiti | Mtafiti, msimamizi | Mwezi mmoja (Machi) |
| Uwasilishaji wa Ripoti ya Utafiti | Kuwasilisha Ripoti ya Utafiti. | Mtafiti, msimamizi, walimu na wanafunzi | Mwezi mmoja (Machi) |

**Mwongozo wa Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili**

1. Nini maana ya fasihi?
2. Nini maana ya tafakuri bunifu?
3. Nini maana ya Mtaala Unaoegemea katika Uwezo?
4. Ni namna gani stadi ya tafakuri bunifu huweza kukuzwa kupitia ufundishaji wa fasihi?
5. Eleza mchango wa Stadi ya tafakuri bunifu katika utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo.
6. Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unaijumuisha stadi ya tafakuri bunifu unapofundisha fasihi?
7. Je, kama mwalimu wa Kiswahili, unaijumuishaje stadi ya tafakuri bunifu unapofundisha fasihi?

8. Kama mwalimu wa Kiswahili, eleza mbinu unazotumia katika ufundishaji wa fasihi ili kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

**Mwongozo wa Mahojiano kwa Wakuu wa Masomo**

1. Nini maana ya stadi za karne ya ishirini na moja?
2. Nini maana ya stadi za tafakuri bunifu?
3. Nini maana ya Mtaala Unaoegemea katika Uwezo?
4. Eleza mchango wa Stadi ya tafakuri bunifu katika utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo.
5. Je, ufundishaji wa fasihi unaweza kuendelezastadi ya tafakuri bunifu kwa wanafunzi?
6. Je, walimu wa Kiswahili wanaijumuisha stadi ya tafakuri bunifu wanapofundisha?
7. Je, walimu wa Kiswahili wanaijumuishaje stadi ya tafakuri bunifu katika kazi zao za ufundishaji?
8. Kama mkuu wa masomo, pendekezambinu zinazotumiwa na walimu ili kukuza stadi ya tafakuri bunifu miongoni mwa wanafunzi.

**Mwongozo wa Ushuhudiaji kwa Walimu wa Kiswahili (Darasani)**

| **ELEMENTI ZA KUSHUHUDIA** | **MATOKEO** | |
|---|---|---|
| | **Ndiyo** | **Hapana** |
| Je, mwalimu anajumuisha udadisi anapoandaa mafunzo? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha udadisi anapofundisha fasihi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha udadisi anapotoa tathmini endelezi na jumuishi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha ufyonzaji anapoandaa mafunzo? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha ufyonzaji anapofundisha fasihi | | |
| Je, mwalimu anajumuisha ufyonzaji anapotoa tathmini endelezi na jumuishi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha msukumo anapoandaa mafunzo? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha msukumo anapofundisha fasihi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha msukumo anapotoa tathmini endelezi na jumuishi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha tafakari anapoandaa mafunzo? | | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mwalimu anajumuisha tafakari anapofundisha fasihi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha tafakari anapotoa tathmini endelezi na jumuishi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha stadi ya tafakuri bunifu anapoandaa mafunzo? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha stadi ya tafakuri bunifu anapofundisha fasihi? | | |
| Je, mwalimu anajumuisha stadi ya tafakuri bunifu anapotoa tathmini endelezi na jumuishi? | | |

## Barua ya Wilaya

Republic of Rwanda
City of Kigali

Ref. nº 17..588/07.01.16/22

Kigali, on 14 FEV 2022

**Mr. NIYIRORA Emmanuel**
**Tel: 0788416625**
**Email: emmaniyirora@gmail.com**

Dear Sir,

**Re: Your application for data collection authorization**

Reference is made to your letter dated on 18th January 2022 applying for data collection authorization in Kicukiro District/ City of Kigali on "***Enhancing creative thinking skills through literature teaching in secondary***";

We would like to inform you that your request is hereby granted. However, before starting your research, you must first introduce you to the **Administration of Kicukiro District,** and clarifying your need.

Sincerely,

**Joseph NIYONGABO**
**Director General of Corporate Services**

Cc:
- City Manager of the City of Kigali
- District Executive Administrator/ Kicukiro District

**KIGALI**

City of Kigali, P.O.Box 3527 Kigali, Hotline 3260, Email: info@kigalicity.gov.rw, Wbsite: www.kigalicity.gov.rw

**Kibali cha Chuo cha kufanya Utafiti**



UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

RESEARCH AND INNOVATION UNIT

Rukara, 14th January 2022
Réf: 03/DRI-CE/001/EN/gi/2022

**The District Executive Administrator**
**Kicukiro District**
**Kigali-City**
**Rwanda**

**Re: Research recommendation letter for Mr. Emmanuel Niyirora**

On behalf of the University of Rwanda-College of Education (UR-CE), I am pleased to introduce Mr. Emmanuel Niyirora, a post-graduate student at the School of Education of UR-CE. Mr. Niyirora is writing his thesis on: **"Enhancing Creative Thinking Skills through Literature Teaching in Secondary Schools: A Case study of Kicukiro District"** to complete his Master of Education in Kiswahili Education.

He wishes to analyze how literature teaching enhances creative thinking skills among Kiswahili learners in Kicukiro secondary schools. Thus, he is requesting permission to collect data from some selected secondary schools located in the Kicukiro district of Kigali city. The research participants are teachers of Kiswahili at the advanced level and Head-teachers of selected schools.

Mr. Niyirora's research project passed successfully through an internal collegial ethical process. Thus, the University of Rwanda-College of Education: Directorate of research and Innovation confirms that his research adheres to ethical standards and principles. Therefore, we kindly request you to accord him your cooperation in this research.

If you need more clarification, please do not hesitate to contact us at wrceresearchin@gmail.com. We very much hope to get your usual cooperation in serving our nation.

Yours sincerely.

COLLEGE OF EDUCATION — UNIVERSITY of RWANDA — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

Digitally signed by UR (Rukara, Directorate of Research & Innovation)
Date: 2022.01.17
Time: 10:05:10 +2'00

**Assoc. Prof. Eugene Ndabaga**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862

Cc:

- Principal, UR-CE
- Postgraduate Program Coordinator, School of Education
- Dr. Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw